kushughulikia changamoto mbalimbali zinazojitokeza ikiwa ni pamoja kuongeza ukubwa wa meli zinazobeba makasha. Kampuni ya CMA kuleta makasha matupu kuanzia mwezi Septemba 2024. Aidha, Timu ya Menejimenti ya TPA kukutana na Uongozi wa Kampuni za PIL, SINOTASHIP na MAERSK kuanzia mwezi Agosti, 2024; Kuhakikisha mitambo yote inafanya kazi kufikia mwezi Agosti 2024; Kufunga mtambo mmoja wa STS katika Bandari ya Mtwara ili kuendelea kuimarisha uhudumiaji wa shehena ya makasha; Kuongeza maeneo ya kuhifadhia makasha matupu ambapo maeneo miwili yameshatengwa na kuanzia mwezi Agosti maeneo hayo yataanza kufanyiwa maandalizi ya msingi ili kuongeza uwezo wa Bandari katika kuhifadhi makasha; Kuanza kwa Mikutano ya Wadau kuanzia ngazi ya Taasisi hadi kufikia Vikao vya Kitaifa kuanzia Mwezi Agosti 2024; Kukarabati barabara zote za ndani ili ziweze kupitika kirahisi kufikia mwezi Septemba, 2024; Kuongeza idadi ya "Terminal Tractors" ili kuongeza kasi ya kuhudumia shehena; Kushirikiana na Sekta Binafsi kufanyia baadhi ya shughuli za "Stuffing" nje ya Bandari ambapo Kampuni mbili zilikuwa zimejiandaa kutekeleza zoezi hilo; Kufanya Kampeni kwenye Vyombo vya Habari juu ya utayari wa Bandari kwenye kutekeleza zoezi hilo; Kufanya semina na Taasisi za Serikali juu ya wajibu na ushirikiano wa kila mdau anayeshiriki zoezi hilo na; Kuwa na Kandarasi za dharura za Ukodishaji wa Mitambo ili inapotokea changamoto kuwepo na uwezekano wa kupata mshitiri kwa wakati.

**Agenda Na 9.4 Taarifa kutoka Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB)**

Taarifa ilieleza kuwa katika kipindi cha misimu mitatu iliyopita kati ya 2021/22 hadi 2023/24 mikoa sita inayozalisha korosho Lindi, Mtwara, Morogoro, Pwani, Ruvuna na Tanga imekuwa ikiratibu mauzo yao kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

Katika kipindi hicho ukusanyaji wa korosho umekuwa ukipanda na kushuka kwa makusanyo ambapo msimu wa 2021/2022 ukusanyaji ulikuwa kilogramu 231,152,847; 2022/2023 ukashuka hadi kilogramu 176,747,460 na kuongezeka tena hadi kilogramu 252,670,448 msimu wa 2023/2024. Katika kipindi cha kati ya 2021/22 hadi 2023/24 mkoa wa Mtwara umekuwa ukiongoza kwa ukusanyaji ambapo kilogramu 358,257,547 zilikusanywa ukifuatiwa na Lindi kilogramu 191,683,183.

Ilielezwa kuwa katika kipindi cha mwaka 2021/22 na 2023/24, kati ya kilogramu 652,670,448 zilizopita kwenye mfumo upungufu ulikuwa kilogramu 4,937,185 sawa

na asilimia 0.77%. Ikilinganishwa na kipindi kuanzia 2015/16 hadi 2020/21 ambapo wastani wa upungufu ulikuwa asilimia 1.00%; Katika misimu mitatu iliyopita wastani kiwango cha upungufu kimeshuka kwa asilimia 0.23%. Kwa kutumia utaratibu uliopo kisheria, kila upungufu uliojitokeza na kuripotiwa kupitia Fomu Namba 7 madai hayo yaliwasilishwa kwa kampuni za bima kwa ajili ya malipo.

Ilifahamishwa kuwa katika msimu wa 2021/2022, jumla ya AMCOS 792 zilishiriki kuuza mazao yao kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Katika msimu wa 2022/2023, idadi ya AMCOS zilizouza kupitia mfumo huo ilikuwa 790, huku msimu wa 2023/2024 idadi hiyo ikiongezeka na kufikia AMCOS 917.

Ilihitimishwa kuwa katika msimu wa 2021/2022, jumla ya kampuni 56 za ununuzi zilijitokeza kununua mazao kupitia minada iliyokuwa ikiratibiwa na ushirika. Msimu wa 2022/2023, idadi ya kampuni za wanunuzi ilipungua hadi kampuni 41, lakini katika msimu wa 2023/2024, idadi hiyo iliongezeka na kufikia kampuni 71.

**Agenda Na 9.5 Taarifa kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)**

Ilifahamishwa kuwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika ina jukumu la kuhamasisha na kusimamia shughuli za Vyama vya Ushirika nchini na katika Vyama vya Korosho Tume ina majukumu yafuatayo: Kutoa waraka wa Usimamizi wa Biashara na masoko ya Korosho kila msimu; Kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania kuandaa Mwongozo wa Mauzo ya Korosho kila Mwaka; Kuratibu na kuhakikisha kuwa Vyama vya ushirika vinakuwa na vifaa na vitendea kazi kama vile vitabu vya Stakabadhi, ghala, Mizani na Vifungashio kipindi cha msimu; Kufanya ufuatiliaji na ukaguzi wa mara kwa mara hususani kipindi cha msimu wa mauzo ya korosho; Kuhakikisha Vyama vya Ushirika vinahakiki mizani za kupimia korosho kabla ya kuanza kwa msimu; Kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania kuratibu mafunzo ya Ubora wa korosho kwa makarani wapimaji; Kuhamasisha na kuratibu upatikanaji na matumizi ya mizani za kidigitali pamoja mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika kielektroniki (MUVU) na; Kutatua migogoro mbalimbali ambayo inaweza kujitokeza kipindi cha mauzo.

Ilelezwa kuwa katika msimu 2023/2024 Tume ya Maendeleo ya Ushirika ilisimamia Vyama vya Ushirika vipatazo 759 katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Pwani, Tanga, Morogoro, Singida, Dodoma, Songwe na Mbeya. Zilielezwa changamoto zilizotokea na namna zilivyotatuliwa.

Ilielezwa mikakati na maandalizi ya msimu 2024/2025 kuwa ni: Kuhamasisha Vyama vya Ushirika kununua na kutumia mizani za kidigitali ambapo hadi sasa tayari mizani ya kidijitali 1,585 imenunuliwa na kusambazwa kati ya mizani 2,200 zinazohitajika kwenye Vyama vya Msingi kupitia Mradi wa Pamoja (KCJE) sawa na 72% ya mahitaji; Kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho kuandaa miongozo ya mauzo na ubora wa korosho kwa msimu 2024/2025; Kutoa waraka wa Usimamizi wa biashara ya Korosho kwa Vyama vya Ushirika; Kusimamia kikamilifu Mauzo na Malipo ya fedha za Korosho kwa wakulima kwa kuhakikisha Maafisa Ushirika na Vyama Vikuu vya Ushirika kwenye vituo vya kuchakata malipo (payment centers); Kuhamasisha Vyama Vikuu vya Ushirika kujenga viwanda vya ubanguaji ambako kwa sasa Chama Kikuu cha TANECU Ltd tayari kinakamilisha kiwanda chake na kinategemea kuanza ubanguaji; Kuendelea kuhamasisha wakulima kukausha korosho na kuzipanga kwenye madaraja stahiki ili kuendelea kulinda ubora wa korosho; Kusimamia uchaguzi wa Viongozi kwenye Vyama vya Ushirika ambako zoezi hili hufanyika kila baada ya miaka mitatu kwa mujibu wa sheria; Kusimamia mikutano Mikuu ya Mwaka kwa ajili ya kupitisha na kuidhinisha bajeti za chama ikiwa ni pamoja na gharama za msimu wa korosho; Kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho na Vyama Vikuu vya Ushirika kuhakikisha upatikanaji na ugawaji wa pembejeo za korosho kwa wakulima; Kuhakikisha kuwa vyama vinakarabati ghala na ujenzi wa ghala; Kusimamia upatikanaji wa vifungashio ambako mpaka sasa Vyama Vikuu Vya Ushirika tayari vina jumla ya gunia 3,600,000 za kuanzia na bado kuna mzabuni mmoja ambaye atasambaza gunia 1,200,000; Kuhakikisha kuwa Vyama vinaingia mikataba na waendesha ghala na; Kuhakikisha vyama vinatangaza zabuni kwa wasafirishaji wa korosho kutoka kwa ghala za AMCOS kwenda ghala kuu.

**Agenda Na. 9.6: Taarifa kutoka Soko La Bidhaa Tanzania (TMX)**

Ilielezwa kuwa katika kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara wa bidhaa mbalimbali nchini, Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania ilianzisha Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) ikiwa ni moja ya suluhisho kwa baadhi ya changamoto zilizokuwepo kwenye minyororo ya thamani ya bidhaa za kilimo, madini, mifugo na nishati. Mifumo mbalimbali ikiwemo Mifumo ya Ushirika na Stakabadhi za Ghala ilianzishwa na kuleta mafanikio makubwa hasa kwenye tasnia ya Kilimo.Pamoja na mafanikio kuonekana kwa kiwango kikubwa bado kuna changamoto zilikuwepo kwenye baadhi ya maeneo zikiwemo bei za mazao kutokuakisi thamani yake halisi

sokoni, ubora haukuwa wa kuridhisha, vipimo visivyo sahihi bado vilikuwa vinatumika, wakulima kutokuwa na uhakika wa malipo yao kwa wakati hali iliyopelekea kuwa kwenye mzunguko wa madeni na kutokukopesheka na Taasisi za kifedha, ugumu wa upatikanaji wa taarifa sahihi za soko na kuwepo kwa takwimu za soko zisizotegemewa.

Ilielezwa kuwa kazi za Soko la Bidhaa zimejikita kwenye yafuatayo: Kuleta uwazi wa bei za bidhaa na mwenendo wa soko; Ugunduzi wa bei kwa ushindani; Hupunguza gharama za kuuza na kununua na; Kutoa kinga ya bei.

Ilifahamu kuwa TMX imeendelea kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB), Bodi za Mazao ya Kilimo pamoja na Mamlaka za Serikali ya Mikoa na Wilaya mbalimbali, kufanya mauzo kupitia mfumo wa kidijitali kwa mazao mbalimbali yakiwemo ufuta, soya, kakao na kahawa.

Kuhusu maandalizi ilielezwa kuwa TMX katika kuelekea mauzo ya korosho msimu wa 2024/2025 inaendelea kushirikiana na wadau mbali mbali wakiwemo Vyama Vikuu vya Ushirika. Baadhi ya hatua zilizochukuliwa na maandalizi mengine ni kama ifuatavyo: Kufanya mafunzo kwa Vyama Vikuu vya Ushirika na wadau wengine kipindi cha msimu wa Ufuta 2024/2025 ili waweze kuelewa mfumo wa mauzo wa kidijitali na ; Kushiriki katika maandalizi ya Muongozo wa Mauzo wa Korosho Msimu wa 2024/2025;

## AGENDA NA 10.0 TAARIFA YA MAENDELEO YA UTAFITI WA ZAO LA KOROSHO NCHINI

Ilielezwa kuwa korosho ni miongoni mwa mazao makuu yanayochangia pato la wakulima wa mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani, Tanga na Ruvuma. Katika kuongeza uzalishaji wa korosho nchini korosho.  Majukumu ya TARI Naliendele ni kufanya utafiti na kuzalisha mbegu na miche bora ya korosho. Aidha, programmu ya Utafiti wa Zao la Korosho ina majukumu yafuatayo: Kugundua, kuzalisha na kusambaza mbegu bora za korosho; Kubaini na kupendekeza njia bora za uzalishaji wa miche; Kubaini magonjwa na wadudu waharibifu wa korosho na mbinu za kudhibiti; Kubaini wadudu rafiki wa zao la korosho na namna ya kuwatumia; Kubaini mbinu za kuboresha na kufufua mashamba ya korosho; Kubaini na kutumia mbinu za baioteknolojia katika kuzalisha mbegu bora za korosho; Kutoa elimu katika upandaji

na utunzaji mashamba ya korosho; Kufanya utafiti wa udongo na matumizi bora ya ardhi kwenye zao la korosho; Kufanya utafiti na kuainisha maeneo yanayofaa kwa kilimo cha korosho; Kusambaza teknolojia za korosho kwa wadau; Kutoa mafunzo ya kilimo cha korosho kwa wagani na wadau wengine na; Kutafiti mbinu za uongezaji thamani korosho na mabibo

Ilielezwa kuwa kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, kumekuwa na milipuko ya magonjwa na wadudu waharibifu ndani ya msimu wa uzalishaji wa korosho katika maeneo mbalimbali. Magonjwa kama vile blaiti, ubwiriunga, vithiripi na chule vimeendelea kuwa tatizo kwenye zao la korosho hasa usipodhibitiwa.

Ilihitimishwa kuwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania Kituo cha Naliendele, kinaendelea na shughuli mbalimbali za utafiti wa zao la korosho ili kuongeza tija ya uzalishaji.

**AGENDA NA 11.0 TAARIFA YA TUME MAALUM YA TATHMINI YA TASNIA YA KOROSHO**

Tume Maalum ya Tathmini ya Tasnia ya Korosho iliwasilisha mapendekezo taarifa yake ikiwa na vipengele 16 kama vile: Maandalizi ya shamba; Upatikanaji wa mbegu bora na miche ya korosho; Usajili wa wakulima, Upatikanaji na usambazaji wa viuatilifu; Upatikanaji wa mitaji kwa wakulima; Upatikanaji wa huduma za ugani; Upatikanaji wa ghala; Taratibu za uendeshaji wa ghala; Upimaji na usafirishaji wa korosho za wakulima; Mifumo ya masoko na malipo kwa wakulima; Tozo kwenye zao la korosho; Uongezaji wa thamani wa korosho; Ushiriki wa wadau wengine kwenye Tasnia ya Korosho; Kuhusu kugawa Chama Kikuu cha TANECU; Mfumo wa uendeshaji Vyama vya Ushirika; Mfumo wa uendeshaji wa minada na; Masuala mengine ya uendelezaji wa tasnia ya korosho;

**AGENDA NA 12.0 UTOAJI WA TUZO KWA WADAU MBALIMBALI**

Tuzo mbalimbali kwa washiriki wenye mchango mahususi katika Tasnia ya Korosho kwa mwaka 2023/2024 ulikuwa kwa makundi kama ifuatavyo:

**Sekretarieti za mikoa ya asili katika kilimo cha korosho:** Mshindi alikuwa ni Mkoa wa Mtwara kwa usimamizi imara wa zao la korosho katika kundi la Sekretarieti za Mikoa inayolima korosho nchini.

**Halmashauri za Wilaya katika mikoa ya asili ya zao la korosho:** Mshindi ilikuwa ni Halmashauri ya Wilaya ya Liwale kwa usimamizi imara wa zao la korosho katika kundi la Halmashauri.

**Kundi la Vyama Vikuu vya Ushirika:** Mshindi ni Chama Kikuu Cha Ushirika cha RUNALI Ltd kwa usimamizi mzuri kwenye Vyama vya Ushirika vya Msingi.

**Kundi la Wabanguaji Wakubwa:** Mshindi alikuwa ni AMAMA FARMS LTD cha Mkoani Mtwara.

**Kundi la Wabanguaji Wadogo:** Mshindi alikuwa ni TANZANIA DELICIOUS CASHEW kutoka Tandahimba cha Mkoani Mtwara

**Kundi la Wasambazaji wa Pembejeo:** Mshindi alikuwa ni Mohammed Enterprises Co. Ltd.

**Kundi la Wasafirishaji bora kwenye Tasnia ya Korosho:** Mshindi ni Elias Transport Co. Ltd

**Kundi la Wanunuzi wa Korosho Ghafi:** Mshindi alikuwa ni Iscon Commodities Tanzania Ltd

**Kundi la Wanahabari wa Televisheni:** Mshindi alikuwa ni John M. Kasembe kutoka Azam Tevevision - Mtwara

**Kundi la Redio za Kijamii:** Mshindi alikuwa ni Ruangwa FM Radio

**Kundi la Wanahabari wa Magazeti:** Mshindi alikuwa ni Sijawa Omary Abdallah kutoka Habari Leo

**Kundi la Wanahabari wa Televisheni Mtandao:** Mshindi alikuwa ni Faida wa Online TV

**Kundi la Maafisa Kilimo (DSMS)** walipata tuzo ya usimamizi bora wa huduma za ugani kwa wakulima wa zao la korosho ni:

i. Rajab A. Namkoko kutoka Mtama DC
ii. Hussein Mwapili kutoka Lindi MC
iii. Juma Hashim Kahamba kutoka Newala TC
iv. Cuthbet Mwinuka kutoka Chunya DC

**Kundi la Wakulima:** Washindi ni

i. Ndg. Fikirini Mohamed Makarani – mkulima bora wa kwanza Kitaifa - Nanyumbu DC
ii. Ndg. Sijahi Swalehe Hassan – Mkulima bora wa pili Kitaifa – Newala TC
iii. Ndg. Seleman Abdallah Mndengeluka – Mkulima bora wa tatu Kitaifa – Mtama DC

**Kundi la watu wenye Mchango Maalum katika Tasnia ya Korosho**

Waliopewa Tuzo ya mchango Maalum walikuwa ni:

i. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuzo maalum kwa uwekezaji mkubwa alioufanya kwenye Tasnia ya Korosho ikiwemo kutoa pembejeo bure kwa wakulima kwa muda wa miaka 3 mfululizo.
ii. Ndg. Audax Rukonge Mkurugenzi Mtendaji Mstaafu wa ANSAF kuanzia mwaka 2013 hadi mwaka 2022, tuzo maalum kwa uhamasishaji wa ubanguaji wa korosho kupitia vikundi vidogo vya ubanguaji nchini.
iii. Mheshimiwa Dkt. Rehema Nchimbi Mkuu wa Mkoa Mstaafu kwa uanzishwaji wa mashamba ya pamoja *(Block farming)* ya korosho yaliyopo Manyoni Mkoa wa Singida.

**AGENDA NA 13.0 MENGINEYO**

Hakukuwa na mengineyo

**AGENDA NA 14.0 KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao ya mawazo kwa uwazi na kuwataka watendaji kuzingatia maelekezo yaliyotolewa. Aidha, alifunga kikao saa 06:45 mchana siku ya pili.

| | |
|---|---|
| ………………………………………. | …………………………………… |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |
| **TAREHE**…………………… | **TAREHE**………………… |

**AGENDA NA 4.0: YATOKANAYO NA MKUTANO MKUU WA WADAU WA TASNIA YA KOROSHO ULIOFANYIKA TAREHE 22 - 23 AGOSTI 2024 KATIKA UKUMBI WA PSSSF, JIJINI DODOMA**

**YATOKANAYO NA MKUTANO MKUU WA WADAU WA TASNIA YA KOROSHO ULIOFANYIKA TAREHE 22 - 23 AGOSTI 2024 KATIKA UKUMBI WA PSSSF, JIJINI DODOMA**

| AGENDA NAMBA | AGENDA | AZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| 1.0 | Kufungua mkutano | Wabanguaji wa ndani wawasilishe mahitaji ya korosho wanazohitaji kubangua kwa mwaka mzima Bodi ya Korosho ili waweze kuwekewa utaratibu wa kununua korosho hizo. | CBT<br>TACP | Kwa msimu wa mwaka 2024/2025 wabanguaji wa ndani walinunua korosho kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi baada ya wakulima wenye korosho hizo kuridhiwa ziuzwe kupitia soko la awali. |
| | | Mfumo wa Soko la Bidhaa utumike kwenye mauzo ya korosho kuanzia msimu wa 2024/2025 baada ya mfumo huo kuleta mafanikio makubwa kwenye mazao mengine | CBT, TMX, WRRB | Azimio limetekelezwa ambapo korosho zote zilizoingia katika mfumo wa stakabadhi za ghala ziliuzwa kupitia mfumo wa Soko la Bidhaa Tanzania (TMX). |
| | | Uwekwe utaratibu wa kuwawezesha Wakuu wa Mikoa na Wilaya ili waweze kusimamia zao la korosho ikiwemo usambazaji na ugawaji wa | CBT, UNION | Katika msimu wa 2024/2025 Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na Vyama Vikuu vya Ushirika ilitenga kiasi cha shilingi 2.00 kutoka katika tozo ya shilingi 110.00 kwa kilo ya |

| AGENDA NAMBA | AGENDA | AZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | | pembejeo. | | uendelezaji wa tasnia ya korosho inayolipwa na mnunuzi kwa ajili ya kuwawezesha Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kusimamia zao la korosho ikiwemo usambazaji na ugawaji wa pembejeo kwa wakulima. |
| | | Taarifa za utendaji kazi wa Bodi ya Korosho zitolewe kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya walioko kwenye Tasnia ya Korosho | CBT | Bodi ya Korosho Tanzania imetoa taarifa za utendaji kazi wake katika Mikoa na Wilaya husika. |
| 5.0 | Taarifa ya maendeleo ya zao la korosho kwa mwaka 2023/2024 na mpango wa mwaka 2024/2025 kwa Mikoa inayozalisha korosho | Serikali iweke mpango mahususi wa kuendeleza zao la korosho kwenye Mikoa Mipya | MOA, CBT | Bodi ya Korosho Tanzania imeandaa mpango mkakati wa kuendeleza zao la korosho katika mikoa mipya ambao utaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2025/2026. |
| 6.0 | Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za uendelezaji | Kuwe na mikakati ya kuanzisha mashamba na kufufua mashamba | CBT, TARi, RS, | Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na TARI Naliendele na |

| AGENDA NAMBA | AGENDA | AZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | zao la korosho msimu wa 2023/2024 na mpango wa kuelekea msimu wa mwaka 2024/2025 kutoka Bodi ya Korosho Tanzania | pori | LGA | Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri inaendelea na kampeni ya kuelimisha wakulima kuzingatia kanuni za kilimo bora cha korosho ikiwa ni pamoja na kufufua mashamba pori na kuhamasisha uanzishwaji wa mashamba makubwa ya pamoja *(Block farming)* ambapo Manyoni kuna ekari **27,000** Manispaa ya Lindi ekari 52,000 na Rufiji ekari 6,500. |
| 7.0 | Mwenendo wa masoko ya korosho kwa msimu wa mwaka 2023/2024 na maandalizi ya mwaka 2024/2025 | Taarifa ya bei ya korosho duniani itolewe kwa wadau mara kwa mara | CBT, TCDC, TMX | Taarifa ya bei inaendelea kutolewa kwa wadau ambapo kila mwisho wa mwezi hutolewa jarida linalionesha bei za korosho duniani. Ambapo jarida hili hupatikana katika tovuti ya Bodi ya Korosho. |

| AGENDA NAMBA | AGENDA | AZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| 8.0 | Mapendekezo ya Tozo. | Tozo ya shilingi 7 kwa kilo moja isimamiwe na taasisi mbili | CBT, WRRB | Utekelezaji umefanyika tozo iliendelea kusimamiwa na taasisi mbili ambazo ni Bodi ya Korosho Tanzania na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala Tanzania. |
| | | Tozo ya zao ilipwe kwenye Halmashauri zao lilipozalishwa na service levy ilipwe kwenye Halmshauri ilipofanyika biashara ya zao | LGA<br>Wanunuzi | Azimio limetekelezwa ambapo tozo na *Service levy* zinalipwa kwenye Halmashauri husika. |
| | | Vyama Vikuu viwajibike kusimamia ubora wa korosho ghafi kuanzia ngazi ya mkulima hadi ghala kuu | TCDC, UNION, CBT, WRRB | Utekelezaji umefanyika ambapo Vyama Vikuu vimesimamia ubora wa korosho. |
| 9.1 | Taarifa kutoka Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) | Chama Kikuu kishiriki kwenye mchakato wa kusajili mwendesha ghala kwenye eneo lake | Union | Utekelezaji umefanyika ambapo Vyama Vikuu vilishiriki katika mchakato wa kumpata mwendesha ghala |

| AGENDA NAMBA | AGENDA | AZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| 11 | Taarifa ya Tume Maalum ya Tathmini ya Tasnia ya Korosho ya Mwaka 2024 | Mapendekezo yaliyowasilishwa na Tume yatekelezwe na taarifa itolewe kwenye Mkutano Mkuu ujao. | CBT, Wadau husika | Taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Tume Maalum ya Tathmini ya Tasnia ya Korosho Nchini mwaka 2024 itawasilishwa katika Mkutano huu. |

**AGENDA NA 5.0:KUPOKEA NA KUPITIA TAARIFA YA MAENDELEO YA ZAO LA KOROSHO KWA MWAKA 2024/2025 NA MPANGO WA MWAKA 2025/2026 KWA MIKOA INAYOZALISHA KOROSHO**

## KUPOKEA NA KUPITIA TAARIFA YA MAENDELEO YA ZAO LA KOROSHO KWA MWAKA 2024/2025 NA MPANGO WA MWAKA 2025/2026 KWA MIKOA INAYOZALISHA KOROSHO

### 5.1. TAARIFA YA MKOA WA MTWARA

#### 5.1.1. Utangulizi

Korosho ni zao kuu la biashara linalotegemewa sio tu na wananchi wa Mkoa wa Mtwara bali na nchi katika uchangiaji wa pato la Taifa. Mchango huo unalifanya zao la korosho kuwa muhimu sana katika ukuaji wa uchumi wa wananchi wa Mtwara na chanzo kikuu cha mapato ya Halmashauri. Zao hili ni mojawapo ya mazao ya kimkakati yanayopewa kipaumbele Mkoani Mtwara.

Mkoa wa Mtwara una wakulima 335,543 waliohuisha taarifa kwenye kanzidata ya Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) katika msimu 2024/25. Mkoa una jumla ya Hekta 934,732.29 sawa na Ekari 2,336,830.73 zenye jumla ya mikorosho 70,104,922 (***Chanzo: CBT***) . Takwimu hizi ndizo zinazotumika kugawa pembejeo za ruzuku za korosho kwa wakulima wenye sifa.

#### 5.1.2. Uzalishaji wa korosho ghafi msimu wa 2024/25 na mpango wa uzalishaji ifikapo 2029/30

Mkoa wa Mtwara unaongoza katika uzalishaji wa korosho nchini, Katika Msimu wa 2024/25 Mkoa ulizalisha Tani 330,505 za korosho ghafi sawa na asilimia 62.6 ya uzalishaji wa korosho kitaifa. Aidha, Mkoa na wadau wake umeweka mikakati ya kuendelea kuongeza uzalishaji wa korosho ghafi ili kuchangia malengo ya kitaifa ya kuzalisha Tani 1,000,000 ifikapo 2029/30.

#### 5.1.3. Uzalishaji Wa Korosho Ghafi Msimu Wa 2024/25

Msimu 2024/25 Mkoa uliweka lengo la kuzalisha Tani 345,651 ambapo katika utekelezaji umezalisha Tani 330,505.051 sawa na asilimia 95.6 ya malengo tuliyowekewa. Uzalishaji wa msimu 2024/25 ni ongezeko la asilimia 83 ukilinganisha na tani 180,544 za korosho ghafi zilizolishwa msimu 2023/24.

**Uzalishaji wa Korosho kuanzia Mwaka 2022/23 hadi 2024/25**

| Mwaka | Malengo ya Uzalishaji (Tani) | Utekelezaji wa Uzalishaji (Tani) | % ya Utekelezaji wa Malengo |
|---|---|---|---|
| 2022/23 | 162,400 | 99,013 | 61.0 |
| 2023/24 | 248,400 | 180,544 | 72.7 |
| 2024/25 | 345,651 | 330,505 | 95.6 |

Kiasi cha korosho ghafi Tani 330,505 zilizozalishwa msimu 2024/25 zimegawanyika katika mafungu yafuatayo:

i. Korosho zilizouzwa kwa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na minada ya kidijitali kupitia Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) - Tani 240,818.8 zenye thamani ya shilingi 873,500,216,083.76

ii. Korosho zilizobanguliwa kupitia wajasiriamali na wakulima wadogo na nyingine kuuzwa katika soko la awali sawa na Tani 39,812.8, na

iii. Korosho zilizobaki kwa wakulima kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo kubangua na kuendelea kuuza kwenye Soko la Awali sawa na Tani 49,873.4

### 5.1.4. Mpango/Makadirio ya Uzalishaji wa Korosho Kiwilaya 2025/26 Hadi 2029/30

Mkoa umeweka mkakati wa kuongeza uzalishaji wa korosho kufikia Tani 580,927 ifikapo 2029/30. Katika kufikia malengo hayo, Mkoa umeanzisha Operesheni ya Ondoa Mapori Ongeza Uzalishaji wa Korosho ambayo imekusudia kuongeza kasi ya kupanda mikorosho mipya, Kuondoa mikorosho iliyozeeka na kupanda mipya au kubebesha mikorosho mizee (Top working) na kuimarisha huduma za ugani. Malengo ya uzalishaji kwa miaka mitano ijayo kufikia mwaka 2029/30 ni kama inavyoonesha kwenye jedwali hapo chini.

**Malengo ya Uzalishaji wa Korosho Mkoa wa Mtwara 2025/26 -2029/30**

| Halmashauri | 2025/26 | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 |
|---|---|---|---|---|---|
| Mtwara (M) | 3,549 | 3,929 | 4,310 | 4,690 | 5,070 |
| Mtwara (V) | 16,579 | 18,355 | 20,132 | 21,908 | 23,684 |
| Nanyamba | 42,090 | 46,599 | 51,109 | 55,618 | 60,128 |
| Tandahimba | 153,031 | 169,427 | 185,823 | 202,220 | 218,616 |
| Newala (V) | 48,443 | 53,634 | 58,824 | 64,014 | 69,205 |
| Newala (M) | 27,630 | 30,590 | 33,550 | 36,511 | 39,471 |
| Masasi (V) | 64,114 | 70,983 | 77,852 | 84,722 | 91,591 |
| Masasi (M) | 12,793 | 14,164 | 15,535 | 16,905 | 18,276 |
| Nanyumbu | 38,420 | 42,536 | 46,653 | 50,769 | 54,885 |
| **Jumla** | **406,649** | **450,218** | **493,788** | **537,357** | **580,927** |

Baadhi ya mikakati iliyotekelezwa iliyochangia kuongezeka kwa uzalishaji ni kama inavyoonesha kwenye Jedwali hapo chini.

**Utekelezaji wa Mikakati ya Kuongeza Uzalishaji**

| Na. | Mkakati | Utekelezaji hadi msimu 2024/25 |
|---|---|---|
| 1. | Kuongeza tija na uzalishaji kutoka Tani 118,575 mwaka 2020/21 hadi Tani 420,000 ifikapo 2025/26 | Uzalishaji umeongezeka Kutoka Tani 118,575 mwaka 2020/21hadi Tani 330,55 mwaka 2024/25 |
| 2. | ii. Kuweka mfumo endelevu na shirikishi wa upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima | Wakulima wamesajiliwa na pembejeo zinasambazwa kidijitali kupitia vyama ushirika |
| 3. | Kutoa mafunzo rejea kwa maafisa ugani na wakulima kuhusu mabadilliko ya teknolojia za uzalishaji wa mikorosho, ubebeshaji, matumizi ya pembejeo na udhibiti wa magonjwa; | Kila mwaka mafunzo rejea yanatolewa kwa maafisa ugani kwa ushrikiano wa CBT na TARI Naliendele. |
| 4. | Halmashauri kuratibu uzalishaji/upatikanaji wa miche bora ya mikorosho na kupanda mikorosho mipya. | Msimu 2024/25 Halmashauri imesambaza miche 1,394,000 kutoka Bodi ya Korosho Tanzania |
| 5. | Vyama Vikuu vya Ushirika (MAMCU na TANECU) kuanzisha mashamba ya korosho | Chama Kikuu Cha Ushirika MAMCU kimeanzisha shamba la korosho Mikorosho lenye ekari 500 |
| 6. | Vyama Vikuu wa Ushirika (MAMCU na TANECU) kuanzisha viwanda 2 vya ubanguaji wa korosho | Chama Kikuu cha TANECU Kimezindua kiwanda Kitangari chenye uwezo wakubangua Tani 3,600 kwa mwaka na wantarajia kujenga kingine eneo la Malopokelo Tandahimba |
| 7. | Kuongeza idadi ya maghala bora ya kuhifadhi mazao kutoka 2 hadi 4 | Jumla ya maghala Makuu 4 yamejengwa na Halmashauri ya Wilaya Masasi, Chama kikuu cha MAMCU na Bodi ya Korosho. |

### 5.1.5. Mpango wa Upatikanaji Mbegu na Miche Bora ya Mikorosho

Msimu 2024/25 wakulima walisambaziwa jumla ya miche 1,430,552 kati ya hiyo miche 1,389,000 ilitolewa na Bodi ya Korosho Tanzania kutia Kituo cha Utafiti cha TARI Naliendele. Aidha, Halmashauri za wilaya, Kiwanda cha Korosho AMAMA - Tandahimba, Msombe Group - Nanymba na watu binafsi walichangia miche 41,522 kama inavyoonesha kwenye jedwali.

Kabla ya ugawaji wa Miche Mkoa uliandaa siku ya uzinduzi wa msimu wa kilimo pamoja na mambo mengine kulifanyika uhamasishaji wa kupanda mikorosho mipya na kuzindua upandaji wa Miche ya mikorosho Kimkoa siku ya 30 Disemba 2024 wilayani Masasi.

Mkoa kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho, Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na TARI Naliendele umelenga kuwawezesha wakulima kupanda walau mikorosho mipya 2,000,000 kila mwaka. Uzalishaji wa miche unafanywa na TARI Naliendele pamoja na vikundi vya watu binafsi vilivyotambuliwa.

**Miche ya Korosho iliyosambazwa msimu 2024/25**

| Na | Halmashauri | Idadi ya Miche ya Mikorosho iliyosambazwa msimu 2024/25 | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Bodi ya Korosho | Halmashauri/ watu binafsi | Jumla |
| 1 | Masasi DC | 450,000 | 0 | 450,000 |
| 2 | Masasi TC | 150,000 | 0 | 150,000 |
| 3 | Mtwara DC | 20,000 | 400 | 20,400 |
| 4 | Mtwara MC | 25,000 | 0 | 25,000 |
| 5 | Nanyamba TC | 300,000 | 1,572 | 301,572 |
| 6 | Nanyumbu DC | 50,000 | 1,080 | 51,080 |
| 7 | Newala DC | 14,000 | 0 | 14,000 |
| 8 | Newala TC | 30,000 | 20,000 | 50,000 |
| 9 | Tandahimba DC | 350,000 | 18,500 | 368,500 |
| | **Jumla** | **1,389,000** | **41,552** | **1,430,552** |

### 5.1.6. Ubanguaji wa korosho msimu 2025/26

Mkoa wa Mtwara una Jumla ya viwanda 27 vinavyofanya kazi vyenye uwezo wa kubangua Tani 44,361 kwa mwaka kama vitafanya kazi kulingana na uwezo wake. Aidha, vipo vikundi na wakulima binafsi wanajihusisha na Shughuli za ubanguaji wa korosho. Mkoa wa Mtwara unabangua asilimia 25 ya korosho zinazozalishwa.

Kumekuwa na uhamasishaji na mwamko mkubwa wa ubanguaji wa korosho kwa siku za karibuni. Mwaka 2025, kiwanda kipya cha TANECU kilifunguliwa chenye uwezo wa kubangua Tani 3600 kwa mwaka. Aidha, mpango wa ujenzi wa viwanda vingine upo mbioni ikiwemo kwenye Kongani ya viwanda Maranje, Kiwanda cha TANECU Tandahimba, Masasi mjini na Kiwanda cha Kitama ambacho ujenzi wake umeanza.

### 5.1.7. Hali ya huduma za ugani na mafunzo 2025

Msimu 2025 mafunzo yalitolewa kwa maafisa ugani wa halmashauri na waliajiriwa na Bodi ya Korrorosho kwa awamu ya mbili. Awamu ya kwanza mwezi Februari 2025, walifundishwa utunzaji wa mashamba ya korosho na awamu ya pili mwezi Mei 2025 walifundishwa matumizi sahihi na salama ya viuatilifu. Jumla ya Maafisa Ugani 541 wakiwemo Maafisa ugani 299 wa Halmashauri na 242 walioajiriwa na Bodi ya Korosho (CBT) walipata mafunzo hayo rejea. Mafunzo yalitolewa kwa ushirikiano wa wataalamu kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, CBT na na TARI Naliendele.

Maafisa ugani waliopatiwa mafunzo waliwafikia jumla ya wakulima na wapuliziaji 145,484 ambao walikuwa wanahudhuria kwenye mikutano ya mafunzo wakiwemo wakulima wa mikorosho 141,730 na wapuliziaji 3,748.

**Wakulima na Wapuliziaji wa Mikorosho waliopatiwa Mafunzo Msimu 2025**

| NA | HALMASHAURI | WAKULIMA | | | WAPULIZIAJI | | | Jumla ya waliofundishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | ME | KE | JUMLA | ME | KE | JUMLA | ME | KE | JUMLA |
| 1 | Tandahimba DC | 15,060 | 7,718 | 22,778 | 948 | 2 | 950 | 16,008 | 7,720 | 23,728 |
| 2 | Newala DC | 5,381 | 2,644 | 8,025 | 423 | - | 423 | 5,804 | 2,644 | 8,448 |
| 3 | Newala TC | 1,663 | 1,211 | 2,874 | 169 | 3 | 172 | 1,832 | 1,214 | 3,046 |
| 4 | Masasi DC | 11,225 | 5,533 | 16,758 | 612 | - | 612 | 11,837 | 5,533 | 17,370 |
| 5 | Masasi Tc | 9,145 | 3,425 | 12,570 | 12 | 1 | 13 | 9,157 | 3,426 | 12,583 |
| 6 | Nanyumbu DC | 14,355 | 6,164 | 20,519 | 772 | - | 772 | 15,127 | 6,164 | 21,291 |
| 7 | Nanyamba TC | 21,531 | 7,177 | 28,708 | 480 | - | 480 | 22,011 | 7,177 | 29,188 |
| 8 | Mtwara DC | 16,592 | 8,652 | 25,244 | 206 | - | 206 | 16,798 | 8,652 | 25,450 |
| 9 | Mtwara MC | 2,609 | 1,645 | 4,254 | 126 | - | 126 | 2,735 | 1,645 | 4,380 |
| | **Jumla** | **97,561** | **44,169** | **141,730** | **3,748** | **6** | **3,754** | **101,309** | **44,175** | **145,484** |

#### 5.1.8. Usambazaji pembejeo za zao la korosho msimu wa mwaka 2025/26 hadi 03 agosti, 2025

Baadhi ya visumbufu vya mikorosho mkoani Mtwara ni pamoja na ubwiriunga, blaiti, vidung'ata na mbu wa mikorosho. Msimu 2025/26 Serikali kupitia Bodi ya Korosho Tanzania na Vyama vya ushirika vimesambaza kwa wakulima jumla ya Tani 20,563.03 ya Salfa, Viuatilifu vya kudhibiti wadudu Lita 338,104 na viuatilifu vya maji vyakudhibiti magojwa Lita 464,009 ambavyo vimesambazwa kwa wakulima kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi - AMCOS kwa mfumo wa kidijitali. Zoezi la kusambaza pembejeo linaendelea na linatarajiwa kukamilika tarehe 30 Agosti, 2025.

#### 5.1.9. Changamoto

i. Magojwa na wadudu wa Mikorosho
ii. Mabadiliko ya Tabianchi
iii. Uelewa mdogo wa baadhi ya wakulima kuhusu matumizi ya sahihi na salama ya viuatilifu
iv. Baadhi ya wakulima wachache kuchelewa kulipwa fedha za mauzo kutokana na baadhi ya viongozi wa AMCOS kukosa uadilifu

### 5.1.10. Hatua za utatuzi wa changamoto

i. Kumekuwa na programu maalum ya kutoa mafunzo rejea kwa wakulima na maafisa ugani ya Teknolojia za zao la korosho.
ii. Uongozi wa Mkoa kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho uliunda kikosi kazi cha kufuatilia changamoto za tasnia ya korosho na kusaidia kupunguza changamoto zilizojitokeza
iii. Mrajis na Uongozi wa Vyama vikuu ulichukua hatua kwa kuwasimamisha viongozi wa AMCOS waliokiuka taratibu.
iv. Viongozi waliokiuka taratibu walifikishwa kwenye vyombo vya sheriakwa hatua zaidi.

### 5.1.11. Mikakati ya kuendeleza zao la korosho ifikapo 2029/30

Mkoa unaendelea kusimamia Tasnia ya Korosho kwa ushirikiano na wadau wengine ili kuhakikisha kuwa zao la korosho linaendelea kukua. Ili kutimiza malengo hayo Mkoa na wadau wake umejipanga kutekeleza mikakati ifuatayo:

i. Kuhamasisha matumizi ya teknolojia bora ili kuongeza uzalishaji wa korosho ili kufikia Tani 580,927 ifikapo 2029/30
ii. Kusimamia ubora wa korosho zinazozalishwa ili zikidhi mahitaji ya soko,
iii. Kusimamia mfumo wa masoko kuhakikisha wakulima wanapata malipo kwa wakati na yanayostahiki,
iv. Kuongeza thamani zao la korosho kwa kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kubangua na kusindika mazao ya korosho ili korosho zote zibanguliwe ndani ya Mkoa ifikapo 2030.
v. Kuhamasisha wakulima kupima mashamba na kujisajili kwenye kanzidata ya wakulima kwa ushirikiano na Bodi ya Korosho Tanzania.

### 5.1.12. Hitimisho

Kuongeza uzalishaji na kubangua korosho zote ndani ya Mkoa wa Mtwara kunawezekana kama wadau watafanya kazi kwa ushirikiano. Kila mdau akitimiza wajibu na majukumu yake kikamilifu Tasnia ya Korosho itakuwa na mchango mkubwa kiuchumi kwa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

## 5.2. TAARIFA YA MKOA WA RUVUMA

### 5.2.1. Utangulizi

Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa Mikoa inayozalisha zao la korosho kwa kiasi kikubwa hapa nchini Tanzania. Mkoa una Wilaya tano (5) za Kiserikali ambazo ni Tunduru, Namtumbo, Mbinga, Songea na Nyasa. Katika Wilaya hizo tano kuna jumla ya Halmashauri nane (8) ambazo ni Tunduru, Namtumbo, Songea Vijijini, Manispaa ya Songea, Madaba, Mbinga Vijijini, Mbinga Mji, na Nyasa. Halmashauri za Wilaya saba (7) ndizo zinazolima zao la korosho kwa viwango na hatua tofauti katika kuanzisha mashamba na uzalishaji isipokuwa Halmashauri moja (1) ndiyo isiyolima zao hili kabisa ambayo ni Manispaa ya Songea.

Uzalishaji wa zao la korosho msimu 2024/2025 na mpango wa uzalishaji ifikapo msimu wa 2029/2030

### 5.2.2. Uzalishaji msimu wa 2024/2025

Katika **msimu 2024/2025** Mkoa wa Ruvuma umezalisha jumla ya kilo **31,446,996** za korosho ikilinganishwa na msimu wa **2023/2024** uzalishaji ulikuwa kilo **25,330,849** sawa na ongezeko la asilimia **25**. Kupanda kwa uzalishaji kumesababishwa na uhakika wa upatikanaji wa pembejeo za kudhibiti visumbufu vya korosho pamoja na usimamizi mzuri wakati wa kukusanya korosho. *Jedwali namba 1* linaonesha hali ya uzalishaj wa zao la korosho kwa miaka mitano (5) na *kiambatanisho namba 1(a) na 1(b)* hapo chini vinaonesha hali ya mwenendo wa uzalishaji wa zao la korosho kutoka 2020/2021 hadi 2024/2025;

**Uzalishaji wa korosho kuanzia Msimu 2017/2018 hadi 2021/2022**

| Na | Halmashauri | 2020/2021 | 2021/2022 | 2022/2023 | 2023/2024 | 2024/2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Tunduru | 14,814,755 | 24,617,262 | 14,845,562 | 25,319,082 | 30,379,488 |
| 2 | Namtumbo | 472,148 | 532,631 | 0 | 0 | 954,000 |
| 3 | Mbinga DC | 27,572 | 33,876 | 26,176 | 11,767 | 23,008 |
| 4 | Nyasa | 19,645 | 33,604 | 0 | 0 | 90,500 |
| 5 | Madaba | 6,963 | 14,377 | 0 | 0 | 0 |
| 6 | Songea Vijijini | 0 | 10,774 | 0 | 0 | 0 |
| | **JUMLA** | **15,410,605** | **25,242,524** | **14,845,562** | **25,330,849** | **31,446,996** |

### 5.2.3. Mpango/makadirio ya uzalishaji kiwilaya misimu ya 2025/2026, 2026/2027, 2027/2028, 2028/2029 na 2029/2030

Mkoa wa Ruvuma umejiwekea malengo ya Kuzalisha zao la korosho kiasi cha kilo **34,418,000** kwa msimu **2025/2026** na matarajio ya kuongeza uzalishaji hadi kilo **46,786,792** kufikia mwaka 2029/2030 ili kufanikisha lengo la Taifa la kuzalisha tani 1,000,000. Mchanganuo wa uzalishaji umeainishwa katika jedwali hapo chini.

**Mpango wa uzalishaji korosho hadi kufikia 2029/2030**

| Halmashauri | 2025/2026 | 2026/2027 | 2027/2028 | 2028/2029 | 2029/2030 |
|---|---|---|---|---|---|
| Tunduru | 33,417,000 | 36,454,948 | 39,492,896 | 42,530,844 | 45,568,792 |
| Namtumbo | 1,001,000 | 1,052,000 | 1,104,000 | 1,160,000 | 1,218,000 |
| Madaba DC | | | | | |
| Songea DC | | | | | |
| Nyasa | | | | | |
| Mbinga DC | | | | | |
| Mbinga TC | | | | | |
| **JUMLA** | **34,418,000** | **37,506,948** | **40,596,896** | **43,690,844** | **46,786,792** |

### 5.2.4. Mpango wa upatikanaji wa mbegu na miche bora ya korosho

Kwa msimu 2024/2025, Mkoa wa Ruvuma umepokea miche bora **22,000** (Tunduru miche **20,000** na Songea DC miche **2,000** ambayo imesambazwa kwa wakulima**.** Kwa kipindi cha misimu kumi(10) kuanzia Msimu 2015/2016 hadi 2024/2025 Mkoa umesambaza miche 1,391,253 kwa wakulima sawa na jedwali hapo chini.

**Idadi ya Miche Bora ya Korosho iliyosambazwa kuanzia Msimu 2015/2016 hadi 2024/2025**

| Msimu | Idadi ya Miche iliyosambazwa kuanzia Msimu 2015/16 hadi 2024/2025 |
|---|---|
| 2015/2016 | 48,800 |
| 2016/2017 | 295,000 |
| 2017/2018 | 602,007 |
| 2018/2019 | 18,717 |
| 2019/2020 | 39,300 |
| 2020/2021 | 13,000 |
| 2021/2022 | 31,429 |
| 2022/2023 | 48,000 |
| 2023/2024 | 7,5000 |
| 2024/2025 | 22,0000 |
| **JUMLA** | **1,391,253** |

### 5.2.5. Ubanguaji wa msimu wa 2024/2025 na mpango ifikapo msimu wa 2029/2030

**Ubanguaji msimu wa 2024/2025**

Mkoa wa Ruvuma umebangua **kilo 2,917** za korosho kwa mwaka kupitia vikundi vya wabanguaji kwenye Halmashauri. Mpango/makadirio ya ubanguaji kiwilaya misimu ya 2025/2026, 2026/2027, 2027/2028, 2028/2029 na 2029/2030.

Mkoa wa Ruvuma unatarajia kubagua kiasi cha tani **2,000** za korosho mwaka 2025/2026 na kuongeza ubanguaji zaidi ya **2,917** ifikapo mwaka 2029/2030 kama jedwali namba 4 linavojieleza. Mkoa unaendelea kuhamasisha wadau katika kuimarisha zoezi la uongezaji thamani kwa zao la korosho.

**Malengo ya ubanguajiji korosho hadi kufikia 2025/2026**

| HALMASHAURI | 2025/2026 | 2026/2027 | 2027/2028 | 2028/2029 | 2029/2029 |
|---|---|---|---|---|---|
| Namtumbo | 2,400 | 2,520 | 2,646 | 2,778 | 2,917 |

### 5.2.6. Huduma za ugani na mafunzo ya Wataalam wa zao

Mkoa una waratibu wa zao la korosho (7) `*District Subject Matter Specialist (DSMS*)` wanaoshirikiana na wataalam wengine wa kilimo waliopo katika kata zote za mkoa na baadhi ya vijiji kwa lengo la kutoa elimu ya kilimo bora cha korosho.

### 5.2.7. Ajira za mkataba

Ajira za mkataba kwa vijana wanaokuza ujuzi kwenye zao la korosho kupitia mpango wa serikali wa Jenga Kesho Iliyo bora (Building Better Tomorrow – **BBT).** Halmashauri ya Tunduru ilipata vijana Hamsini (50) wataalam wa kilimo kwa ajili ya kukuza ujuzi kwenye zao la korosho waliopo kwenye kata kwa ajili ya kushirikiana na wataalam wa kilimo wa Halmashauri katika kutoa elimu ya kilimo bora cha korosho na usimamizi wa usajili, uhuishaji wa kanzi data ya wakulima wa korosho na ugawaji wa pembejeo za ruzuku za korosho kwa wakulima.

### 5.2.8. Vitendea kazi

Vitendea kazi kwa maafisa ugani kilimo wote. Wataalam wa kilimo wote wamepatiwa vitendea kazi; Pikipiki kwa ajili ya kurahisisha kuwafikia wakulima pamoja na vishikwambi.

### 5.2.9. Upatikanaji wa pembejeo za ruzuku za korosho kwa wakulima wa korosho.

Kwa kipindi cha misimu mnne (4) kuanzia msimu 2021/2022 hadi 2024/2025, Mkoa umepokea viuatilifu vya unga (**salfa)** jumla ya kilo **12,883,123** na viuatilifu vya maji **Lita 808,865**.

**Mapokezi ya pembejeo za korosho kuanzia msimu 2021/2022 hadi 2024/2025**

| Na | Msimu / Mwaka | Viuatilifu vya Unga (Salfa) (Kg) | Viuatilifu vya Kudhibiti Wadudu 'Sumu' (Lita) | Viuatilifu vya Kudhibiti Magonjwa (Lita) |
|---|---|---|---|---|
| 2 | 2021/2022 | 265,187 | 37,883 | 136,701 |
| 3 | 2022/2023 | 1,484,441 | 36,555 | 188,774 |
| 4 | 2023/2024 | 5,140,745 | 37,097 | 100,500 |
| 5 | 2024/2025 | 5,992,750 | 58,805 | 212,550 |
| | **JUMLA** | **12,883,123** | **170,340** | **638,525** |

### 5.2.10. Changamoto zinazokabili shughuli za uendelezaji zao la korosho na mapendekezi ya utatuzi wake

i. **Ukosefu wa kiwanda kikubwa cha kupangua korosho Tunduru**

Kufungwa kwa shughuli za ubanguaji wa korosho kwenye kiwanda cha Korosho Africa kilichochopo wilaya ya Tunduru kimepunguza hamasa ya wakulima kuona fursa zaidi kwenye zao la korosho zaidi ya kuuza korosho ghafi tu. Utofauti wa hali ya hewa kati ya Wilaya ya Namtumbo na sehemu za wazalishaji wakubwa wa ukanda wa pwani, hali inayochelewesha msimu wa masoko kwa wakulima wa Namtumbo hivyo kuchangia kuporomoka kwa thamani ya zao sokoni.

ii. **Utatuzi**

Kiwanda kilichokuwepo kifunguliwe ili shughuli za kiwanda ziweze kuendelea;

Kutoa elimu ya mara kwa mara pamoja na hamasa kwa wakulima ili waweze kuhudumia vyema zao la korosho kwa manufaa yao na serikali ili kuongeza tija ya uzalishaji.

### 5.2.11. Mikakati ya kuendeleza zao la korosho ifikapo 2029/2030

Mkoa/Wilaya/Halmashauri tunaendelea kushirikiana na Wizara ya Kilimo kupitia Bodi ya Korosho Tanzania na Taasisi ya Utafiti wa kilimo Tanzania Kituo cha Naliendele (TARI – Naliendele) kuhakikisha Mbegu/miche bora ya korosho inazalishwa na kusambazwa kwa wakulima ili kuongeza eneo la kilimo cha korosho na uzalishaji; Kuhamasisha wakulima wengi kufufua mashamba pori ya mikorosho yaliyotelekezwa na kuyahudumia kwa kufuata ushauri wa wataalam wa kilimo; Kuwa na mashamba makubwa ya pamoja (Block farming) ya korosho; na Kuhamasisha, Kufufua na kusajili vikundi vya ubanguaji korosho kwa wingi

### 5.2.12. Hitimisho.

Zao la korosho katika Mkoa wa Ruvuma ndiyo zao kuu la kibiashara na kiuchumi kwa wananchi, Tunaendelea kuishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoobgozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania kuendelea kuweka kipaumbele katika juhudi za uwekezaji mkubwa katika Tasnia ya Korosho kupitia Bodi ya Korosho Tanzania, Mikoa, Wilaya na Halmashauri.

## 5.3 TAARIFA YA MKOA WA PWANI

### 5.3.1. Utangulizi

Korosho ni zao kuu la biashara katika Mkoa wa Pwani, Mkoa wa Pwani unashika nafasi ya nne (4) Kitaifa katika uzalishaji wa zao la Korosho baada ya Mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma. Mkoa unahimiza wananchi wake kulima zao la Korosho kwa wingi kwa kufuata kanuni bora za kilimo na kuongeza tija ya uzalishaji ili kukuza pato la mkulima mojamoja na Taifa kwa ujumla.

### 5.3.2. Uzalishaji Msimu wa 2024/2025 na Mpango wa Uzalishaji ifikapo Msimu wa 2029/2030

#### 5.3.2.1 Uzalishaji Msimu wa 2024/2025

Uzalishaji wa zao la korosho Mkoa wa Pwani msimu wa 2024/2025 ni tani 25,862 kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini.

**Uzalishaji wa korosho ghafi Msimu wa 2023/2024**

| Na | Halmashauri | Uzalishaji (Tani) |
|---|---|---|
| 1. | Kibiti | 10,990 |
| 2. | Bagamoyo | 301 |
| 3. | Kibaha | 241 |
| 4. | Kisarawe | 756 |
| 5. | Kibaha Mji | 360 |
| 6. | Mafia | 64 |
| 7. | Chalinze | 127 |
| 8. | Mkuranga | 8,222 |
| 9. | Rufiji | 4,806 |
| | **Jumla** | **25,862** |

#### 5.3.2.2 Makadirio ya uzalishaji wa zao la korosho Msimu wa 2025/2026 na 2026/2027

Kutokana na malengo ya Kitaifa yaliyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya kuzalisha tani 700,000 za korosho ghafi hapa nchini ifikapo 2026/27, na tani 1,000,000 ifikapo mwaka 2029/30, Mkoa wa Pwani una malengo kama kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini:

**Malengo ya uzalishaji wa zao la korosho hadi kufikia msimu wa 2026/2027**

| Halmashauri | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 |
|---|---|---|---|---|
| Kibiti | 12,500 | 13,000 | 13,500 | 14,000 |
| Bagamoyo | 250 | 250 | 250 | 250 |
| Kibaha | 600 | 650 | 700 | 700 |
| Kisarawe | 2,140 | 2,200 | 2,500 | 3,000 |
| Kibaha Mji | 250 | 250 | 240 | 240 |
| Mafia | 500 | 551 | 560 | 560 |
| Chalinze | 300 | 310 | 320 | 330 |
| Mkuranga | 12,000 | 13,000 | 14,000 | 15,000 |
| Rufiji | 9,000 | 10,000 | 11,000 | 12,000 |
| **JUMLA KUU** | **37,540** | **40,211** | **43,070** | **46,080** |

*Chanzo: Halmashauri*

#### 5.3.2.3 Mpango wa Upatikanaji wa Mbegu na Miche bora ya Korosho

Mkoa wa Pwani una mipango mbalimbali ya upatikanaji wa mbegu kama ifuatavyo:-

i. Kushirikiana na Bodi ya Korosho ili kuhakikisha Mkoa wa Pwani unapata mgao wa miche bora kilo 101,000 kwa msimu wa 2025/2026 kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini

**Mahitaji ya Miche bora ya korosho Mkoa wa Pwani**

| Na. | Halmashauri | Mahitaji ya Miche |
|---|---|---|
| 1 | Rufiji | 22,000 |
| 2 | Kibiti | 5,000 |
| 3 | Mkuranga | 20,000 |
| 4 | Kisarawe | 12,000 |
| 5 | Mafia | 10,000 |
| 6 | Chalinze | 10,000 |
| 7 | Kibaha Mji | 2,000 |
| 8 | Bagamoyo | 5,000 |
| 9 | Kibaha | 15,000 |
| | **Jumla** | **101,000** |

ii. Kuhimiza Halmashauri kurudisha mapato ya asilimia 20 yanayotikana na ushuru wa zao la korosho ili kuendeleza zao la korosho ikiwemo kununua mbegu bora.

iii. Kushirikiana na Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Pwani CORECU ili kuhakikisha kinanunua mbegu bora kwa ajili ya wakulima.

### 5.3.3. Ubaguaji Msimu wa 2025/26 na Mpango ifikapo 2029/30

**Ubanguaji msimu 2025/2026**

| Na. | Halmashauri | Kiasi cha korosho kilichobanguliwa (Kilo) |
|---|---|---|
| 1 | Kibiti | 3,000 |
| 2 | Bagamoyo | 7,000 |
| 3 | Kibaha | 256,320 |
| 4 | Kisarawe | 3,360 |
| 5 | Kibaha Mji | 80,000 |
| 6 | Mafia | 0 |
| 7 | Chalinze | 0 |
| 8 | Mkuranga | 1,969,746 |
| 9 | Rufiji | 0 |
| | **JUMLA** | **2,319,426** |

#### 5.3.3.1. Mpango/Makadirio ya Ubanguaji misimu ya 2026/27, 2027/28, 2028/29 na 2029/30

Mpango wa ubanguaji wa korosho Mkoa wa Pwani kuanzia msimu wa 2026/27 hadi msimu wa 2029/30 umeoneshwa katika jedwali hapo chini;

**Malengo ya ubanguaji wa korosho ghafi.**

| Halmashauri | Misimu | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 |
| Kibiti | 12 | 15 | 20 | 25 |
| Bagamoyo | 30 | 32 | 35 | 40 |
| Kibaha | 1000 | 1,200 | 1,500 | 2,000 |
| Kisarawe | 50 | 55 | 60 | 65 |
| Kibaha Mji | 45 | 50 | 55 | 60 |
| Mafia | 275 | 280 | 285 | 290 |
| Chalinze | 5 | 7 | 10 | 12 |
| Mkuranga | 2,000 | 2,200 | 2,500 | 2,700 |
| Rufiji | 20 | 22 | 23 | 25 |
| **JUMLA** | **3,437** | **3,,861** | **4,488** | **5,217** |

*Chanzo: Halmashauri*

### 5.3.4. Hali ya Huduma za Ugani na Mafunzo na Mpango wa 2025/26

Halmashauri za Wilaya Mkoa wa Pwani zimeendelea kutoa mafunzo kwa wakulima ikiwa ni pamoja na kuzingatia kanuni bora za kilimo zitakazopelekea uzalishaji wa tija katika zao la korosho ili kufikia malengo ya tija ya tani 3 kwa hekta. Mafunzo hayo yamefanyika kwa kushirikiana na Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Pwani pamoja na Bodi ya Korosho.

### 5.3.5. Changamoto zinazolikabili shughuli za uendeshaji wa zao la korosho na mapendekezo ya utatuzi wake

Zipo changamoto kadhaa zinazolikabili zao la korosho kwenye uzalishaji na mauzo kwa Mkoa wa Pwani. Changamoto hizo ni pamoja na: -

i. Kutokuhudumiwa kwa mikorosho hasa palizi na upuliziaji wa viuatilifu kwa wakati.
ii. Pembejeo kuchelewa kuwafikia wakulima katika baadhi ya maeneo
iii. Miundombinu duni hivyo kuathiri usafirishaji
iv. Upungufu wa mabomba ya kupulizia mikorosho

Pamoja na changamoto hizo Mkoa unapendekeza masuala yafuatayo:-

i. Kuendelea kuhimiza wakulima kuhudumia mikorosho ikiwemo kupuliza madawa na kusafisha mashamba kwa wakati ili kuzalisha korosho bora.
ii. Pembejeo za korosho ziwafikie wakulima kwa wakati kwa kuzingatia mahitaji

iii. Kuboresha miundombinu ya barabara ili kurahisisha usafirishaji
iv. Kuongeza upatikanaji wa mabomba

### 5.3.6. Mikakati ya kuendeleza zao la korosho ifikapo 2029/2030

Mkoa wa Pwani una mikakati ifuatayo ili kuendeleza zao la Korosho.

i. Kuendelea kutoa elimu ya Kilimo Bora cha zao la Korosho kwa wakulima hususani kuwahimiza kusafisha mashamba yao ili kupunguza athari ya magonjwa, wadudu waharibifu na kurahisisha uokotaji wa Korosho.
ii. Kutoa elimu kwa wakulima juu ya umuhimu wa kukausha na kudararisha vizuri korosho baada ya kuvuna ili kulinda ubora wa Korosho.
iii. Kuendelea kuhamasisha wakulima wa korosho kupanda miche bora ambayo huzaa kwa wingi na kwa muda mfupi.
iv. Wataalam wa Kilimo na Ushirika kwa kushirikiana na Chama Kikuu cha Ushirika (CORECU) kuendelea kusimamia kikamilifu usambazaji wa vifungashio ili viwafikie wakulima kwa wakati.
v. Kuhamasisha uanzishwaji wa mashamba makubwa ya pamoja (Block farming).

### 5.3.7. Hitimisho

Mkoa wa Pwani umejipanga kuinua uzalishaji wa zao la korosho kutoka tani 25,862 msimu 2024/25 hadi kufikia tani 36,000 ifikapo 2026/27 na kufikia tani 46,000 ifikapo mwaka 2029/30 kwa kutekeleza mikakati mbaimbali. Hali hii itachochea na kuimarisha kwa kiasi kikubwa uchumi wa Mkulima mmoja mmoja na Mkoa kwa ujumla. Kuendelea kuhamasisha na kuviwezesha vikundi vya wabanguaji wa korosho ili viwe na uwezo wa kubangua korosho kwa kiwango kikubwa zaidi hali itakayochochea ukuaji wa uchumi.

## 5.4 TAARIFA YA MKOA WA TANGA

### 5.4.1 Utangulizi

Zao la korosho Mkoani Tanga linalimwa katika Halimashauri tisa (9) zenye jumla ya mikorosho 421,164 na wakulima 3,292. Halmashauri tano (5) zikiwa ni za asili na 4 zikiwa mpya. Halmashauri za asili ni Mkinga, Pangani, Muheza, Korogwe (W) na Korogwe (M). wakati  halmashauri mpya ni Handeni (W), Handeni (M), Korogwe (M)

na Kilindi ambazo zilianza kujishughulisha na kilimo cha zao la korosho kuanzia mwaka 2018. Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga ndiyo inayoongoza kwa uzalishaji.

### 5.4.2 Uzalishaji wa korosho msimu wa 2024/2025 na mpango wa uzalishaji msimu wa mwaka 2029/2030

#### 5.4.2.1 Uzalishaji msimu wa 2024/2025

Msimu wa mwaka 2024/2025 jumla ya tani 586.9 ziliuzwa katika mfumo rasmi. Katika mauzo hayo jumla ya tani 112.1 ziliuzwa katika Soko la awali na tani 474.8 zikiuzwa kwa mfumo wa TMX. Aidha tani 39.1 zikiwa ni daraja la kwanza (SG) na tani 547.7 zikiwa ni daraja la pili (UG).

**Mpango/makadirio ya uzalishaji ya uzalishaji kiwilaya msimu wa 2025/2026, 2026/2027, 2027/2028, 2028/2029 na 2029/2030**

| Halmashauri | Makadirio ya uzalishaji | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2025/2026 | 2026/2027 | 2027/2028 | 2028/2029 | 2029/2030 |
| Mkinga | 249 | 270 | 285 | 300 | 315 |
| Pangani | 100 | 110 | 115 | 120 | 125 |
| Tanga jiji | 50 | 55 | 60 | 70 | 75 |
| Muheza | 13 | 18 | 20 | 25 | 28 |
| Korogwe DC | 35 | 38 | 50 | 57 | 60 |
| Korogwe TC | 12.35 | 15 | 19 | 23 | 27.64 |
| Handeni DC | 47 | 52.71 | 60 | 65 | 80 |
| Handeni TC | 7 | 9 | 13 | 15.82 | 18 |
| Kilindi | 3 | 4 | 5 | 7 | 9 |
| **Jumla** | **1,000** | **1300** | **1500.45** | **1800** | **2000.5** |

#### 5.4.2.2 Mpango wa upatikanaji wa mbegu na miche bora ya mikorosho

Msimu wa 2024/2025 jumla ya kg 1,660 ya mbegu bora ya korosho ilipokelewa toka Bodi ya Korosho na na kuzalisha jumla ya miche 68,747 na kusambazwa kwa wakulima bure.

**Kiasi cha miche iliyozalishwa na Halmashauri na kugawiwa bure kwa wakulima msimu wa 2024/2025.**

| Halmashauri | Kiasi cha mbegu kilichogawiwa kwa Halmashauri (kg) | Idadi ya miche iliyozalishwa | Maoni |
|---|---|---|---|
| Mkinga DC | 160 | 15,000 | |
| Pangani DC | 230 | 13,862 | |
| Tanga jiji | 90 | 4000 | |
| Korogwe DC | 50 | - | Ziligawiwa mbegu kwa wakulima na kupanda shambani moja kwa moja |
| Korogwe DC | 90 | 2,400 | |
| Muheza | 60 | 6,300 | |
| Handeni DC | 700 | 25,285 | |
| Handeni TC | | | |
| Kilindi | 100 | | Zitazalishwa msimu msimu wa Vuli |
| **Jumla** | **1,660** | **68,747** | |

### 5.4.3 Ubanguaji wa korosho msimu wa 2024/2025 na mpango wa ubanguaji ifikapo msimu wa 2029/2030

#### 5.4.3.1 Ubanguaji msimu wa 2024/2025

Msimu wa 2024/2025, jumla ya tani 27 zilifanikiwa kubanguliwa kupitia vikundi rasmi pamoja na wakulima wadogo wadogo kwa njia mbalimbali za kienyeji. Kiasi cha korosho kilichobanguliwa msimu wa mwaka 2024/2025

| Na. | Halmashauri | Kiasi kilichobanguliwa (Tani) | Wabanguaji |
|---|---|---|---|
| 1. | Pangani | 15 | Vikundi 2 na wakulima binafsi |
| 2. | Muheza | 5 | Vijana binafsi wanaouza barabarani |
| 3. | Mkinga | 2 | Vikundi |
| 4. | Handeni DC | 3 | Watu binafsi |
| 5 | Tanga jiji | 2 | Mtu binafsi |
| | **Jumla** | **27** | |

#### 5.4.3.2 Mpango/makadirio ya ubanguaji kiwilaya msimu wa 2025/2026, 2026/2027, 2027/2028, 2028/2029 na 2029/2030

| **Halmashauri** | **Makadirio ya Mpango wa ubanguaji** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **2025/2026** | **2026/2027** | **2027/2028** | **2028/2029** | **2029/2030** |
| Mkinga | 95 | 100 | 150 | 200 | 230 |
| Pangani | 65 | 70 | 80 | 100 | 122 |
| Tanga jiji | 5 | 10 | 20 | 25 | 27 |
| Muheza | 17 | 20 | 30 | 34 | 37 |
| Korogwe DC | 0 | 3 | 10 | 13 | 15 |
| Korogwe TC | 0 | 2 | 8 | 15 | 18 |
| Handeni DC | 10 | 15 | 17 | 20 | 32 |
| Handeni TC | 3 | 5 | 9 | 12 | 15 |
| Kilindi | 0 | 2 | 3 | 3.5 | 4 |
| **Jumla** | **195** | **227** | **327** | **422.5** | **500** |

### 5.4.4 Huduma za ugani na mafunzo

Mafunzo ya usimamizi na uthibiti ubora kutolewa kwa maafisa ugani kata 100 wa Halmashauri, wakulima viongozi 120, Wathibiti ubora (BBT korosho) 24, Viongozi wa AMCOS 120 na vikundi 8 vya wabanguaji. Aidha, Maafisa Kilimo/BBT korosho 24 walipewa mafunzo kuhusu kilimo bora cha korosho.

**Changamoto zinazokabili shughuli za uendelezaji wa zao na korosho na utatuzi wake**

| Na. | Changamoto | Utatuzi wake |
|---|---|---|
| | **Changamoto za uzalishaji** | |
| 1. | Mabadiliko ya tabia nchi yaliyopelekea uzalishaji duni | • Wakulima kuendelea kuhamasishwa kupanda mbegu bora zinazostahili mabadiliko ya tabia ya nchi na zenye ukinzani dhidi ya magonjwa na wadudu.<br>• Jumla ya miche bora 68.747 ilizalishwa na kugawanywa bure kwa wakulima kupitia kilo 1,660 ya mbegu bora iliyosambazwa na Bodi ya korosho kwenye Halmashauri za mkoa wa Tanga. |
| 2. | Mashamba mengi ya mikorosho yametekelezwa/mashamba pori | Zoezi la kuondoa mashamba pori kuwa endelevu kwa kila kijiji. Jumla ya mashambapori 3,382 yaliibuliwa na jumla ya ekari 980 zimeshafufuliwa na zoezi ni endelevu.<br>Maafisa ugani walioajiriwa wameelekezwa kuifanya hii agenda yao kuu na itakuwa moja ya KPI (RC-Tanga). |
| 3. | Mikorosho mingi imezeeka | Uanzishwaji wa mashamba darasa kwa kila kata. Jumla ya mashamba darasa 17 yameshaanzishwa yakiwemo kufufua ya zamani na mapya. |
| 4. | Kutokuwepo kwa bajeti ya kuendeleza zao katika Halmashauri za Wilaya. | Mkoa unaendelea kuhamasisha Halmashauri kutenga bajeti ya kutosha ya kuendeleza zao la korosho.<br>• Msimu wa 2024/2025 Tsh 35, 900,000/= na Msimu wa 2025/2026 Tsh 42, 050,000/= |
| 5. | Kangomba – Ununuzi holela wa korosho ghafi kupeleka nje ya Mkoa unasababisha kutokuwa na takwimu halisi ya uzalishaji na mauzo | • Kangomba kuthibitiwa kwa kuweka wakaguzi wa korosho kwenye mageti. |
| 6. | Uzalishaji mdogo wa korosho unasababisha kutokuwepo kwa ushindani | • Kuimarishwa kwa huduma za ugani kwa kupewa pikipiki.Jumla ya Pikipiki 373 `kugawiwa kwa wagani -373 toka serikali kuu na 7 toka bodi ya koroshoTanzania. |
| 7. | Ufahamu mdogo wa wakulima wa katika matumizi ya viuatilifu | • Mafunzo ya usimamizi na uthibiti ubora kutolewa kwa maafisa ugani kata 100 wa Halmashauri, wakulima viongozi 120, Wathibiti ubora (BBT korosho) 24, Viongozi wa AMCOS 120 na vikundi 8 vya wabanguaji. Aidha, Maafisa |

| | | |
|---|---|---|
| | | Kilimo/BBT korosho 24 walipewa mafunzo kuhusu kilimo bora cha korosho.<br>● Upatikanaji wa viutilifu vya kutosha kwa wakulima. Takriba. Mkoa ulipokea mgao wa Salfa ya unga (Simba Sulphur) mifuko 5,974 sawa na tani 149.350, Viuatilifu vya maji lita 14,693 ikiwa ni sumu za wadudu |
| **B.** | **Changamoto za ubanguaji** | |
| 1. | Ukosefu wa malighafi kwa ajili ya ubanguaji kutokana na uzalishaji mdogo uliosababishwa na mabadiliko ya tabianchi - mvua kubwa/ukame. | ● Wakulima wamehamasishwa kuongeza uzalishaji kwa kupanda mbegu bora zenye kutoa mavuno mengi na inayostahili ukame na yenye ukinzani kwa magonjwa na visumbufu vya mazao. |
| 2. | Ukosefu wa mashine za kisasa za kubangua korosho kwa vikundi vya wakulima | ● Halmashauri zimeshauriwa kukopesha vikundi vya ubanguaji kupiti 10% (Vijana, wanawake na wenye ulemavu)<br>● Kuiomba bodi ya korosho Tanzania kuviwezesha vikundi mashine ndogo za ubanguaji pamoja na elimu rejea ya ubanguaji. |
| 3. | Halmashauri kutokurejesha 20% kwa ajili ya kuendeleza zao | Halmashauri zimeshaanza kutenga fedha kwa ajili ya kuendeleza zao la kprosho<br>● Msimu wa 2024/2025 Tsh 35, 900,000/=<br>● Msimu wa 2025/2026 Tsh 42, 050,000/= |
| 4. | Ufahamu mdogo wa wakulima juu ya elimu ya ubanguaji wa korosho | ● Elimu rejea ya mnyororo wa thamani wa zao la Korosho kupitia CARE International na Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga imetolewa kwa kwa Maafisa kilimo 48 ngazi ya wilaya, kata na vijiji kwa ajilinya kuongeza tija na ubanguaji |
| 5. | Mitaji midogo kwa wakulima wanaobangua korosho | Halmashauri zimeshauriwa kuwezesha vikundi mitaji kwa ajili ya ubanguaji wa ndani |
| 6. | Kangomba – Ununuzi holela wa korosho ghafi nje ya Mkoa unaosababisha kutokuwa na takwimu halisi ya ubanguaji na mauzo. | ● Mauzo kwa mfumo wa stakabadhi ghalani umeimarishwa pamoja na uwepo wa AMCOS 15 za uratibu mauzo<br>● Uwepo wa mageti ya Ukaguzi wa magari ya abiria na mizigo yanayopitisha korosho na faini kutolewa kwa mwenye gari pindi anapobainika kupakia korosho. |

### 5.4.5 Mikakati ya kuendeleza zao la korosho Mkoa wa Tanga

i. Wakulima kuendelea kuhamasishwa kupanda miiche bora ya korosho inazostahili mabadiliko ya tabianchi na zenye ukinzani dhidi ya magonjwa na wadudu.

ii. Uzalishaji wa miche bora nakuisambaza kwa wakulima.Jumla ya miche 68,747 imesambazwa msimu wa mwaka 2024/2025 na msimu wa mwaka 2025/2026 itasambazwa miche 300,000

iii. Zoezi la usajili wa wakulima na mikorosho kuwa endelevu.Jumla ya wakulima 3,292 wameshahuisha takwimu zao.

iv. Upatikanaji wa viutilifu vya kutosha kwa wakulima kwa wakati. Mkoa ulipokea mgao wa Salfa ya unga (Simba Sulphur) mifuko 5,974 sawa na tani 149.350, Viuatilifu vya maji lita 14,693 ikiwa ni sumu za wadudu

v. Uwepo wa kampeni endelevu wa ufufuaji wa mashamba pori na mikorosho iliyozeeka

vi. Uwepo wa shirika la CARE International linalotoa mafunzo kuhusu kilimo bora cha korosho na uongezaji wa thamani

vii. Uwepo wa chama kikuu cha Korosho (TACACU) pamoja na AMCOS 15 zinazoratibu mauzo na upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima

viii. Kuhamasisha wakulima kuchanganya mazao ili kurahisisha palizi-nyenzo ya kuondoa mashamba pori na kuongeza kipato

ix. Kuwasimamia kwa karibu maafisa ugani kutekeleza majukumu yao kwa wakulima ilikuongeza tija kwa eneo.

### 5.4.6 Hitimisho na maoni

#### 5.4.6.1 Maoni

i. TCB iweke utaratibu wa kutoa mbegu za mazao mengine ya chakula kwa wakulima wa korosho kwa njia ya ruzuku ili kuwawezesha kufanya kilimo mchanganyo kwa lengo;

- Kuondoa Mashamba pori
- Usalama wa chakula na lishe katika jamii hasa pale wanapokuwa nje ya msimu wa mavuno ya korosho
- Kuongeza uzalishaji wa korosho

ii. TCB kwa kushirikiana na LGA iweke nguvu ya pamoja ya kutoa elimu na vifaa vya vya ubanguaji wa korosho kupitia vikundi vya wakulima wadogo na AMCOS ili waweze kubangua na kuuza korosho karanga badala ya korosho ghafi na kujiongezea kipato zaidi.
iii. Awepo afisa ubanguaji katika kila halmashauri/wagani wapewe mafunzo kuhusu ubangauji ili mnyororo wathamani ukamilike
iv. Maeneo mengi ya mashamba yamekuwa yakitumia sulphur kama kiwatilifu cha kuzuia ukungu na magonjwa mengine kwenye Mkorosho kuna uwezekano wa hali ya udongo kuwa na pH ndogo ni vema zoezi la upimaji sampuli za udongo kwenye mashamba ya wakulima likafanyika ili Wizara ikaona namna ya kuweka ruzuku ya "Agricultural lime" kwenye kilimo cha korosho.

#### 5.4.6.2 Hitimisho

Tunashukuru Bodi ya Korosho Tanzania/ niaba ya serikali

i. Kutuletea pembejeo kwa wakati
ii. Kutusafirishia viwatilifu vya unga hadi Tanga

## 5.5 TAARIFA YA MKOA WA MOROGORO

### 5.5.1 Utangulizi:

Mkoa wa Morogoro ni moja kati ya Mikoa inayolima Korosho nchini na kuendelea na utekelezaji wa mikakati mbalimbali kwa lengo la kulisimamia zao hilo katika Halmashauri nane kati ya tisa zilizopo hapa Mkoani Morogoro. Halmashauri za Wilaya zinazolima zao la Korosho ni Malinyi, Kilosa, Gairo, Morogoro, Mlimba, Mvomero, Ulanga na Halmashauri ya Mji wa Ifakara. Mkoa una zaidi ya Hekta 15,890 zilizopandwa Mikorosho na tunategemea ongezeko kwa siku zijazo kutokana na hamasa zinazoendelea.

### 5.5.2 Uzalishaji wa Korosho 2024/2025 na mpango wa uzalishaji ifikapo 2029/2030.

#### 5.5.2.1 Uzalishaji wa Korosho 2024/2025

Mkoa wa Morogoro unazalisha kiasi kidogo cha Korosho kwani mikorosho mingi iliyopandwa bado michanga na haijaanza kuvunwa rasmi. Kwa msimu wa 2024/2025 Mkoa ulifanikiwa kuzalisha Jumla ya Tani 527,010 za Korosho.

| Na | Halmashauri | Kiasi kilichozalishwa 2024/2025 (Kg) |
|---|---|---|
| 1. | Ifakara Mji | 103,000 |
| 2. | Malinyi Dc | 208,677 |
| 3. | Mlimba Dc | 54,350 |
| 4. | Ulanga Dc | 224,400 |
| 5. | Kilosa | 38,500 |
| 6. | Morogoro Dc | 52,000 |
| 7. | Mvomero | 20,000 |
| 8. | Gairo | 721 |
| | **Jumla** | **701,648** |

Katika Msimu wa 2024/2025 mauzo ya zao la korosho yalifanyika kupitia chama kikuu cha UKICU na jumla ya **kilo 590,786** zenye Thamani ya **Tshs. 1,581,362,794.36** ziliuzwa. Katika minada hiyo bei ya wastani ilikua **Tsh. 2,676.71**

N:B Chama kikuu MOFACU waliujza kilo 20,454 kwa bei ya shilingi 2210 na 20410.

***Mauzo ya korosho msimu wa 2024/2025 kwa kila Halmashauri.***

| Halmashauri | Amcos zinazoshiriki | Korosho (Kg) | Thamani (TSHS) |
|---|---|---|---|
| Ifakara Mji | 3 | 103,280 | 276,450,608.8 |
| Mlimba | 2 | 54,350 | 145,479,188.5 |
| Malinyi | 7 | 208,756 | 558,779,272.76 |
| Ulanga | 4 | 224,400 | 600,6543,724 |
| **Jumla** | **16** | **590,786** | **1,581,362,794.36** |

**Mpango/Makadirio ya uzalishaji 2025/2026, 2026/2027, 2027/2028, 2028/2027 na 2029/2030.**

| Halmashauri Uzalishaji (Tani) | 2025/26 | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/2030 |
|---|---|---|---|---|---|
| Gairo | 68.15 | 76 | 83.3 | 98.7 | 126.74 |
| Ifakara Mji | 136 | 170 | 204 | 438 | 576 |
| Kilosa | 35 | 67 | 89 | 115 | 205 |
| Malinyi | 374 | 440 | 506.9 | 676.9 | 747 |
| Mlimba | 30.5 | 40.6 | 50.4 | 55.6 | 70.5 |
| Morogoro | 62 | 64.7 | 70 | 90.5 | 102 |
| Mvomero | 36 | 47 | 53 | 79 | 96 |
| Ulanga | 203.6 | 305.5 | 407.3 | 509.1 | 576 |
| **Jumla** | **945.25** | **1,210.8** | **1463.9** | **2,062.8** | **2,502.24** |

#### 5.5.2.2 Mpango wa upatikanaji na Usambazaji wa Miche/Mbegu

Katika msimu wa Kilimo wa 2023/2024 Mkoa haujapokea mbegu/ miche kutoka Bodi ya Korosho moja kwa moja bali zipo baadhi ya Halmashauri zilipokea mbegu kutoka Bodi ya Korosho moja kwa moja. Mfano Halmashauri ya Malinyi walipata jumla ya Kilo 500 na Mji Ifakara walipokea kilo 200. Lakini sambamba na hilo Halmashauri zimekuwa zikitenga bajeti kwa lengo la kuzalisha miche na kuisambaza bure kwa Wakulima. Kwa mfano Halmashauri za Wilaya zilizotenga pesa kwa ajili ya uzalishaji miche ni Ulanga Tsh. 4,000,000/= ili kuzalisha miche zaidi ya 100,000/=.

Aidha Msimu wa 2024/25 kupitia ofisi ya Bodi ya Korosho iliyopo Mkoani Morogoro Jumla ya Kilo 1,200 ziligawiwa katika Halmashauri 4 kwa ajili ya kuanzisha vitalu vya miche kama Ifuatavyo;- Malinyi kilo 300, Mbilmba kilo 200, Kilosa kilo 400 na Morogoro kilo 400. Kati ya mbegu hizi Halmashauri ya Malinyi ilifanikiwa kuanzisha Kitalu cha Miche 50,000. Halmshjauri zingine zinajipanga kuanzisha vitalu msumu unaofuata. Msimu wa 2025/2026, Halmashauri ya Morogoro imejipanga kuzalisha miche 85,000, halmashauri ya Mlimba imepanga kuzalisha miche 50,000. Halmashauri ya Malinyi pia imepanga kuzalisha miche 50,000 kwa ajili ya kuigawa bure kwa Wakulima, Halmashauri ya Kilosa imetenga Tsh. 3,440,000/= kwa lengo la kuzalisha miche na kuigawa bure kwa Wakulima Wadogowadogo.

| **Na.** | **Halmashauri** | **Idadi ya Miche iliysambazwa** | **Idadi ya mbegu zilizosambazwa (kg)** |
|---|---|---:|---:|
| 1. | Gairo | 0 | 0 |
| 2. | Ifakara Mji | 10,512 | 0 |
| 3. | Kilosa | 0 | 350 |
| 4. | Malinyi | 50,000 | 0 |
| 5. | Mlimba | 0 | 485 |
| 6. | Morogoro | 20,000 | 0 |
| 7. | Mvomero | 0 | 0 |
| 8. | Ulanga | 22,000 | 0 |
| | **Jumla** | **102,512** | **835** |

### 5.5.3 Ubanguaji msimu wa 2025/2026 na mpango wa ubanguaji ifikapo 2029/2030 Halmashauri ya Ulanga kilo, 4,231, Malinyi kilo 260

**Mpango wa ubanguaji 2025/2026, 2026/2027, 2027/2028, 2028/2027 na 2029/2030.**

| Mwaka | Mpango wa Mavuno (kilo) |
|---|---:|
| 2025/2026 | 203,644 |
| 2026/2027 | 305,466 |
| 2027/2028 | 407,288 |
| 2028/2029 | 509,110 |
| 2029/2030 | 610,932 |
| **Jumla** | **2,036,440** |

### 5.5.4 Hali ya huduma za ugani

Hali ya huduma za ugani ni nzuri kutokana na wataalamu kupatiwa usafiri wa Pikipiki hivyo kuweza kuwafikia wakulima wengi zaidi. Maafisa wa ugani wanotumika ni wale wa Halmashauri ambao pia hutoa huduma ya ugani kwa mazao mengine yanayolimwa katika kata husika. Kwa msimu wa 2024/2025 Jumla ya Maafisa Ugani walipatiwa elimu ya udhibiti wa visumbufu. Mpango kwa mwaka 2025/2026 ni kuendelea kushirikiana na Bodi ya Korosho na TARI Naliendelea kuendela kutoa elimu kwa Maafisa ugani 100.

Idadi ya wataalam na wakulima waliopatiwa elimu

| Na. | Halmashauri | Idadi ya Wataalam | Idadi ya Wakulima |
|---|---|---|---|
| 1 | Mlimba | 12 | 379 |
| 2. | Malinyi | 20 | 356 |
| 3. | Ulanga | 15 | 137 |

### 5.5.5 Changamoto na Utatuzi

Katika kutekeleza mpango wa kuendeleza zao la korosho Wakulima wanakabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:

i. Viuatilifu vya ruzuku vya korosho kutoka Bodi ya Korosho kuchelewa kuwafikia wakulima.
ii. Ukosefu wa zana bora za kupulizia sumu (motorized blowers) kwa ajli ya kudhibiti visumbufu vya korosho.

iii. Uwepo wa walanguzi wa korosho (Kangomba) ambao huwarubuni baadhi ya wakulima na kwenda kuuza korosho hizo Mikoa ya Pwani na Lindi hivyo kuzikosesha Halmashauri mapato na kutopata takwimu sahihi za mwenendo wa uzalishaji wa korosho.
iv. Uvamizi wa mifugo kwenye mashamba ya mikorosho hasa katika maeneo mbalimbali jambo ambalo linaathiri uzalishaji na takwimu sahihi ya miche ya mikorosho mashambani.
v. Baadhi ya Wakulima kuyatelekeza mashamba ya mikorosho na kuonekana kama mashamba pori na hivyo kupelekea baadhi ya Wafugaji kuchungia mifugo yao hasa ng’ombe.
vi. Taarifa za usambazaji au ugawaji wa mbegu/ miche kwa Halmashauri kutoka Bodi ya Korosho Nchini bila kuishirikisha Ofisi ya Mkuu wa Mkoa moja kwa moja hupelekea kutokuwa na takwimu sahihi za shughuli za kuliendeleza zao hilo.
vii. Ugawaji wa viuatilifu vya korosho uendane na mahitaji sahihi ya Wakulima ambao wamesajiliwa kwenye daftari.

### 5.5.6 Mapendekezo ya kukabiliana na changamoto

i. Bodi ya Korosho inatakiwa kuweka utaratibu mzuri utakaowezesha wakulima kupata vipulizia sumu (motorized blowers) kwa njia ya mkopo kupitia AMCOS zao ili waweze kurejesha mikopo hiyo mara tu watakapouza mazao yao. Morogoro ina VyamaVikuu vya Ushirika (MOFACU & UKICU) na vyama vya msingi kwa ajili ya kuwahudumia Wakulima. Tunashauri mabomba yatakayopatikana kwa bei ya ruzuku yaletwe Morogoro ili Wakulima wauziwe.
ii. Kushirikiana na Bodi ya Korosho kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa Maafisa ugani na Wakulima juu ya udhibiti wa visumbufu na ubanguaji wa korosho kwa Wakulima sababu kuna fedha zinakatwa kwa kila kilo ya korosho inayouzwa kwa ajili ya kuendeleza zao la korosho.
iii. Kubainisha idadi ya Wakulima Wadogo na Wakubwa ambao wanalima au wanampango wa kulima zao la Korosho kwa msimu huu wa 2025/2026 na kujua ukubwa wa mashamba yao kwa kuwasajili katika Daftari maalum. Zoezi

hili ni muhimu katika kufanya makadirio ya pembejeo zikiwemo mbegu/miche na viuatilifu.

iv. Kuwaagizia Wakulima mabomba maalum ya kupulizia viuatilifu (*Motorized sprayers*) na kuwauzia kwa bei ya ruzuku ili kurahisisha zoezi la upuliziaji wa viuatilifu kwa urahisi na kulinda afya zao.

v. Kuhakikisha zao hili linauzwa kwa njia ya Mnada katika Halmashauri za Kilosa na Gairo wanafanya minada kupitia Chama Kikuu KICU na Mvomero na Morogoro kupitia Chama kikuu MOFACU kama inavyofanyika katika Halmashauri za Malinyi, Ulanga, Mlimba na Ifakara Mji kwenye Chama cha UKICU ili kupunguza utoroshwaji wa Korosho ghafi.

### 5.5.7 Mkakati wa kuendeleza zao la Korosho

#### a. Kuendelea Kutoa Elimu juu ya zao la Korosho.

Viongozi na Wataalamu kuanzia ngazi ya Mkoa hadi Vijiji kwa kushirikiana na Wataalam kutoka Bodi ya Korosho waliopo katika ngazi ya Kanda, Mkoa na Halmashauri za Wilaya hufanya uhamasishaji kwa Wakulima kupitia mikutano ya hadhara na vikao mbalimbali. Elimu ya kilimo bora cha Korosho ikiwemo udhibiti wa Visumbufu (Magonjwa na Wadudu) hutolewa na Wataalam wa Kilimo. Radio za jamii kwa Halmashauri zenye vituo vya Radio kama Gairo, Ulanga na Kilosa hutumika katika kuhamasisha na kuwaelimisha Wakulima kuhusiana na zao la korosho. Aidha katika siku za karibuni Watafiti kutoka TARI Naliendele waliendesha mafunzo juu ya Agronomia na udhibiti wa visumbufu vya zao la Korosho kwa Wakulima na wataalam wa Kilimo katika Halmashauri zinazolima zao hilo. Wakulima wengi walipatiwa mafunzo hayo.

#### b. Uhamasishaji wa Wakulima

Mkoa utaendelea kuhamasisha Wakulima juu ya umuhimu wa kulima korosho kama zao la kudumu la biashara na kutunza mazingira kwa kufanya mikutano katika vijiji kwa kushirikisha viongozi wote kuanzia ngazi ya Mkoa hadi vitongoji pamoja na kutumia Radio za jamii katika Halmashauri zenye Radio.

#### c. Usambazaji wa Viuatilifu

Kuendelea kusambaza viuatilifu vya ruzuku toka Bodi ya Korosho na kutoa elimu ya matumizi sahihi ya viuatilifu. Katika kipindi cha msimu wa 2023/2024 Mkoa ulpokea viuatilifu vya korosho kiasi cha Lita 8,213 ikiwa ni **Joninja** Lita 1,600, **Bravia** 5,406

na **Bacox** 1,200 kutoka Bodi ya Korosho tarehe 05 Agosti, 2023. Viuatilifu hivyo vimesambazwa katika Halmashauri zinazolima zao la Korosho kadiri ya utaratibu uliyoelekezwa na Bodi ya Korosho. Hali kadhalika katika msimu huu wa kilimo 2025/2026 Mkoa umepokea Viuatilifu vya Korosho kutoka Bodi ya Korosho na kuvisambaza kwenye Halmashauri zote za Mkoa kwa kuzingatia uzalishaji. Viuatilifu hivyo ni ***Indazole Lita 2,962*** na ***Tegata Lita 1,812*** Jumla **Lita 4,774.**

**d. Kuanzisha na Kuimarisha Vyama vya Ushirika wa Wakulima na kuwashauri ili waweze kujiunga na kufugua akaunti kwenye Benki mpya ya Ushirika**

Ili kusimamia uuzwaji wa korosho za Wakulima Mkoa Umeweka mkakati wa kuanzisha na kuimarisha vyama Ushirika vya msingi vya mazao ya Kilimo (AMCOs) na kuendelea kuimarisha Chama Kikuu cha Ushirika cha Kilombero na Ulanga UKICU ili kusimamia uuzajii wa korosho kupitia mfumo unaotambulika wa stakabadhi ghalani.

**e. Kukuza Soko la Ndani la Korosho**

Ili kupata soko kwa Korosho zinazozalishwa Mkoani Wakulima wanahamasishwa kubangua Korosho kwa kuanzisha vikundi vya wabanguaji au Mkulima mmoja mmoja ili ziweze kupata soko la ndani ya Halmashauri na Mkoa kwa ujumla. Juhudi pia zinafanyika katika kuhamasisha wawekezaji kuanzisha viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya kubangua korosho.

**f. Usimamizi na Ufuatiliaji**

Ili kuwa na matokeo mazuri utafanyika usimamizi, na ufuatiliaji wa karibu wa Kilimo cha Korosho katika vijiji vinavyolima zao hilo ili kuweza kuzibaini Changamoto zinazowakabili Wakulima katika kutekeleza Shughuli zao za kila siku na kuzipatia ufumbuzi unaostahiki.

**g. Uzalishaji wa miche ya Korosho**

Kuendelea kuzalisha miche ya Korosho na kuisambaza kwa wakulima ili kupanua maeneo ya kilimo. Kwa msimu wa 2025/2026 Mkoa unapanga kuzalisha miche 450,000 na kuisambaza kwa wakulima.

### 5.5.8 Hitimisho

Tunaishukuru Serikali ya Muungano wa Tanzania kupitia Bodi ya Korosho kwa kuendelea kulisimamia zao la korosho kwa kutoa viuatilifu vya Ruzuku na usambazaji wa mbegu za Korosho. Motokeo ya kuongezeka kwa uzalishaji yametokana na nguvu kubwa inayowekwa na Serikali ya kuwainua wakulima.

## 5.6 TAARIFA YA MKOA WA SINGIDA

### 5.6.1 Utangulizi

Korosho ni miongoni mwa mazao ya kimkakati ya biashara yanayolimwa katika Mkoa wa Singida na linalo waongezea wakulima kipato na kuinua uchumi wa Mkoa. Mazao mengine ya biashara ni pamoja na Alizeti, Pamba, Vitunguu na Dengu/Choroko. Mkoa wa Singida una jumla ya Ekari 62,876 za Mashamba ya pamoja (Block Farming) za korosho kwa mchanganuo wa Halmashauri ya Manyoni Ekari 35,000, Itigi Ekari 26,676 Ikungi Ekari 1000 na Mkalama Ekari, 200. Kati ya eneo hilo jumla ya ekari 32,158.4 zimelimwa korosho, ambapo hadi kufikia msimu wa 2025/2026 korosho zipo katika hatua mbali mbali za ukuaji.

### 5.6.2 Hali ya uzalishaji wa zao la korosho msimu wa 2024/2025

Msimu wa kilimo 2024/2025 jumla ya tani 378.2 za korosho zilivunwa kwenye ekari 9200 (Masigati ekari 7000, Mkwese ekari 2000 na Gumanga ekari 200) kati ya lengo la kuvuna tani 1200. Kati ya mavuno hayo tani 288.7 zilivunwa kwenye mashamba ya pamoja ya vijiji vya Masigati tani 72.3 na Mkwese vilivyopo Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni na tani 17.2 zilivunwa katika shamba la kijiji cha Gumanga Wilayani Mkalama. Aidha kati ya korosho zilizozalishwa jumla ya tani 39.5 ziliuzwa kupitia mnada na zilizobaki zilibanguliwa na wabanguaji wadogo wadogo waliopo na wenye viwanda 2 vya kubangua korosho vilivyoanzishwa Wilayani Manyoni.

### 5.6.3 Mpango /Makadirio ya uzalishaji kihalmashauri ifikapo 2029/2030

Katika msimu wa 2029/2030 jumla ya tani **7582.6** zinatarajiwa kuvunwa katika mashamba ya pamoja na ya wkulima wadogo wadogo waliopo Mkoani Singida kwa mchanganuo wa kila Halmashauri ulioonyeshwa kwenye jedwali hapo chini;

**Mpango /Makadirio ya uzalishaji kihalmashauri msimu wa 2025/2026 hadi 2029/2030**

| Na. | | Mpango/ Makadirio ya uzalishaji (Tani) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Halmashauri** | **2025/2026** | **2026/2027** | **2027/2028** | **2028/2029** | **2029/2030** |
| 1 | Iramba | 33 | 37 | 41 | 46 | 50 |
| 2 | Mkalama | 18 | 26 | 31 | 38 | 46 |
| 3 | Manyoni | 975 | 2560 | 4450 | 6340 | 7324 |
| 4 | Ikungi | 17 | 21 | 32 | 37.2 | 48.2 |
| 5 | Itigi | 32 | 38 | 40.2 | 43.1 | 49 |
| 6 | Manispaa MC | 14.5 | 16.7 | 25.8 | 30.7 | 47.2 |
| 7 | Singida | 7.5 | 8 | 10 | 13.1 | 18.2 |
| **Jumla** | | **1097** | **2706.7** | **4630** | **6548.1** | **7582.6** |

### 5.6.4 Mpango na Upatikanaji wa mbegu/ miche bora ya korosho

Katika msimu wa 2025/2026 Mkoa umebaini mahitaji ya mbegu na miche bora ya korosho kwa kila Halmashauri kulingana na ekari zitakazolimwa na kuwasilisha Bodi ya Korosho kwa ajili ya kufanikisha upatikanaji wa mbegu hizo. Aidha Halmashauri zinahimizwa kutenga bajeti za ununuzi wa mbegu bora za korosho kutoka taasisi ya TARI Naliendele na kuzalisha miche na kugawa kwa wakulima. Mchanganuo wa mahitaji ya mbegu/miche ya korosho ni kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini.

**Mahitaji ya mbegu na miche bora ya korosho mkoa wa singida msimu wa 2025/2026**

| Halmashauri | Mahitaji | | Ukubwa wa maeneo yaliyo wazi yanayofaa kuanzisha mashamba ya ‘’ Blockfarming’’ ( Ekari) |
|---|---|---|---|
| | Mbegu (Kg) | Idadi ya miche | |
| Iramba DC | 1000 | 105,000 | 3,500 |
| Mkalama DC | 0 | 0 | Hakuna maeneo yaliyo wazi |
| Singida DC | 1,500 | 110,000 | 6,000 |
| Singida MC | 100 | 12,000 | 400 |
| Ikungi DC | 2,000 | 140,000 | 8,000 |
| Itigi DC | 700 | 84,000 | 2,800 |
| Manyoni DC | 3,000 | 260,000 | 12,000 |
| **Jumla** | **8,300** | **711,000** | **32,700** |

### 5.6.5 Hali ya ubanguaji wa zao la korosho msimu wa 2024/20225

Tani 378.2 za korosho ghafi zilizozalishwa na wakulima zimebanguliwa katika viwanda vidogo viwili (2) vya kubangua korosho vilivyoanzishwa na watu binafsi katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni na wabanguaji wadogo wadogo waliopo Mkoa wa Sinmgida. Aidha shughuli za ubanguaji kwa sehemu kubwa zinafanywa na wakulima wenyewe waliopo ndani ya Mkoa wa Singida, hivyo uhamasishaji unaendelea kufanyika ili wakulima waweze kubangua korosho zao kwenye viiwanda vilivyopo.

### 5.6.6 Makadirio ya ubanguaji kihalmashauri msimu wa 2025/2026 hadi kufikia 2029/2030

Mkoa wa Singida unakadiria kuzalisha tani **1516.5** za kurosho zilizobanguliwa ifikapo 2029/2030 kwa mchanganuo ulioonyeshwa kwenye jedwali hapo chini.

**Mpango/Makadirio ya ubanguaji misimu ya 2025/2026 hadi 2029/2030**

| Na | | Mpango/ Makadirio ya ubanguaji (Tani) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **HALMASHAURI** | **2025/2026** | **2026/2027** | **2027/2028** | **2028/2029** | **2029/2030** |
| 1 | Iramba | 6.6 | 7.4 | 8.2 | 9.2 | 10 |
| 2 | Mkalama | 3.6 | 5.2 | 6.2 | 7.6 | 9.2 |
| 3 | Manyoni | 195 | 512 | 890 | 1268 | 1464.8 |
| 4 | Ikungi | 3.4 | 4.2 | 6.4 | 7.44 | 9.64 |
| 5 | Itigi | 6.4 | 7.6 | 8.04 | 8.62 | 9.8 |
| 6 | Manispaa MC | 2.9 | 3.34 | 5.16 | 6.14 | 9.44 |
| 7 | Singida | 1.5 | 1.6 | 2 | 2.62 | 3.64 |
| **Jumla** | | **219.4** | **541.34** | **926** | **1309.6** | **1516.5** |

### 5.6.7 Hali ya huduma za uigani na mafunzo

Hali ya huduma za ugani ni ya kuridhisha kwakuwa Bodi ya korosho imeajiri maafisa ugani wanaoshirikiana na maafisa ugani wa Halmashauri kutoa elimu ya kilimo bora cha korosho kwenye mashamba ya pamoja yaliyoanzishwa na ya wakulima wadogo wadogo. Aidha maafisa ugani wamewzeshwa vitendeakazi (Pikipiki, vishikwambi na vifaa vya kupima afya ya udongo) vinavyowasaidia kutoa huduma za ugani kwa urahisi. Katika msimu wa 2025/2026 Mkoa utaendelea kuwasiliana na Bodi ya Korosho kwa ushauri wa kutoa mafunzo rejea kwa maafisa ugani juu ya matumizi sahihi ya viuatilifu vya zao la korosho, upuliziaji na kanuni za kilimo bora cha zao hilo ili kuweza kufanikisha ongezeko la uzalishaji.

### 5.6.8 Changamoto zinazokabili uendelezaji wa zao la korosho

i. Baadhi ya wakulima kutokuhudumia mashamba na kutokupulizia madawa ya huthibiti magonjwa na wadudu waharibifu wa zao la korosho.
ii. Ukosefu wa mafunzo rejea kwa Maafisa Ugani waliopo kwenye maeneo yanayolima zao la korosho.
iii. Ukosefu wa fedha za uratibu na ufuatiliaji wa zao la korosho kwa ngazi ya Mkoa na Halmashauri.
iv. Bei kubwa ya viuatilifu vya kuthibiti magonjwa na wadudu waharibifu wa zao la korosho

### 5.6.9 Utatuzi wa changamoto zinazokabili uendelezaji wa zao la korosho

i. Tunahamasisha wakulima juu ya umuhimu wa kuhudumia mashamba ya korosho, upuliziaji na matumizi ya miche bora ya korosho.
ii. Mkoa unaendelea kuwasiliana na Bodi ya korosho ili mafunzo rejea yaweze kutolewa kwa Maafisa Ugani waliopo kwenye maeneo ya uzalishaji wa korosho.
iii. Mkoa unaishauri Bodi ya korosho kutenga fedha kwa ajili ya uratibu na ufuatiliaji wa zao la korosho.
iv. Mkoa unaishauri Bodi ya korosho kuleta pembejeo za korosho zenye ruzuku na Halmashauri kufanya usimamizi wa matumizi ya pembejeo aza korosho.
v. Halmashauri zinasisitizwa kuviwezesha vikundi vya vijana,
vi. wanawake na watu wenye ulemavu kuanzisha viwanda vidogo vya
vii. ubanguaji kwa kutumia mikopo ya 10% itokanayo na mapato ya ndani, pia Mkoa unaendelea kushawishi Wawekezaji kuja kuanzisha viwanda vya ubanguaji ndani ya Mkoa.

## 5.7: TAARIFA YA MKOA WA TABORA

### 5.7.1. Utangulizi

Kilimo cha Korosho Mkoani Tabora kilianza rasmi katika msimu wa kilimo wa mwaka 2017/2018. Hii ni baada ya watafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Naliendele, kutembelea wilaya za Mkoa na kujiridhisha kuwa zao hili linaweza kustawi vizuri. Ilionekana kuwa zao la korosho linaweza kustawi katika Halmashauri zote za Mkoa wa Tabora. Ni sehemu chache tu katika wilaya ya Igunga ambazo haziwezi kustawisha zao hili. Sehemu hizo ni zenye udongo mweusi ambao unaofaa kwa kilimo cha pamba. Bodi ya Korosho Tanzania iliweza kuuingiza Mkoa wa Tabora katika Mpango wa Kilimo cha korosho na hivyo ilitoa pembejeo kwa ajili ya kuanzisha kilimo hicho.

### 5.7.2. Uzalishaji msimu 2024/2025 na mpango wa uzalishaji ifikapo msimu 2029/2030

#### 5.7.2.1 Uzalishaji msimu 2024/2025

Katika msimu wa 2024/2025, jumla ya kilo 265,607 za korosho zilizalishwa katika eneo lenye jumla ya ekari 10,472. Uzalishaji kiwilya ni kama inavyoonekana katika Jedwali hapo chini;

**Mavuno ya korosho msimu 2024/2025**

| Na. | Halmashauri | Eneo (Ekari) | Kiasi kilichovunwa (kg) |
|---|---|---|---|
| 1 | Nzega TC | 96 | 4,500 |
| 2 | Nzega DC | 614 | 2,800 |
| 3 | Igunga | 195 | 21,796 |
| 4 | Kaliua | 2,125 | 59,500 |
| 5 | Urambo | 224 | 3,875 |
| 6 | Sikonge | 3,834 | 75,000 |
| 7 | Tabora MC | 1,080 | 31,320 |
| 8 | Uyui | 2,304 | 66,816 |
| | **Jumla** | **10,472** | **265,607** |

***Chanzo: Halmashauri za Mkoa wa Tabora***

### 5.7.3. Makadirio ya uzalishaji kiwilaya misimu ya 2025/2026 hadi 2029/2030

Kilimo cha korosho kilianza mwaka 2017/2018. Baadhi ya mikorosho ambayo haikubebeshwa ilionekana kutoa maua katika muda wa mwaka mmoja tangu kupandwa kwake. Mavuno yalianza kupatikana msimu 2020/2021 japokuwa ni kidogo. Katika msimu 2024/2025, jumla ya kilo 265,607 zilizalishwa. Makadilio ya uzalishaji kiwilaya kuanzia msimu 2025/2026 hadi 2029/2030 yamaeoneshwa kwenye Jedwali hapo chini.

**Makadilio ya uzalishaji (Kg) kiwilaya kuanzia msimu 2025/2026 hadi 2029/2030**

| Halmashauri/Msimu | 2025/2026 | 2026/2027 | 2027/2028 | 2028/2029 | 2029/2030 |
|---|---|---|---|---|---|
| Igunga | 43,592 | 54,490 | 81,735 | 108,980 | 136,225 |
| Kaliua | 959,850 | 994,400 | 1,190,000 | 1,204,000 | 1,232,000 |
| Nzega DC | 3,080 | 3,400 | 3,740 | 4,100 | 4,500 |
| Nzega Mjini | 7,500 | 15,000 | 25,000 | 40,000 | 61,000 |
| Sikonge | 193,000 | 289,500 | 965,000 | 1,447,500 | 1,930,000 |
| Tabora MC | 52,650 | 113,400 | 452,250 | 791,100 | 1,384,000 |
| Urambo | 20,375 | 93,520 | 208,600 | 580,000 | 1,612,600 |
| Uyui | 332,370 | 345,870 | 517,210 | 1,912,545 | 2,860,000 |
| **Jumla** | **1,612,417** | **1,909,580** | **3,443,535** | **6,088,225** | **9,220,325** |

***Chanzo: Halmashauri za Mkoa wa Tabora***

### 5.7.4. Mpango wa upatikanaji wa mbegu bora ya korosho

Upatikanaji wa mbegu bora za korosho ni hatua muhimu katika kuongeza uzalishaji na kipato kwa mkulima. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Halmashauri ya Wilaya ya Urambo imetenga fedha kiasi cha shilingi 1,160,000 kwa ajili ya kununulia mbegu bora na kusambaza miche kwa wakulima.

### 5.7.5. Ubanguaji msimu 2024/2025 na mpango wa ubanguaji ifikapo msimu 2029/2030

#### 5.7.5.1 Ubanguaji msimu 2024/2025

Sehemu kubwa ya korosho iliyopatikana katika msimu wa 2024/2025 ilipelekwa Wilayani Manyoni kwa ajili ya kubanguliwa. Wakulima wa Chama cha Ushirika cha Msingi cha Korosho (Korosho AMCOS) walipatiwa eneo la kukusanyia korosho ili ziuzwe kwa pamoja.

#### 5.7.5.2 Mpango wa Ubanguaji kiwilaya misimu ya 2025/2026 hadi 2029/2030

Halmashauri za Mkoa wa Tabora zimeweka mikakati ya kuwawezesha wakulima kupata mashine za kubangulia korosho. Katika wilaya ya Urambo, utaratibu wa kuanzisha AMCOS moja ya korosho unaendelea. AMCOS hii inatarajiwa kuwezeshwa kununua mashine ili korosho zote zibanguliwe Wilayani Urambo. Inatarajiwa kuwa mashine hii itatumika kubangua korosho za wilaya zilizoko jirani na Urambo. Halmashauri ya Mji wa Nzega kwa kushirikiana na Bodi ya korosho Tanzania na chama cha msingi cha korosho inaendelea kutoa elimu ya kanuni za kilimo bora cha korosho kwa lengo la kuimarisha uzalishaji na tija kwa wakulima ili kuvutia wadau wa tasnia ya korosho kuwekeza kwenye miundombinu ya uchakataji na usindikaji wa zao hilo ikiwemo upatikanaji wa mashine za kubangua korosho ili kuongeza thamani yake kufikia msimu wa 2029/2030.

### 5.7.6. Huduma za ugani na mafunzo

Mkoa una maafisa ugani wapatao 290. Kati ya hao, Maafisa ugani 76 wamepatiwa mafunzo ya kilimo cha korosho na wataalamu kutoka TARI Naliendele. Wataalamu hawa wanaendelea kutoa huduma za ugani kwa wakulima wa korosho. Mkoa unatarajia kutoa mafunzo kwa maafisa ugani wengine kwa kutumia kituo cha kuzalisha mbegu kilichoko Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Tumbi. Maafisa ugani hawa wataendelea kuhudumia wakulima. Mamlaka za Serikali za

Mitaa za Mkoa wa Tabora zimetenga fedha kwa ajili ya huduma za ugani kwa mazao yote likiwemo zao la korosho.

### 5.7.7. Changamoto zinazokabili shughuli za uendelezaji wa zao la korosho na mapendekezo ya utatuzi wake

Changamoto zinazokabili uendelezaji wa zao korosho katika Mkoa wa Tabora ni:-

i. Upatikanaji wa mbegu
ii. Mbegu zinapatikana mbali sana na hivyo kuongeza gharama za uzalishaji wa miche ya korosho.
iii. Upungufu wa maafisa ugani na elimu ndogo ya kilimo cha korosho.
iv. Idadi ya wataalamu wa ugani waliopo ni ndogo ikilinganishwa na ukubwa wa maeneo yanayotakiwa kupata huduma. Kwa sasa mkoa una maafisa ugani 290 kuanzia ngazi ya Mkoa hadi wilaya ambao wanatakiwa kuhudumia Halmashauri 8, Kata 206 na vijiji 724.
v. Gharama kubwa na kutokupatikana kwa baadhi ya viuatilifu
vi. Ugonjwa wa ubwiri unga umeonekana kushambulia mikorosho. Viuatilifu vilivyopendekezwa na watafiti kuudhibiti ugonjwa huu havipatikani kwa wingi. Aina chache zinazopatikana zinauzwa kwa bei kubwa. Aidha, viuatilifu vyenye ruzuku ya Serikali vinavyotolewa na Bodi ya Korosho kwa wakulima bila malipo havitoshelezi mahitaji.
vii. Mabadiliko ya viongozi wa kisiasa katika ngazi ya Mkoa
viii. Mkoa umekuwa na mabadiliko ya mara kwa mara ya viongozi katika ngazi ya Mkoa ambapo kila kiongozi anakuja na kipaumbele chake. Mara nyingine viongozi hao wamekuwa wakizuia utekelezaji wa vipaumbele vilivyokutwa.

### 5.7.8. Mapendekezo ya utatuzi

Hatua zifuatazo zinachukuliwa ili kukabiliana na changamoto hizo

i. Mkoa unahimiza Halmashauri kuagiza mbegu kwa pamoja ili kupunguza gharama za usafirishaji na idadi ya wafuatiliaji.
ii. Mkoa unazihimiza Halmashauri kutafuta uwezekano wa kulima mashamba ya pamoja (*Block Farming*) ili wataalamu wachache waliopo waweze kuwahudumia wakulima kwa pamoja. Hadi sasa jumla ya ekari 15,157 za kilimo cha pamoja zimetengwa katika kijiji cha Karangasi wilayani Uyui.

iii. Mkoa unaendelea kuzielekeza halmashauri kuomba vibali vya ajira na kutenga bajeti kila mwaka.
iv. Ili kupunguza gharama na kuimarisha upatikaji wa pembejeo. Mkoa umeendelea kuhamasisha wakulima kuanzisha vyama vya ushirika vya msingi katika maeneo ambayo kimeanzishwa kilimo cha korosho.
v. Halmashauri za Mkoa wa Tabora zimetenga katika bajeti ya mapato yake ndani fedha za kusaidia kutoa mafunzo ya kilimo bora cha korosho.

#### 5.7.9. Hitimisho

Zao la korosho linafanya vizuri katika maeneo mengi ya Mkoa wa Tabora pamoja na kuwepo kwa changamoto za kitalaam. Korosho zilizobanguliwa zilionekana kuwa zenye ubora wa kuridhisha. Mkoa unaendelea kuhamasisha kilimo cha zao la korosho ili wakulima waweze kuwa na zao la kudumu.

## 5.8 TAARIFA YA MKOA WA NJOMBE

### 5.8.1. Utangulizi

Zao la korosho ni miongoni mwa mazao ya kimkakati yanayolimwa ndani ya Mkoa wa Njombe katika Halmashauri tatu (3) ambazo ni Ludewa, Makete na Wanging'ombe. Zao hili linalimwa zaidi katika Wilaya ya Ludewa ikilinganishwa na Wilaya nyingine. Mazao mengine ya biashara yanayolimwa katika Mkoa wa Njombe ni Parachichi, Chai, Kahawa, Viazi mviringo, Apple, Nyanya, Ngano, Mahindi, na Mazao jamii ya Mikunde.

### 5.8.2. Uzalishaji wa msimu 2024/2025 na mpango wa uzalishaji hadi msimu wa 2026/2027

#### 5.8.2.1 Uzalishaji msimu 2024/2025.

Katika msimu wa 2024/2025 uzalishaji wa zao la Korosho ulikua ni tani **103.962,** jumla ya ekari 1,934 zilivunwa. Ambapo jumla ekari 221 (Ludewa) za korosho zimepandwa na uhamasishaji unaendelea katika maeneo mengine.

#### 5.8.2.2 Mpango/makadirio ya uzalishaji kiwilaya msimu 2025/2026,2026/2027, 2027/2028,2028/2029 na 2029/2030

**Mpango/makadirio ya uzalishaji msimu 2024/2025-2029/2030**

| **Ludewa** | **Malengo/Makadirio** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Msimu | 2025/2026 | 2026/2027 | 2027/2028 | 2028/2029 | 2029/2030 |
| Uzalishaji | 130tan | 170tan | 200tan | 250tan | 300tan |

**Mpango/makadirio ya uzalishaji msimu 2024/2025-2029/2030**

| **Makete** | **Malengo/Makadirio** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Msimu | 2025/2026 | 2026/2027 | 2027/2028 | 2028/2029 | 2029/2030 |
| Uzalishaji | 0.48tan | 0.52tan | 0.7tan | 1.2tan | 1.68tan |

M**pango/makadirio ya uzalishaji msimu 2024/2025-2029/2030**

| **Wanging'ombe** | **Malengo/Makadirio** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Msimu | 2025/2026 | 2026/2027 | 2027/2028 | 2028/2029 | 2029/2030 |
| Uzalishaji | 4.5tan | 6tan | 8tan | 10.5tan | 13tan |

### 5.8.3. Mpango wa upatikanaji wa mbegu na miche bora ya Korosho.

Mpango wa upatikanaji wa mbegu bora na miche bora ya Korosho, Halmashauri ya Ludewa inauhitaji wa mbegu bora kilo 700. Uzalishaji wa miche bora ya korosho Halmshauri inatarajia kuzalisha miche 50400 ya mbegu bora za Korosho ambayo itagawiwa kwa wakulima walioandaa mashamba yao.Tunatarajia kugawa miche hiyo kwa wakulima wa kata za Masasi,Luilo,Mkomang'ombe,Ilela,Manda na Ruhuhu wenye jumla ya ekari 1200

**Mpango/makadirio ya upatikanaji wa mbegu bora msimu 2024/2025-2026/2027**

| **Ludewa** | **Malengo/ Makadirio** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Msimu** | **2024/2025** | | **2025/2026** | | **2026/2027** | |
| Kiasi cha mbegu na ekari | Kiasi(kg) | ekari | Kiasi(kg) | ekari | Kiasi(kg) | ekari |
| | 700 | 1200 | 800 | 1400 | 900 | 1700 |

### 5.8.4. Ubanguaji wa msimu 2024/2025 na mpango wa ubanguaji ifikapo msimu 2026/2027.

#### 5.8.4.1 Ubanguaji msimu 2024/2025

Msimu 2024/2025 hakuna korosho zilizobanguliwa ndani ya Mkoa

#### 5.8.4.2 Mpango/makadirio ya ubanguaji kiwilaya ya msimu 2025/2026 hadi 2029/2030

Mpango wa ubanguaji uliopo ni kuhamasisha makapuni ya ubanguaji kuwekeza kwenye maeneo yenye uzalishaji mkubwa hasa Wilaya ya Ludewa katika kata ya Masasi na Luilo kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji wa zao la Korosho. Pia kuhamasisha Vyama vya Ushirika na vikundi kubangua/kusindika zao la Korosho na kuviunganisha kupata mikopo ya kutoka Taasisi za kifedha na mikopo ya Halmashauri kwa vikundi vitakavyokua tayari kuanza ubanguaji/usindikaji msimu 2025/2026.

**Mpango wa ubanguaji 2024/2025-2029/2030**

| **Ludewa** | **Makadirio ya Ubanguaji** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Msimu** | **2024/2025** | **2025/2026** | **2026/2027** | **2027/2028** | **2028/2029** | **2029/2030** |
| **Luilo AMCOS** | 0 | 30,000kg | 65,000kg | 100,000kg | 130,000kg | 150,000kg |
| **Umoja ni nguvu Amcos** | 0 | 20,000kg | 35,000kg | 50,000kg | 70,000kg | 100,000kg |

### 5.8.5. Huduma za ugani na mafunzo zilizotolewa

i. Elimu ya kilimo bora cha korosho kuanzia maandalizi ya miche, upandaji mpaka uuzaji.
ii. Elimu ya uthibiti magonjwa na wadudu wanaoathiri zao la Korosho.
iii. Elimu ya matumizi sahihi ya viatilifu kwenye zao la Korosho.

### 5.8.6. Changamoto zinazokabili shughuli za uendashaji wa zao la Korosho

i. Kituo cha utafiti TARI NALIENDELE kutofanya utafiti wa zao la Korosho kwa kipindi kirefu.
ii. Maafisa ugani wa maeneo ya uzalishaji wa korosho kutokua na mafunzo kwa kipindi kirefu hali inayofanya kua na mbinu zilezile kila msimu na wengine kutokua na elimu ya uzalishaji wa zao la Korosho kabisa kutokana na asili ya vyuo walivyojifunza.
iii. Ucheleweshwaji wa viuatilifu
iv. Vyama vya ushirika kusafirisha korosho umbali mrefu kufika mnadani unaosababisha ongezeko kubwa la bei ya usafirishaji.
v. Teknolojia hafifu ya ubangauaji

### 5.8.7. Mapendekezo ya utatuzi

i. Kituo cha utafiti wafike kwenye eneo letu na kufanya utafiti ili wakulima waweze kuongeza uzalishaji.
ii. Wadau wanaohusika na mafunzo wafike kwa Wakulima na watoe mafunzo ya kilimo bora cha zao la Korosho kulingana na uhalisia wa eneo.
iii. Bodi wahakikishe wakulima wanapata pembejeo kwa wakati iliziweze kuwasaidia kwenye msimu husika.
iv. Kuomba stakakabdhi gharani kufanya minada katika maeneo ya Halmashauri kupunguza gharama ya usafirishaji kwa wakulima.

### 5.8.8. Mpango mkakati wa kuendeleza zao la Korosho hadi ifikapo 2029/2030

i. Kuongeza uzalishaji wa miche bora na mbegu kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho na kituo cha utafiti Tari-Naliendele.
ii. Kuongeza eneo la kilimo kutoka ekari 1092 hadi 2700
iii. Kuongeza uzalishaji kutoka kilo2-5 kwa mti hadi kilo 10-20 kwa mti
iv. Kuhamasisha kilimo cha zao la Korosho na kuhudumia/kutunza mikorosho iliyopo

### 5.8.9. Hitimisho

Mkoa unawashukuru wadau wote wanaofanya kazi na wakulima wa zao la Korosho na itaendelea kutoa ushirikiano wowote katika kuhakikisha malengo ya Halmashauri zinazolima zao la Korosho yanatimia. Aidha Mkoa utaendelea kuhamasisha kilimo cha zao la Korosho katika maeneo mengine ili kuongeza uzalishaji. Pia Mkoa unawakaribisha wawekezaji kwa ajili ya shughuli za kilimo na viwanda.

## 5.9 TAARIFA YA MKOA WA MBEYA

### 5.9.1 Utangulizi

Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa Mikoa inayozalisha zao la korosho nchini, Halmashauri ambazo ziko katika mpango wa kuendeleza zao la Korosho kwa Mkoa wa Mbeya ni Chunya, Mbarali na Kyela. Hali ya hewa katika Halmashauri hizo hustawisha vizuri zao la korosho pia katika Halmashauri za Chunya na Mbarali kuna maeneo ya kutosha yanayoshawishi uwekezaji mkubwa wa kilimo cha korosho hususani uanzishaji wa mashamba ya kitalu kama vile **Block farming**. Aidha Jumla

ya ekari 1000 zimetengwa katika Halmashauri ya chunya kwa ajili ya uanzishaji wa mashamba ya pamoja kati ya hizo ekari 200 tayari zimepandwa korosho.

### 5.9.2 Uzalishaji msimu wa 2024/2025 na Makadirio ya Uzalishaji hadi 2029/2030

Jumla ya eneo la Hekta 14,321 limepandwa miti ya korosho ipatayo 1,036,374 na kwa msimu wa kilimo wa 2017 hadi 2018 ndio msimu ambao kulikuwa na kampeni ya kupanda miti hiyo katika halmashauri za chunya na Mbarali Hivyo uzalishaji unaendela kuongezeka kadiri miti hiyo inavyoendelea kukua na kuhudumiwa vizuri. Katika msimu wa 24/2025 jumla ya **Tani 69.39** za korosho zimezalishwa katika Mkoa wa Mbeya. Mchanganuo wa uzalishaji kwa kila wilaya umeoneshwa katika jedwali hapo chini.

**Uzalishaji wa Korosho msimu wa 2024/2025**

| | | **KYELA** | **MBARALI** | **CHUNYA** | **JUMLA** |
|---|---|---|---|---|---|
| **Na** | **Msimu** | **Kiasi (Tani)** | **Kiasi Tan** | **Kiasi Tani** | |
| 1. | 2024/2025 | 58 | 8.753 | 2.640 | **69.39** |

**Makadirio ya Uzalishaji.2025/2026 hadi 2029/2030**

| | **KYELA** | | **MBARALI** | **CHUNYA** |
|---|---|---|---|---|
| **Na** | **Msimu** | **Kiasi (Tani)** | **Kiasi Tan** | **Kiasi Tani** |
| 1 | 2025/2026 | 164.44 | 13 | 19.4 |
| 2 | 2026/2027 | 167.76 | 18 | 24.3 |
| 3 | 2027/2028 | 167.76 | 22 | 30 |
| 4 | 2028/2029 | 172.55 | 25 | 38.2 |
| 5 | 2029/2030 | 174.50 | 30 | 47.9 |

### 5.9.3 Mpango wa Upatikanaji wa Mbegu na Miche Bora ya Korosho.

Katika msimu wa 2024/2025 Mkoa wa Mbeya ulipokea mbegu bora za korosho kilo 500 kutoka Bodi ya korosho na kuipatia Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ambapo iligawa kwa wakulima. Aidha Mkoa kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho pamoja na Halmashauri za Chunya, Kyela na Mbarali unatarajia kuzalisha miche bora 350,000 ya Korosho kwa msimu wa 2025/2026 na kugawa bure kwa wakulima.

### 5.9.4 Ubanguaji Msimu wa 2024/2025

Mafunzo ya Ubanguaji wa Korosho yamefanyika kwa wakulima 144 kwa mchanganuo ufuatao, Halmashauri za chunya wakulima 51, Mbarali wakulima 46 na Kyela wakulima 47. Lengo la mafunzo haya ni kuwafundisha wakulima njia bora za

kubangua korosho wanazozalisha ili kuingiza sokoni bidhaa yenye ubora. Aidha Mkoa unalenga kuendelea kutoa elimu ya ubanguaji kwa vikundi vya wakulima, Amcos na mkulima mmoja mmoja katika msimu huu wa 2025/2026.

**Makadirio ya Ubanguaji Kiwilaya msimu wa 2026/2027 hadi 2029/2030**

| | Kyela | | Chunya | Mbarali | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Na** | **Msimu** | **Kiasi (Tani)** | **Kiasi Tani** | **Kiasi Tani** | **JUMLA** |
| 1 | 2026/2027 | 25.2 | 22 | 12 | **59.2** |
| 2 | 2027/2028 | 25.5 | 27 | 17 | **69.5** |
| 3 | 2028/2029 | 26.1 | 33 | 22 | **81.1** |
| 4 | 2029/2030 | 26.6 | 38 | 25 | **89.6** |

#### 5.9.5 Huduma za ugani na Mafunzo

Pamoja na kuboresha Huduma za ugani kwa maafisa ugani hasa wanaoratibu zao la korosho, Mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu yamepangwa kufanyika kwa Halmashauri za Chunya, Kyela na Mbarali ambapo jumla ya wakulima 250 na maafisa ugani 15 wanatarajiwa kufikiwa na mafunzo hayo. Bodi ya korosho imetoa bomba moja kwa Halmashauri ya Chunya la kupulizia korosho, Aidha Mkoa kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho inaendelea kufanya yafuatayo ili kuboresha huduma za ugani.

i. Kutoa elimu ya matumizi sahihi ya viuatilifu kwa wakulima na maafisa ugani juu ya namna bora ya upuliziaji na udhibiti wa wadudu na magonjwa katika zao la korosho.
ii. Kufanya ufuatiliaji na usajili wa mashamba ya korosho na wakulima ili kuhakikisha mbinu bora za kilimo zinafuatwa.
iii. Kuwasaidia wakulima kufanya (layout) pindi wanapo anzisha mashamba mapya ya zao la korosho

#### 5.9.6 Hali ya upatikanaji na usambazaji wa viuatilifu vya korosho

Hali ya upatikanaji wa viuatilifu vya zao la korosho katika Mkoa wa Mbeya kwa msimu wa kilimo 2024/2025 ni kama inavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo:-

**Viuatilifu vya Maji**

| Msimu wa 2024/2025 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **Chunya** | **Kyela** | **Mbarali** | |
| **Na** | **Aina ya Kiuatilifu kudhibiti Magonjwa** | **Kiasi (Lita)** | Kiasi | **Kiasi (Lita)** | **JUMLA** |
| 1 | Indazole 25 SC | 1,239 | 774 | 294 | 2,307 |
| 2 | Pacha | 360 | 240 | 360 | 960 |
| 3 | Tegata | 758 | 474 | 180 | 1412 |
| | **JUMLA** | **2,357** | **1,488** | **834** | **4679** |

**Viuatilifu vya Unga (Sulphur)**

| Msimu wa 2024/2025 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **Chunya** | **Kyela** | **Mbarali** | |
| **Na** | **Aina ya Kiuatilifu kudhibiti Magonjwa** | **Kiasi (Kg)** | Kiasi | **Kiasi (Kg)** | **JUMLA** |
| 1 | Simba Sulphur | 2500 | 1225 | 1250 | 4,975 |

### 5.9.7 Changamoto

Changamoto za zao la korosho katika Mkoa wa Mbeya ni kama ifuatavyo:-

i. Wakulima kukosa soko la uhakika kwa kuwa hakuna wanunuzi wanaojitokeza kutokana na uzalishaji mdogo hali hiyo hupeleleka wakulima kubaki na korosho walizozalisha kwa muda mrefu au kuuza korosho katika soko ambalo sio rasmi.

ii. Elimu ya ubanguaji korosho Kutowafikia wakulima wengi na uchache wa mashine za kisasa za kubangulia korosho kunapelekea kutumia njia za asili na duni za ubanguaji korosho.

iii. Mifugo kuingia katika baadhi ya mashamba ya mikorosho na kuharibu miti hali hii hujitokeza katika Halmashauri za Mbarali na Chunya.

iv. Upungufu wa fedha kwa ajili ya kuendeleza zao la korosho katika Mkoa kwa kuwa hakuna fungu maalumu lilotengwa kwa ajili ya kuendeleza zao la korosho ikiwemo kutoa mafunzo, kwa wakulima na wataalamu, kuwa na vitendea kazi kama mabomba ya kupulizia viuatilifu.

### 5.9.8 Utatuzi wa Changamoto

i. Kuwa na soko la uhakika kwa korosho inayozalishwa katika mkoa wa Mbeya

ii. Bodi ya korosho imewezesha upatikanaji wa pembejeo za korosho za kutosha na kwa wakati pamoja na vifaa vya kupulizia kama vile mabomba.

iii. Kutoa mafunzo kwa wakulima na wajasiriamali juu ya ubanguaji wa korosho na kuwezesha upatikanaji wa viwanda vidogo vya kubangulia korosho kwa Vikundi vya wabanguaji ili Kuongeza thamani ya korosho.
iv. Kuzingatia matumizi bora ya ardhi kwa kutenga maeneo na kuanzisha mashamba ya malisho na malambo ya maji hali ambayo itapunguza mifugo kuharibu mazao ikiwemo korosho.
v. Kuendelea kutoa elimu juu ya udhibiti ya wadudu na matumizi sahihi ya viuatilifu kwa wakulima na maafisa ugani na hatimae kupata korosho ya daraja la kwanza itakayofanya vizuri sokoni.
vi. Kuwa na mfuko maalumu utakaotumika kuendeleza zao la korosho kama ilivyokuwa hapo nyuma na kugawa sawa katika mikoa yote inayolima korosho ili kuendeleza zao hilo.

**5.9.9 Ili kuweza kufikia makadirio ya Uzalishaji hadi ifikapo 2030 jitihada zifuatazo zinafanyika;**

i. Kutoa mafunzo ya mbinu bora za kilimo cha korosho kwa Maafisa Ugani na kwa wakulima kwa kuzingatia kalenda ya zao
ii. Kutoa mafunzo kwa wapuliziaji kuhusu mbinu bora za upuliziaji wa viuatlifu kwenye mikorosho pamoja na Kuhamasisha matumizi ya mabomba ya kisasa ya kupulizia korosho na matumizi sahihi ya viuatilifu hivyo.
iii. Kuendelea kuhamasisha wakulima wa korosho kuunda vikundi vya ubanguaji na kutoa mafunzo kwa vikundi hivyo juu ya mbinu bora za ubanguaji wa korosho
iv. Halmashauri kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania itaendelea kuwasajili wakulima wenye miti ya mikorosho kwa ajili ya kuwekwa kwenye kanzi data ya Bodi ya Korosho na kupatiwa huduma kama vile mafunzo pamoja na pembejeo.
v. Kuanzisha mashamba kitalu ya zao la korosho **(Block farming)** katika Halmashauri ya Mbarali na chunya
vi. Kuunda chama cha ushirika cha wakulima wa korosho katika mkoa wa mbeya.

## 5.10 TAARIFA YA MKOA WA KAGERA

### 5.10.1 Utangulizi:

Mkoa wa Kagera unalo eneo linalofaa kwa kilimo linalokadiriwa kufikia hekta **1,124,19**, kati ya hekta hizo, eneo linalotumika kuzalisha mazao mbalimbali ni hekta **646,410** sawa na **57.5%** ya eneo lote linalofaaa kwa kilimo. Mkoa wa Kagera unayo misimu miwili ya mvua ambayo ni msimu wa vuli na msimu wa masika. Wakulima katika mkoa wa Kagera hutumia misimu yote miwili kuzalisha aina mbalimbali za mazao ya chakula na biashara jambo linalouhakikishia mkoa kuwa na uhakika wa kipato kwa wakulima na uhakika wa chakula kwa mwaka mzima.

Zao la korosho ni moja ya mazao ya biashara yanayozalishwa katika mkoa wa Kagera. Korosho hulimwa katika halmashauri 1 ya Biharamulo kati ya halmshauri **8** za mkoa huu. Eneo linalolimwa korosho ni hekta **352** sawa na asilimia **0.05** ya eneo lote linalotumika kuzalisha mazao mbalimbali katika mkoa. Idadi ya wakulima wa korosho katika mkoa ni **550 wenye jumla ya miche 108,000.**

### 5.10.2 Hali ya uzalishaji wa korosho kwa mwaka 2024/2025 na mpango wa uzalishaji ifikapo mwaka 2029/2030

#### 5.10.2.1 Uzalishaji na Mpango wa 2029/2030

Korosho inazalishwa kwa kiasi kidogo katika mkoa huu wilayani Biharamulo wastani wa tani **5** kwa mwaka. Katika msimu wa 2024/2025, mkoa wa Kagera ulizalisha tani **6.8** za korosho ambazo wakulima waliziuza kwa mchakataji kwa bei ya shilingi **2500/=** hadi **3,000/=** kwa kilo moja.

Mkoa umejiwekea malengo ya kuzalisha korosho kwa miaka mitano kama inavyoonekama kwenye jedwali hapa chini: -

| **Malengo ya uzalishaji wa korosho kwa mwaka (tani)** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **2025/26** | **2026/27** | **2027/28** | **2028/29** | **2029/30** |
| 9.5 | 14.8 | 21.5 | 28.3 | 37.5 |

#### 5.10.2.2 Hali ya uzalishaji na upatikanaji wa mbegu na miche bora ya korosho:

Kituo cha utafiti cha Naliendele kilichopo Mtwara, ndicho chanzo pekee cha mbegu bora za korosho kwa mkoa wa Kagera. Mkoa unae mzalishaji mmoja tu wa miche ya korosho ambae hupata mbegu bora za korosho kutoka TARI Naliendele, huziotesha mbegu hizi na kuwauzia miche wakulima wenzake. Mzalishaji huyu wa miche huagiza kilo **100** za mbegu na kuzalisha miche **10,000** kila mwaka.

### 5.10.3 Hali ya ubanguaji wa korosho kwa mwaka 2025/2026, na mpango wa ubanguaji ifikapo mwaka 2029/2030

#### 5.10.3.1 Hali ya ubanguaji wa korosho kwa mwaka 2025/2026.

Katika msimu wa 2025/2026, mkoa wa Kagera unae mchakataji mmoja tu wa korosho ambae ana mashine ndogo ya kubangua korosho yenye uwezo wa kubangua kilo **50** kwa siku. Mchakataji huyu ndie aliyenunua korosho za msimu wa 2024/2025 tani **6.8** kutoka kwa wakulima. Kwa sasa anaendelea na kazi ya kubangua na kuuza Korosho zilizobanguliwa. Bei ya sasa kwa korosho zilizobanguliwa ni kati ya shilingi **12,000/=** hadi **15,000/=** kwa kilo. Aidha, malengo ya mkoa ya ubanguaji wa korosho kwa miaka mitano ni kama ifuatavyo; -

| Malengo ya ubanguaji wa korosho kwa mwaka (tani) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **2025/26** | **2026/27** | **2027/28** | **2028/29** | **2029/30** |
| 9.5 | 14.8 | 21.5 | 28.3 | 37.5 |

### 5.10.4 Huduma za ugani na mafunzo

Zao la korosho ni zao geni katika mkoa wa Kagera. Kutokana na ugeni huo, wagani wengi katika mkoa wa Kagera hawalifahamu vyema zao hili hivyo kushindwa kutoa huduma za ugani kikamilifu kwa wakulima hao wa korosho.

### 5.10.5 Changamoto na mapendekezo ya utatuzi

i. Uwepo wa magonjwa pamoja na wadudu waharibifu wa korosho.
ii. Maafisa ugani wengi kutolifahamu vyema zao la korosho hivyo kushindwa kutoa huduma za ugani kikamilifu kwa wakulima.
iii. Uzalishaji na upatikanaji mdogo wa miche bora ya korosho kwa wakulima.
iv. Kukosekana kwa mashine za kutosha na zenye uwezo mkubwa wa kubangua korosho.

### 5.10.6 Mapendekezo ya utatuzi wa Changamoto

i. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kagera imeishauri halmashauri ya wilaya ya Biharamulo ambayo ndio halmashauri pekee inayozalisha korosho katika mkoa kuendelea kutenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya mambo yafuatayo; -
   a. Uzalishaji wa miche bora ya korosho
   b. Kutoa mafunzo kwa Maafisa Ugani juu ya uzalishaji wa zao la korosho ili wawe na uwezo wa kuwaelimisha na kuwasimamia vyema wakulima wa zao hili.
   c. Kusaidia upatikanaji wa mashine za kutosha na zenye uwezo mkubwa kwa ajili ya kubangua korosho za wakulima.

ii. Kuhimiza sekta binafsi kuwekeza kikamilifu katika zao hili

### 5.10.7 Hitimisho

Kutokana na mwamuko mkubwa unaoonyeshwa na wakulima wa zao la Korosho katika mkoa wa Kagera hususani wilaya ya Biharamulo, ipo haja kwa Serikali ya Mkoa, Bodi ya Korosho Tanzania na wadau wengine kuongeza nguvu katika kuwekeza kwenye zao hili.

## 5.11 TAARIFA YA MKOA WA KILIMANJARO

Mkoa wa Kilimanjaro ni miongoni mwa mikoa mipya inayolima zao la korosho katika Halmashauri za Same, Mwanga, Rombo na Moshi**.**

### 5.11.1 Halmashauri ya wilaya ya Same

Halmashauri ya Wilaya ya Same ilianza kulima zao la korosho msimu wa kilimo 2017/18, katika maeneo ya tambarare ya Mashariki na tambarare ya magharibi. Maeneo yanayostawi zao hili ni kata za Maore, Kisiwani, Vumari, Mabilioni, Makanya, Njoro, Hedaru, Gavao Saweni, Same, Stesheni, Kisima, Ruvu, Ndungu, Kihurio, Bendera. Mwembe, Bangalala na Kalemawe.

**Uzalishaji 2024/2025.**

| Na. | Ekari zilizolimwa | Mavuno (kg) |
|---|---|---|
| 1. | 32 | 1200 |

#### 5.11.1.1 Mpango wa uzalishaji 2022 hadi 2026.

Halmashauri ya Wilaya ya Same ina mpango wa kuendeleza zao la korosho kutoka ekari 32 msimu 2024/2025 hadi kufikia ekari 150 msimu wa 2029/2030

| **Mwaka** | **2025/26** | **2026/27** | **2027/2028** | **2028/29** | **2029/2030** |
|---|---|---|---|---|---|
| **Ekari** | 50 | 60 | 90 | 100 | 150 |
| **Kilo** | 2,000 | 3,000 | 4,000 | 10,000 | 20,000 |

#### 5.11.1.2 Upatikanaji wa mbegu 2025/26

Halmashauri ya Wilaya ya Same inategemea kupata mbegu kilo 100 kutoka kituo cha utafiti Naliendele, kupitia Bodi ya korosho Tanzania.

#### 5.11.1.3 Ubanguaji wa korosho.

Halmashauri ya Wilaya ya Same haina mashine za kubangulia korosho, katika msimu wa kilimo 2024/2025 wakulima walitumia njia za kienyeji katika kubangua korosho, hivyo tunaomba kupatiwa mashine hizo kuanzia msimu wa kilimo 2025/2026.

#### 5.11.1.4 Mpango wa ubanguaji korosho 2022/23 hadi 2025/26.

| **Mwaka** | **2025/2026** | **2026/2027** | **2027/2028** | **2028/20/29** | **2029/2030** |
|---|---|---|---|---|---|
| **Kilo** | 2000 | 3000 | 4000 | 10,000 | 20,000 |

#### 5.11.1.5 Huduma za ugani na mafunzo.

Huduma za ugani zinatolewa na maafisa ugani waliopo katika kata na vijiji, Maafisa ugani na wakulima walipatiwa mafunzo kutoka kwa wataalam kuhusu kilimo cha zao la korosho Naliendele mwaka 2020. Mafunzo zaidi kwa maafisa ugani na wakulima yanahitajika kwa sababu tangu tuanze kilimo hiki cha zao la korosho Halmashauri ya Wilaya ya Same ilipata mafunzo mara moja kwa muda wa siku mbili tu. Mwaka 2025/2026 Wilaya ya Same inaomba kupatiwa mafunzo ikizingatiwa maafisa ugani wapya hawajapata mafunzo ya zao la korosho.

#### 5.11.1.6 Changamoto.

i. Wanyama waharibifu kama tembo wanaharibu miti ya mikorosho kwa kiasi kikubwa.
ii. Bodi ya korosho kutoleta mbegu na viuatilifu vya zao la korosho.

iii. Maafisa ugani kutopata mafunzo ya mara kwa mara na hivyo kuwafanya kutokuelewa vema zao la korosho.

#### 5.11.1.7 Mapendekezo.

i. Tunaomba kupatiwa elimu ya kilimo cha zao la korosho mara kwa mara ikizingatiwa zao hili ni geni kwetu.
ii. Tunaomba elimu ya ubanguaji wa korosho na mashine za kubangulia korosho.
iii. Tunaomba kupatiwa mashine za kupulizia viuatilifu vya miti ya korosho.
iv. Tunaomba kupatiwa ziara za mafunzo ya zao la korosho kwa maafisa ugani na wakulima.

#### 5.11.1.8 Mikakati ya kuendeleza zao la korosho ifikapo 2029/2030

i. Wilaya ya Same imepanga ifikapo 2029/2030 kuongeza eneo kutoka ekari 32 hadi kufikia ekari 150, hii ni kujumuisha maeneo ambayo yaliathiriwa na tembo kuanza kulima korosho tena.
ii. Kudhibiti tembo ambao wamekuwa kikwazo kikubwa katika eneo la Same.

### 5.11.2 Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga

#### 5.11.2.1 Uzalishaji wa Msimu wa Mwaka 2024 / 2025 na Mpango wa Uzalishaji ifikapo msimu wa Mwaka 2029 / 2030.

i. Uzalishaji wa Msimu wa mwaka 2024 / 2025 – Tani 1.5
ii. Mpango / Makadirio ya Uzalishaji kiwilaya misimu ya :-
    a. 2025 / 2026 – Tani 3
    b. 2026 / 2027 – Tani 7
    c. 2027 / 2028 – Tani 12
    d. 2028 / 2029 – Tani 25
    e. 2029 / 2030 – Tani 50

#### 5.11.2.2 Mpango wa Upatikanaji wa Mbegu na Miche bora ya Korosho

Mwaka 2025 / 2026 Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga kwenye mipango ya bajeti ya mapato ya ndani imepanga kununua mbegu ya Korosho kilo 100 kwaajili ya kuzalisha miche na kuigawa kwa Wakulima pamoja na kumalizia ujenzi wa Kitalu cha kuzalisha miche.

#### 5.11.2.3 Ubanguaji wa msimu wa mwaka 2025 / 2026 na mpango wa ubanguaji ifikapo msimu wa 2029 / 2030.

i. Ubanguaji kwa Msimu wa mwaka 2021 / 2022 – Hakuna
ii. Mpango / Makadrio ya Ubanguaji Kiwilaya Misimu ya :-
   a. 2025 / 2026 – Hakuna
   b. 2026 / 2027 – Hakuna
   c. 2027 / 2028 – Hakuna
   d. 2028 / 2029 – Utafanyika
   e. 2029 / 2030 – Utafanyika

#### 5.11.2.4 Hali ya huduma za ugani na Mafunzo.

Wakulima wameendelea kupata huduma za ugani hususani kuzingatia kanuni bora za kilimo cha Korosho kupitia Maafisa ugani wa Kata na Vijijii wanaotoa huduma katika Maeneo hayo. Aidha Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga katika Mwaka wa fedha 2025/2026 imetenga fedha kwaajili ya kumalizia ujenzi wa Kitalu cha kuzalisha Miche ya Korosho na ununuzi wa Mbegu kwaajili ya kuzalisha Miche na kuigawa kwa Wakulima.

#### 5.11.2.5 Changamoto zinazokabili shughuli za Uendelezaji wa zao la Korosho na Mapendekezo ya utatuzi wake.

| Na. | Changamoto | Mapendekezo ya Utatuzi |
|---|---|---|
| 1. | Uhaba wa fedha za kutosha kuhamasisha zao la Korosho kwani ni jipya katika Wilaya ya Mwanga. | Pamoja na Halmashauri kuendelea kutenga fedha , pia jitihada za kutafuta na kushirikiana na wadau wengine ziendelee ili kuongeza hamasa na uwezeshaji katika zao hili. |
| 2. | Kutoa elimu ya upatikanaji wa viuatilifu vya visumbufu vya zao la Korosho na Soko. | Kwa kuwa ni zao jipya hapa Wilayani kwetu Mwanga nguvu bado inahitajika kutoka kwa wadau mbalimbali. |
| 3. | Mwaka 2024/2025, Bodi ya Korosho iliahidi kuipatia Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga Miche bora ya Korosho Kwaajili ya kuigawa kwa Wakulima lakini ahadi hiyo haikutekelezwa. | Bodi ya korosho kutekeleza ahadi yake, hata hivyo ufuatiliaji wa ahadi hii unaendelea kwa msimu wa mwaka 2025 / 2026 |

| | | |
|---|---|---|
| 4. | Uvamizi wa Tembo wanaharibu Mikorosho | Halmashauri inashirikiana na Taasisi zinazoshughulikia Wanyama pori kufundisha Wakulima namna bora za kukabiliana na Tembo. |

#### 5.11.2.6 Mikakati ya kuendeleza zao la Korosho ifikapo 2029/2030

Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea kuhamasisha Wakulima kuotesha Mikorosho mipya kila Mwaka ili kuongeza uzalishaji na pia kutenga bajeti hususani ya kuzalisha Miche ili iweze kupatikana kwa Wakulima katika Misimu ya kuotesha na kuhamasisha Wawekezaji kuwekeza kilimo cha Korosho Wilayani Mwanga.

### 5.11.3 Halmashauri ya Wilaya ya Rombo

#### 5.11.3.1 Uzalishaji Msimu wa 2024/2025 na mpango wa uzalishaji ifikapo msimu wa 2029/2030

##### 5.11.3.1.1 Uzalishaji Msimu wa 2024/2025:

Kwa sasa hakuna uzalishaji kutokana na miti michache ya korosho iliyopona kushambuliwa na magonjwa ya ukungu na pia miti hiyo bado haijafikia hatua ya uzalishaji.

##### 5.11.3.1.2 Mpango wa makadirio ya uzalishaji kiwilaya misimu wa 2024/2025, 2025/2026, 2026/2027, 2027/2028, 2028/2029 na 2029/2030.

Makadirio ya uzalishaji utategemea sana upatikanaji wa miche mipya, dawa ya sulfur na mafunzo kwa Maafisa ugani pamoja na wakulima ili waweze kuhamasika kuendelea kuotesha mikorosho. Kwa sasa ni vigumu kufanya makadirio ya uzalishaji kwa vile Wilaya ndio inaanza upya uzalishaji wa zao la korosho baada ya zile za awali kutofanya vizuri.

#### 5.11.3.2 Mpango wa upatikanaji wa mbegu

Mbegu zitaendelea kupatikana kutoka Bodi ya Korosho ili vikundi vya wakulima viweze kuzalisha miche mingi iwezekanavyo na kuigawa kwa wakulima wa Ukanda wa Kati na chini.

#### 5.11.3.3 Ubanguaji msimu wa 2025/2026 na mpango wa ubanguaji msimu 2026/2027.

#### 5.11.3.3.1 Ubanguaji Msimu wa 2025/2026:

Hakuna ubanguaji kwa sasa kwa sababu miche michache iliyopona bado ni midogo ndio inaanza kutoa maua.

#### 5.11.3.3.2 Mpango/makadirio ya ubanguaji kiwilaya msimu 2026/2027, 2027/2028, 2028/2029 na 2029/2030.

Hakuna mpango wa ubanguaji korosho kiwilaya msimu wa 2026/2027, 2027/2028, 2028/2029 na 2029/2030. Aidha mpango wa ubanguaji utaanza baada ya miche michache iliyopo kukomaa na miche mingine mipya kupatikana na kuoteshwa kwa wakulima.

#### 5.11.3.4 Huduma za ugani na Mafunzo:

Bodi ya Korosho inatakiwa kuandaa mpango wa mafunzo kwa Maafisa ugani wa Wilaya zinazoanza kulima zao hilo ili wawe na uwezo wa kuwashauri wakulima kulima kwa tija, zao la korosho ambalo kwa sasa ni geni katika Wilaya ya Rombo hasa ikizingatiwa kuwa limekuwa na changamoto nyingi katika majaribio.

#### 5.11.3.5 Changamoto zinazokabili shughuli za uendelezaji wa zao la korosho na mapendekezo ya utatuzi:

| Na | Changamoto | Mapendekezo ya utatuzi |
|---|---|---|
| 1 | Ukosefu wa elimu ya kutosha juu ya zao la korosho kwa Maafisa Ugani | Bodi ya Korosho iandae mpango wa mafuzo kwa maafisa ugani wa Wilaya zinazoanza kulima zao hilo. |
| 2 | Ukosefu wa miche ya korosho pamoja | Bodi ihakikishe kuwa miche ya korosho inapatikana ya kutosha. |
| 3 | Mabadiliko ya tabia nchi (upungufu wa mvua) pamoja na magonjwa ya korosho. | Bodi ihakikishe kuwa miche ya korosho inapatikana kwa wakati sahihi (mwezi Oktoba/Nov) kila mwaka pamoja na upatikanaji wa dawa ya sulfur kwa wakulima watakao otesha zao hilo. |
| 4 | Upungufu mkubwa wa Maafisa ugani (Wilaya ina Kata 28 na vijiji 68 vyenye Maafisa ugani 35 tu) | Serikali iendelee kuajiri Maafisa Ugani ili huduma za ugani vijijini ziweze kutolea kwa tija kwa wakulima. |

#### 5.11.3.6 Mikakati ya kuendeleza zao la korosho ifikapo 2029/2030

Bodi ihakikishe kuwa miche ya korosho inapatikana ya kutosha kwa wakati na iandae mpango wa mafuzo kwa maafisa ugani wa Wilaya zinazoanza kulima zao hilo pamoja na wakulima ili waweze kuhamasika kulima zao la korosho.

### 5.11.4 Halmashauri ya Wilaya ya Moshi

#### 5.11.4.1 Uzalishaji msimu 2024/2025 na mpango wa uzalishaji msimu wa 2029/2030.

##### 5.11.4.1.1 Uzalishaji wa msimu 2024/2025.

Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kwa msimu wa 2024/25 imeendelea kutoa elimu kwa wakulima wa mfano 17 katika kata za Kahe Magharibi, Kahe Mashariki, Makuyuni, Uru Kusini na Uru shimbwe na wataalamu 13 lengo ni kuwa na uelewa wa zao la korosho.

##### 5.11.4.1.2 Mpango/Makadirio ya uzalishaji kiwilaya misimu ya 2024/2025, ya moshi misimu 2025/2026, 2027/2028 na 2029/2030

Halmashauri ya Wilaya ya Moshi itaendelea kutoa elimu kwa wataalamu na wakulima juu ya mbinu bora za ukuzaji na ustawishaji zao la korosho, Pia imenunua pampu tatu (Motorized blower) za kufundishia wataalamu na wakulima juu ya elimu ya uthibiti wa wadudu na magonjwa. Aidha kwa msimu wa 2024/25 Halmashauri haikupokea mbegu wala viuatilifu kutoka bodi ya korosho Tanzania.

**Mahitaji ya Mbegu**

| MSIMU | 2024/25 | 2025/26 | 2026/27 | 2028/29 | 2029/2030 |
|---|---|---|---|---|---|
| KILO | 500 | 1500 | 500 | 500 | 500 |

#### 5.11.4.2 Mpango wa upatikanaji wa mbegu bora na miche bora ya korosho

Kuanzia msimu 2022/2023 Halmashauri ilitenga bajeti ya TSH 6,000,000/= kupitia vyanzo vyake vya ndani ili kuhakikisha uanzishwaji wa vitalu vya miche bora ya korosho ambavyo wakulima wangechangia kiasi kidogo ingawa fedha hizo hazikuweza kupatikana kutokana na makusanyo ya mapato kuwa kidogo.

### 5.11.5 Ubanguaji wa msimu 2025/2026 na mpango wa ubanguaji ifikapo msimu 2029/2030.

#### 5.11.5.1 Ubanguaji Msimu 2025/2026.

Halmashauri ya wilaya ya Moshi kifupi bado tupo katika hatua za awali kabisa katika uzalishaji wa zao la korosho ingawa kiasi kidogo ambacho kimeanza kupatikana kinatumika kufundishia jinsi ya kubangua korosho kwa ngazi ya kaya kiasili.

### 5.11.6 Mpango/Makadirio ya ubanguaji kiwilaya kwa msimu 2026/2027, 2027/2028, 2028/2029, 2029/2030.

Aidha kabla ya msimu 2026/2027 mpango wa wilaya kiubanguaji utakuwa

i. Kutoa elimu ya ubanguaji ngazi ya kaya kwa kutumia mashine rahisi zinazopatikana SIDO.
ii. Wakulima wadogo kujiunga pamoja ili kuwapatia elimu ya ubanguaji kwa njia ya vikundi ili kuongeza mnyororo wa thamani wa zao la korosho.
iii. Kwa kushirikiana na gereza la Karanga tutajadiliana kwa pamoja kuona umuhimu wa kuwa na kiwanda kidogo cha kubangua korosho ghafi
iv. Ifikapo 2029/2030 tutawezesha wakulima kupata elimu ya matumizi mbalimbali ya korosho zilizobanguliwa kama maziwa ya korosho, siagi ya korosho

### 5.11.7 Hali ya huduma za ugani na mafunzo na mpango wa 2025/26 wa kuendeleza zao la korosho.

Halmashauri hadi sasa inaendelea na zoezi la kuhamasisha kilimo cha Korosho kupitia wataalamu 32 ngazi ya kata kwa kuwajengea uelewa juu ya umuhimu wa uandaaji mashamba, udhibiti wa wadudu na magonjwa, masoko, ubanguaji na faida ya zao la korosho.

### 5.11.8 Changamoto na mapendekezo ya utatuzi.

| NA. | CHANGAMOTO | PENDEKEZO LA UTATUZI |
|---|---|---|
| 1 | kukosekana fedha ya kuratibu zao la korosho katika Halmashauri | BODI ya korosho Tanzania iwezeshe fedha Halmashauri mpya |
| 2 | Kukosekana mafunzo rejea ya zao la korosho kwa wataalam wa kilimo. | TARI na CBT waratibu mafunzo kwa wataalamu |
| 3 | Uhaba wa maafisa ugani | Wizara itoe ajira. |

### 5.11.9 Hitimisho

Mkoa umejipanga kuhakikisha zao la korosho linalimwa kwa tija hivyo tunapendekeza BODI YA KOROSHO na TARI (kituo cha utafiti Naliendele) iendelee kutoa mafunzo hasa fursa zinapopatikana.

## 5.12. TAARIFA MKOA WA KIGOMA

### 5.12.1. Utangulizi

Mkoa wa Kigoma ni miongoni mwa Mikoa mipya katika uzalishaji wa zao la Korosho. Zao hili lilianza kuhamasishwa na hatimaye kupandwa katika msimu wa kilimo wa 2017/2018 katika Halmashauri za Uvinza na 2028/2019 katika Halmashauri ya Kibondo. Mkoa wa Kigoma umekusudia kuendeleza kilimo cha zao la korosho hata kwenye Halmashauri nyingine ili kuwezesha wananchi kuendena na uchumi wa kati wa viwanda. Kufutia azma hiyo hamasa inaendelea kufanyika katika Halmashauri za Kakonko, Kasulu Vijijini na Kigoma Vijijini imeonesha mwitikio mkubwa wa kuanza kulima zao hilo. Matarajio kwa msimu wa 2029/2030 Halmashauri zinazozalisha Korosho katika mkoa wa Kigoma zinatarajia kuongezeka hadi kufikia 5.

### 5.12.2. Takwimu za uzalishaji msimu 2024/2025

Kwa msimu wa 2024/2025 Halmashauri **pekee ya Uvinza** imezalisha jumla ya kilo 1**7,000** za Korosho. Kwa Halmashauri ya Kibondo uzalishaji unatarajiwa kuanza msimu wa 2025/2026.

**Mpango wa Uzalishaji na Makadilio ya uzalishaji kiwilaya.**

| WILAYA | Malengo ya Uzalishaji kwa Mwaka | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2025/26 | | 2026/27 | | 2027/28 | | 2028/29 | | 2029/30 | |
| | HA | MT | HA | MT | HA | MT | HA | MT | HA | MT |
| Uvinza | 760 | 116 | 1000 | 380 | 1500 | 532 | 2400 | 592 | 3463 | 800 |
| Kibondo | 134 | 10 | 400 | 130 | 530 | 150 | 600 | 300 | 936 | 400 |

### 5.12.3. Halmashauri ya Uvinza inatarajia kuendelea kupata mbegu na miche bora

Kutoka bodi ya korosho Tanzania. Halmashauri ya Kibondo haihitaji mbegu kwa sasa bali inafatilia maendeleo na utunzwaji wa miche mashambani ili kuona uzalishaji utakavyokuwa kabla ya kuendelea kuhamasisha wakulima. Mbegu bora za

korosho zinazotumika na zilizopandwa kwenye mashamba zinatoka TARI Naliendele. Hadi sasa Jumla ya mbegu bora 197,608.72 (151,080 Uvinza na 46,528.72 Kibondo).

### 5.12.4. Ubanguaji na mpango uliopo

i. Pamoja na Halmashauri ya Uvinza kuanza uvunaji wa Korosho katika msimu wa 2020/2021 hakuna kiwanda  cha kubangua korosho isipokuwa mashine ndogo ndogo zinazobangua korosho mojamoja na kufanya kazi hiyo kuwa ngumu. Jitihada kubwa zinafanyika ili kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo katika tasnia hii ya Korosho kuja kuwekeza katika viwanda uzalishaji utakapokuwa wa kuridhisha.

ii. Makadirio ya ubanguaji kwa misimu ya 2026-2030 yataendelea kutumia Mashine ndogo kama hakutojitokeza muwekezaji/wadau watakaowezesha upatikanaji wa mashine kubwa au viwanda vidogo.

### 5.12.5. Hali ya huduma za ugani.

Katika baadhi ya kata zinazozalisha zao la Korosho kuna Maafisa Ugani kilimo. Uwepo wao umeendelea kutatua changamoto mbalimbali za Wakulima ikiwemo utoaji wa elimu kuhusu kanuni bora za kilimo cha korosho.

### 5.12.6. Changamoto katika uzalishaji wa korosho na utatuzi wake

i. Ukosefu wa pembejeo za zao la Korosho hasa Sulpher na pampu za kupulizia kwani kwa sasa bidhaa hizo zinapatina kituo kilichopo Singida.
ii. Ukosefu wa maghala kwa ajili ya kuhifadhia korosho pamoja na eneo maalum kwa ajili ya kuendeshea  masoko kwa mfumo wa soko la pamoja na minada.
iii. Ukosefu wa mafunzo rejea kwa maafisa ugani kuhusu kanuni za kilimo bora cha korosho kwa wataalam wa ngazi ya Mkoa na Serikali za Mitaa.
iv. Ukosefu wa viwanda vya kubangua pamoja na elimu ya ubanguaji wa Korosho kwa wakulima.
v. Ushirikishanaji wa taarifa baina ya Bodi, Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.
vi. Uchomaji hovyo wa moto unaofanywa na wakulima/wafugaji.
vii. Miche mingi kuharibika/kukauka kwa sababu ya matunzo duni ya wakulima na kutojua aina za magonjwa ya zao hilo.

#### 5.12.7. Utatuzi wa changamoto

i. Kwa kuwa sasa Mkoa wa Kigoma umeanza kilimo cha zao la Korosho, Bodi ya korosho Tanzania inashauriwa kupendekeza kituo cha TARI Kihinga kilichopo Mkoani Kigoma ambacho kinajihusisha na utafiti wa zao la chikichi, kiongezewe wataalam waliobobea katika zao la Korosho kwa ajili ya kuendeleza zao katika ukanda wa Magharibi

ii. Kwa kuwa uvunaji na uokotaji wa Korosho umeshaanza wakati wakulima hawana mashine/viwanda vya kubangua Korosho, Bodi ya Korosho Tanzania isaidie upatikanaji wa mashine.

iii Bodi ya korosho kwa kushirikiana na Mamlaka zingine igharamie mafunzo kuhusu mbinu na kanuni bora za kilimo cha Korosho kwa Maafisa Ugani kutoka ngazi ya Mkoa na Halmashauri.

#### 5.12.8. Mikakati ya kuendeleza zao la korosho hadi 2029/2030

Katika kipindi cha miaka Mitano ijayo kuanzia 2024/2025 hadi 2029/20230 Mkoa umejipanga kufanya yafuatayo ili kuendeleza zao la Korosho.

i. Kuongeza eneo la uzalishaji wa zao la korosho kutoka ekari **2235** hadi kufikia ekari **11,997** ikiwa ni pamoja na kuzalisha Korosho zenye ubora wa daraja la juu

ii. Kushirikiana na wadau wa maendeleo ili kujenga angalu maghala 3 yatakayotumika kuhifadhia korosho pamoja na kutenga eneo kwa ajili ya kuendeshea minada.

iii. Kuendelea kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania kutoa mafunzo kwa wakulima wa zao la Korosho kuhusu mbinu sahihi za utunzaji na uendelezaji wa zao la Korosho.

iv. Kwa ushirikiano na Bodi ya Korosho Tanzania na SIDO yaandaliwe mafunzo kwa wakulima kuhusiana na namna bora kubangua Korosho ili kuwawezesha wakulima kuuza Korosho iliyobanguliwa.

v. Kuhamasisha wakulima kuunda na kujiunga na vyama vya wakulima (AMCOS) vya Korosho na kuwajengea uwezo viongozi wa vyama vitakavyoundwa katika masuala ya fedha na uendeshaji wa masoko ya zao la Korosho.

vi. Kuendelea kuhamasisha wafanyabiashara kuwekeza katika fursa ya uuzaji wa Pembejeo za zao la Korosho ili kurahisisha upatikanaji wa bidhaa hizo kwa wakulima.

### 5.12.9. Hitimisho.

Mkoa wa Kigoma unalenga kuendelea kukuza mazao ya kimkakati Ikiwemo zao la korosho na kuyaendeleza ili kuendelea kuboresha kipato cha Mkoa, kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Ni katika Mazingira hayo Mkoa unaendelea kushirikiana na Wadau mbalimbali ikiwemo Bodi ya Korosho katika jitihada za kuendeleza zao hili muhimu.

## 5.13. TAARIFA YA MKOA WA LINDI

### 5.13.1. Utangulizi

Mkoa wa Lindi una jumla ya wilaya 5 ikiwemo Kilwa, Lindi, Liwale, Nachingwea na Ruangwa na halmashauri 6 ikiwemo Kilwa, Mtama, Lindi Manispaa, Liwale, Nachingwea na Ruangwa. Mkoa kupitia mamlaka ya Serikali za mitaa ina mabonde mazuri ambayo hutumika kuzalisha mazao mbalimbali ikiwemo ya chakula pamoja na ya bustani. Kilimo ni shughuli kuu ya kiuchumi ambayo inaajiri asilimia kubwa ya wakazi wa Mkoa wa Lindi, takribani asilimia 90 ya wakazi wote wanajishughulisha na kilimo.

### 5.13.2. Uzalishaji 2024/2025 na mpango wa uzalishaji ifikapo msimu 2029/2030

**Uzalishaji msimu 2024/2025**

| NA | HALMASHAURI | UZALISHAJI TANI |
|---|---|---|
| 1 | Liwale | 19,693.408 |
| 2 | Nachingwea | 31,334.00 |
| 3 | Ruangwa | 22,799.01 |
| 4 | Kilwa | 10,652.60 |
| 5 | Manispaa ya Lindi | 6,507.79 |
| 6 | Mtama | 24,693.48 |
| | **JUMLA KUU** | **115,680.505** |

Soko la awali

***Kiasi cha korosho kilichouzwa kupitia soko awali msimu 2024/2025***

| S/N | JINA LA KAMPUNI | CHAMACHA MSINGI ALICHONUNUA | HALMASHAURI | KILO ZILIZOUZWA (KG) | BEI Shs. T | THAMANI Shs. T |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Al-andalus CO. Ltd | Ulina AMCOS | Kilwa | 10,000 | 2,200 | 22,000,000 |
| 2 | Al-andalus CO. Ltd | Ulina AMCOS | Kilwa | 10,000 | 2,000 | 20,000,000 |
| 3. | Min Holding tz Ltd | Namakongoro AMCOS | Kilwa | 20,000 | 2,000 | 40,000,000 |
| 4 | Al-andalus CO. Ltd | Ulina AMCOS | Kliwa | 3,000 | 2,200 | 6,600,000 |
| 5. | Amama Farms Ltd | Kiwalala AMCOS | Mtama | 200,000 | 2,500 | 500,000,000 |
| 6 | Afritech Co. Ltd | Sudi AMCOS | Mtama | 22,000 | 1,350 | 29,700,000 |
| 7 | Min holding Tz Ltd | Mandwanga AMCOS | Mtama | 20,000 | 2,000 | 40,000,000 |
| 8 | Al-andalus CO. Ltd | Kitumiki AMCOS | Lindi Manispaa | 10,476 | 1,100 | 11,523,600 |
| 9 | Min Holding Tz Ltd | A/Mingoyo AMCOS | Lindi Manispaa | 10,000 | 2,000 | 20,000,000 |
| 10 | Min Holding Tz Ltd | A/Mingoyo AMCOS | Lindi Manispaa | 4,000 | 2,000 | 8,000,000 |
| 11 | Farhem Co Ltd | Nduruka AMCOS | Liwale | 10,896 | 1,500 | 16,344,000 |
| | **JUMLA** | | | **309,476** | | **714,167,600** |

**Mpango/makadirio ya uzalishaji kiwilaya misimu 2025/2026, 2026/2027, 2027/2028, 2028/2029 na 2029/2030**

| MWAKA | LIWALE | NACHINGWEA | RUANGWA | KILWA | LINDI MC | MTAMA | JUMLA YA MKOA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Lengo uzalishaji Tani | Lengo uzalishaji Tani | Lengo uzalishaji Tani | Lengo uzalishaji Tani | Lengo uzalishaji Tani | Lengo uzalishaji Tani | |
| 2025-2026 | 50,843.95 | 34,000 | 17,500 | 10,567 | 8,500 | 27,127 | **148,537.95** |
| 2026-2027 | 56,291.51 | 38,000 | 23,000 | 12,226 | 10,500 | 29,560 | **169,577.51** |
| 2027-2028 | 61,739.08 | 40,000 | 24,500 | 14,887 | 12,500 | 31,994 | **185,620.08** |
| 2028-2029 | 67,186.64 | 44,000 | 27,000 | 15,466 | 14,000 | 34,428 | **202,080.64** |
| 2029-2030 | 72,634.21 | 50,000 | 30,000 | 16,894 | 16,500 | 36,861 | **222,889.21** |
| | **308,695.39** | **206,000** | **122,000** | **70,040** | **62,000** | **159,970** | **928,705.39** |

#### 5.13.3. Mpango wa upatikanaji wa mbegu na miche bora ya mikorosho

Msimu 2025-2026 Mkoa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali una lengo la kuzalisha miche bora ya mikorosho 720,000 kupitia Mamlaka za serikali za Mitaa na kusambaza kwa wakulima bure. Uzalishaji huu utafanyika kupitia vikundi mbalimbali vya wakulima, Taasisi au mkulima mmojammoja. Aidha, Halmashauri ya Kilwa na Ruangwa inatarajia kuanzisha kitalu cha miche ya mikorosho kwenye eneo la shamba la halmashauri kwa ajili ya kuwasambazia wakulima.

**Vikundi/Taasisi vitakavyozalisha miche msimu 2025/2026 Halmashauri ya Ruangwa**

| KIKUNDI/MZALISHAJI | KIJIJI | MICHE ILIYOBEBESHWA | MICHE ISIYOBEBESHWA | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| Idara ya kilimo | Kilimanihewa | 4,000 | 60,000 | 100,000 |
| MAGESA group | Kilimanihewa | - | 20,000 | 20,000 |
| Umoja Likwachu group | Likwachu | - | 5,000 | 5,000 |
| Kikundi cha Nahanga group | Nahanga | - | 10,000 | 10,000 |
| **Jumla** | | | **95,000** | **135,000** |

**MPANGO WA UZALISHAJI MICHE BORA MIKOROSHO 2025-26**

| Na | Halmashauri | Kiasi cha miche inayotarajia kuzalishwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1 | Liwale | 50,000 | Halmashauri inatarajia kununua mbegu kilo 1000 kupitia mapato ya ndani |
| 2 | Nachingwea | 200,000 | Uzalishaji hutegemea Halmashauri na wadau wengine |
| 3 | Ruangwa | 135,000 | Halmashauri inatarajia kununua kilo 900 za mbegu bora na kuzalisha miche |
| 4 | Kilwa | 300,000 | Halmashauri ya wilaya imepanga kununua mbegu bora za korosho kilo 2000 na kusambaza kwa wakulima |
| 5 | Manispaa ya Lindi | 20,000 | |
| 6 | Mtama | 150,000 | Halmashauri itaboresha miche iliyozeeka, na miche itapatikana TARI kituo kidogo cha Nyangao |
| | | **720,000** | |

**5.13.4.** Ubanguaji msimu 2025/2026 na mpango wa ubanguaji ifikapo msimu 2029/2030

a) Ubanguaji msimu 2025/2026

| NA | HALMASHAURI | UBANGUAJI TANI |
|---|---|---|
| 1 | Liwale | 30 |
| 2 | Nachingwea | 5 |
| 3 | Ruangwa | 7685 |
| 4 | Kilwa | 200 |
| 5 | Manispaa ya Lindi | 8 |
| 6 | Mtama | 6814 |
| | **JUMLA KUU** | **14,742** |

b) Mpango/makadirio ya ubanguaji kiwilaya misimu 2026/2027, 2027/2028, 2028/2029, 2029/2030

**MAKADIRIO YA UBANGUAJI KWA MWAKA**

| MWAKA | LIWALE | NACHINGWEA | RUANGWA | KILWA | MANISPAA | MTAMA | JUMLA YA MKOA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Makadirio Tani | Makadirio Tani | Makadirio Tani | Makadirio Tani | Makadirio Tani | Makadirio Tani | |
| 2025-2026 | 30 | 5 | 8 | 300 | 12 | 6,814 | **354.50** |
| 2026-2027 | 100 | 6 | 10 | 700 | 13 | 7,544 | **827.50** |
| 2027-2028 | 400 | 7 | 11 | 1,200 | 14 | 8,274 | **1,631.50** |
| 2028-2029 | 600 | 8 | 16 | 1,700 | 15 | 9,004 | **2,338.50** |
| 2029-2030 | 1,000 | 11 | 21 | 2,200 | 16 | 9,735 | **3,247.50** |
| | **2,130.** | **37** | **66** | **6,100** | **68** | **41,371** | 8,399.50 |

**5.13.5. Hali ya huduma za ugani na mafunzo na mpango 2025/2026**

TARI Naliendele kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania na Sekretarieti ya mkoa walitoa mafunzo ya agronomia ya korosho na matumizi sahihi na salama ya viuatilifu vya zao la korosho kwa Maafisa ugani wa BBT na ngazi ya halmashauri.

Jumla ya Maafisa ugani 151 wa BBT na Maafisa ugani 268 wa Halmashauri walipata mafunzo hayo. Aidha, mkoa kwa kushirikiana na halmashauri za wilaya kupitia wataalam wake wameendelea kutoa elimu ya kilimo bora cha zao la korosho na ushauri kwa wakulima hasa ubebeshaji wa mikorosho ya zamani, matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa wakulima na wapuliziaji, udhibiti ubora wa korosho, utunzaji wa mashamba na upangaji wa madaraja. Jumla ya wakulima 76,340 wamepatiwa elimu hiyo kupitia mikutano mbalimbali ya vijiji, wakati wa ugawaji wa pembejeo kwenye AMCOS

### 5.13.6. Changamoto zinazokabili shughuli za uendelezaji zao la korosho na mapendekezo ya utatuzi wake

i. Upatikanaji wa pembejeo za korosho kwa wakati
ii. Ukosefu wa mikopo midogo na mikubwa kwa wakulima ili kuendeleza kilimo cha korosho na mazao mengine, ununuzi wa mabomba ya kupulizia mikorosho.
iii. Kutokuwa na miundombinu ya uhakika kama barabara hususan maeneo ya vijijini kipindi cha masika
iv. Uchanganyaji wa korosho chafu na safi kwa baadhi ya Vyama vya Msingi
v. Mabadiliko ya tabianchi inayopelekea milipuko ya magonjwa ya mikorosho ukiwemo ugonjwa wa mnyauko fusari unaoathiri na kuangamiza mashamba ya mikorosho ambapo miti hukauka na kufa kabisa kwa baadhi ya maeneo ikiwemo Kata ya Liwale B Halmashauri ya Liwale na Kata ya Mnazi mmoja halmashauri ya Manispaa ya Lindi.
vi. Uvamizi wa tembo kwenye mashamba ya mikorosho na kuvunja miti, kumenya magome ya miti na kung;oa miche iliyopandwa.
vii. Uwepo bwa viuatilifu vipya na kukosa elimu ya matumizi sahihi juu ya upuliziaji.
viii. Upatikanaji mdogo wa viuatilifu vya kuzuia na kudhibiti magonjwa kwenye zao la korosho msimu 2025/2026.
ix. Gharama kubwa ya kusafirisha miche ya mikorosho, sanjari na kuharibika kwa miche mingi wakati wa kupakia na kushusha kutokana na umbali mrefu.
x. Ucheleweshaji wa Mafunzo ya (upuliziaji) na matumizi ya viuatilifu vipya.
xi. Hakuna uhakika wa masoko ya korosho zilizobanguliwa
xii. Changamoto ya mfumo wa upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima

### 5.13.7. Mikakati ya kuendeleza zao la korosho ifikapo 2029/2030

i. Kuandaa mashamba ya mfano katika maeneo yaliyotengwa ili kupanda mikorosho mipya.
ii. Kwa kushirikiana na Bodi ya korosho kuhamasisha na kugawa mbegu za korosho kwa wakulima na kuotesha miche bora na kusambaza kwa kulima ili kuongeza uzalishajikwa msimu inayoendelea.
iii. Kuendelea kutoa elimu ya namna mzuri ya utunzaji wa mashamba ya mikorosho na upuliziaji.
iv. Kutoa mafunzo kwa wakulima ya kuongeza thamani ya zao la korosho kwa kubangua na kuuza.
v. Ufufuaji wa mashamba pori na uanzishwaji wa mashamba mapya na kusambaza miche na mbegu bora kwa wakulima.
vi. Kubebesha mikorosho ya zamani ili kuongeza tija ya uzalishaji
vii. Kuratibu na kusimamia upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima
viii. Kusimamia uboreshaji wa kiwanda cha kubangua korosho kinachosimamiwa na Umoja wa ubanguaji korosho wilaya ya Ruangwa.
ix. Kuendeleza na kuanzisha mashamba ya pamoja katika Kata na Vijiji kwenye Mamlaka za serikali za Mitaa
x. Kuendeleza na kuanzisha vitalu vipya vya miche bora ya mikorosho
xi. Halmashauri kuhakikisha inasajili wakulima wote na kuingiza kwenye daftari la wakulima ili kuwa na takwimu sahihi.
xii. Kusimamia masoko ya ndani na nje ya nchi kwa kuimarisha vyama vya ushirika/SACCOS

### 5.13.8. Hitimisho

Wadau wa kilimo kwa kushirikiana na Taasisi za serikali zina wajibu wa kuinua tasnia ya korosho kwa kumuwezesha mkulima kuzalisha kwa tija kwa kutumia kanuni bora za kilimo pamoja na kusimamia masoko ya ndani nan je ya nchi kwa kuimarisha utendaji bora wa vyama vya msingi vya mazao, SACCOS na kuwezesha upatikanaji wa mikopo ya kilimo na pembejeo kwa wakulima. Aidha, ushirikiano na uwajibikaji wa Pamoja katika ngazi zote utaleta ufanisi katika Mpango wa uendelezaji wa zao la korosho.

## 5.14. TAARIFA YA MKOA WA DODOMA

### 5.14.1 Utangulizi

Baada ya kufanyika utafiti na matokeo kuonyesha kuwa zao la korosho linaweza kustawi na kuzaa katika mkoa wa Dodoma, jitihada za kuanzisha zao hili zilianza mwaka 2007/2008. Kilimo cha zao la korosho kinafanyika zaidi katika wilaya za Kongwa na Mpwapwa. Idadi ya Wakulima, Mikorosho nae neo linalolimwa korosho

Mkoa una jumla ya wakulima 1940 wenye jumla wenye mashamba yanayofikia ekari 23,835. Mchanganuo wa idadi ya wakulima, idadi ya mikorosho na eneo umeonyeshwa kwenye jedwali hapo chini.

**Idadi ya wakulima, mikorosho na eneo linalolimwa**

| Na | Halmashauri | Idadi ya wakulima | Idadi ya Mikorosho | Eneo (Ekari) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kongwa | 1583 | 254,215 | 9079 |
| 2. | Mpwapwa | 357 | 413,164 | 14756 |
| | **Jumla** | **1940** | **667,379** | **23835** |

### 5.14.2 Uzalishaji Msimu wa 2024/25

Uzalishaji wa korosho unaendelea katika Halmashauri za Kongwa na Mpwapwa, Inakadiriwa jumla ya tani 45 zimezalishwa katika Halmashauri za Kongwa na Mpwapwa kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini

**Uzalishaji wa Korosho kwa msimu wa 2024/25**

| Na | Halmashauri | Uzalishaji (Tani) |
|---|---|---|
| 1. | Kongwa | 9 |

### 5.14.3 Mpango/Makadirio ya uzalishaji msimu wa 2025/26 – 2029/30

Mkoa unatarajia kuongeza uzalishaji wa korosho kutoka tani 45 mwaka 2024/25 hadi tani 335.9 mwaka 2029/30. Mchanganuo kwa kila Halmashauri umeonyeshwa kwenye jedwali hapo chini.

**Makadirio ya uzakishaji msimu wa 2025/26 – 2029/30**

| Na | Halmashauri | Malengo ya Uzalishaji (Tani) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2025/2026 | 2026/2027 | 2027/2028 | 2028/2029 | 2029/30 |
| 1. | Kongwa | 22.8 | 45.6 | 68.4 | 102.6 | 153.9 |
| 2. | Mpwapwa | 36 | 75 | 150 | 168 | 182 |
| | **Jumla** | **58.8** | **120.6** | **218.4** | **270.6** | **335.9** |

### 5.14.4 Ubanguaji Msimu wa 2024/25 na Mpango wa ubanguaji kwa misimu ijayo

Kwa sasa Mkoa una mdau mmoja katika Halmashauri ya Kongwa ambaye ameanzisha kiwanda kimoja cha kubangua korosho chenye uwezo wa kubangua tani 60 za korosho kwa mwaka. Aidha, chama cha Ushirika wa Korosho DOMASICA kimepanga pia kuanzisha kiwanda cha kubangua korosho. Ni matarajio ya mkoa, uwekezaji huo utasaidia kubangua korosho katika kipindi hiki tunachoendelea kuhamasisha.

### 5.14.5 Huduma za ugani na mafunzo

Huduma za Ugani zinaendeleakutolewa kwa wakulima wa Korosho juu ya utunzaji wa mikorosho hususan matumizi sahihi ya viuatilifu. Bodi ya Korosho ilitoa viuatilifu lita 694 za kudhibiti wadudu na magonjwa

Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na TARI Naliendele imekuwa ikitoa mafunzo kwa Maafisa ugani na wakulima juu ya kanuni bora za kilimo cha korosho . Mafunzo haya yamesaidia kiasi lakini bado hayawezi kukidhi mahitaji kwa sababu ni ya muda mfupi, siku mbili hazitoshi kumjengea Afisa Ugani ubobezi stahiki. Ushauri kwa Bodi na TARI Naliendele ili kupata Wataalam mahiri kwenye tasnia ya Korosho ni muhimu kuwa na mafunzo maalum yatakayochukua muda mrefu kuanzia mwezi kwa baadhi ya Maafisa ugani yakihusisha elimu kwa vitendo. Hii itasaidia kuwa na Maafisa Ugani wabobezi kwenye kanuni bora za Kilimo cha Korosho.

Chama cha Ushirika DOMASICA kimepatiwa mafunzo yaliyowezeshwa na wataalam kutoka Chama cha Ushirika Moshi kanda ya Dodoma. Hadi sasa chama hiki kina wanachama 83 kutoka Halmashauri za Kongwa, Mpwapwa, Chamwino, Kiteto na Bahi.

### 5.14.6 Changamoto zinazokabili shughuli za uendelezaji wa zao la korosho na mapendekezo ya utatuzi wake.

i. Gharama kubwa za pembejeo hivyo wakulima kushindwa kumudu gharama za ununuzi wa pembejeo.
ii. Ukosefu wa mabomba ya kupulizia korosho miongoni mwa wakulima wa korosho hali inayofanya uzalishaji kuwa duni kutokana na kushindwa kuzuia magonjwa na wadudu.

iii. Ukosefu mkubwa wa pembejeo hususani viuatilifu vya zao la korosho kwa kuwa wakulima ambao hawapo chini ya DOMASICA AMCOS hawapatiwi viuatilifu vya zao hilo kwa kuwa siyo wanachama
iv. Ukosefu wa mafunzo rejea ya kilimo bora cha korosho miongoni mwa wakulima na maofisa ugani katika wilaya.
v. Magonjwa na wadudu.
vi. Ukosefu wa soko la uhakika.
vii. Maeneo mengi ni makame hivyo ni vigumu kuanzisha vitalu vya uzalishaji wa miche ya korosho.
viii. Ulishaji wa mifugo kiholela hivyo kuharibu miche iliyokwishapandwa mashambani.

#### 5.14.7 Mapendekezo

i. Kuwaunganisha wakulima na masoko
ii. Kuwapatia wakulima ruzuku ya pembejeo ili kuongeza uzalishaji
iii. Kuendelea kuwapatia wakulima elimu ya utunzaji wa zao la Korosho
iv. Uanzishwaji wa sheria ndogo ndogo katika ngazi ya Kijiji/ Kata ili kulinda mikorosho dhidi ya mifugo

#### 5.14.8 Hitimisho

Ili kilimo cha korosho kiwe endelevu na chenye tija kwa wakulima nguvu kubwa inahitajika ikiwa ni pamoja na kufanya uhamasishaji kwa wakulima ili kuongeza maeneo ya uzalishaji na kuwaunganisha na masoko. Pia utoaji wa pembejeo za ruzuku ni muhimu kwa wakulima kwa kuwa wakulima wengi wana kipato duni hivyo hushindwa kumudu gharama za pembejeo na kupelekea mikorosho kushindwa kuzaa kutokana na uharibifu wa magonjwa na wadudu.

### 5.15 TAARIFA YA MKOA WA SHINYANGA

#### 5.15.1 Utangulizi

Mkoa wa Shinyanga unalima mazao mbalimbali ya biashara ambayo ni pamba, umbaku, mkonge, alizeti na korosho. Mkonge hulimwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, korosho hulimwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu na mazao mengine ya biashara yakilimwa katika Halmashauri 6 za Mkoa wa

Shinyanga. Jumla ya hekta 365 zimepandwa mikorosho katika Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu. Mikorosho hiyo imepandwa na wakulima 402 kuanzia mwaka 2028/2029 ambao wana jumla ya miti 28,116 hadi msimu wa kilimo wa 2024?2025. Kiasi cha tani 2.6 za korosho ghafi kimevunwa ikiwa ni matokeo ya mikorosho iliyopandwa msimu wa kilimo wa 2028/2019.

#### 5.15.2 Uzalishaji wa zao la korosho msimu 2024/2025 na Mpango wa Uzalishaji Ifikapo 2029/2030

**Uzalishaji msimu 2024/2025**

| Na | Lengo (ha) | Uzalishaji (ta) |
|---|---|---|
| 1 | 465 | 2.6 |

**Mpango/makadirio ya uzalishaji kwa msimu wa 2024/2025, 2025/2026, 2026/2027, 2027/2028, 2028/2029 na 2029/2030**

| Halmashauri | 2024/2025 | 2025/2026 | 2026/2027 | 2027/2028 | 2028/2029 | 2029/2030 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Lengo (Tani) | Lengo (Tani) | Lengo (Tani) | Lengo (Tani) | Lengo (Tani) | Lengo (Tani) |
| Ushetu | 12 | 128 | 170 | 200 | 220 | 375 |

#### 5.15.3 Mpango wa Upatikanaji mbegu na miche bora ya korosho.

Mkoa wa Shinyanga kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu iliotesha jumlaya miche 17,000 kwa msimu wa kilimo wa 2023/2024 na kuigawa wa wakulima ikiwa ni jitahada za kuhamasisha wakulima kulima zao hilo. jumla ya miche 17,000 ilioteshwa na halmashauri na kugaiwa kwa wakulima wake wapya na wazamani ambao waliongeza maeneo ya uzalishaji, ambapo jumla ya hekta 365 zimepandwa. Msimu wa kilimo 2024/2025, Halmashauri ilipokea gunia mbili za mbegu za korosho kutoka Bodi ya Korosho ambazo zitaoteshwa kuziotesha katika msimu wa kilimo wa 2025/2026 na kugawiwa kwa wakulima ili kuongeza wigo wa uzalishajiwa zao la korosho .

### 5.15.4 Ubanguaji msimu 2024/2025 na mpango wa ubanguaji ifikapo msimu wa 2029/2030

Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu ilinunua mashine mbili ndogo za kubangulia korosho ambazo zinatumiwa na wakulima kulingana na uhitaji kwa wale ambao wameanza/wataanza kuvuna korosho. Aidha Halmashauri katika bajeti ya 2024/2025 imenunua mashine ndogo kumi na mbili (12) za mkono kwa ajili ya kuwasaidia wakulima kubangua korosho.

**Mpango/Makadirio ya ubanguaji misimu ya 2024/2025 hadi 2029/2030**

| **Halmashauri** | **2024/2025** | **2025/2026** | **2026/2027** | **2027/2028** | **2028/2029** | **2029/2030** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Lengo (Tani) | Lengo (Tani) | Lengo (Tani) | Lengo (Tani) | Lengo (Tani) | Lengo (Tani) |
| Ushetu | 12 | 128 | 170 | 200 | 220 | 375 |

### 5.15.5 Huduma za Ugani

Idara ya Kilimo inatekeleza na kusimamia huduma za ugani katika kata 20 zilizohamasishwa kulima zao la korosho. Shughuli za uendelezaji wa zao la korosho ngazi ya Kata na Vijiji linasimamiwa na maafisa ugani 48. Hadi sasa wakulima wamepatiwa huduma za ugani ikiwemo elimu juu ya kanuni bora za kilimo cha zao la korosho kama palizi ya mikorosho, upogoleaji wa mikorosho, elimu ya matumizi salama ya pembejeo na utunzaji wa mashamba. Aidha Halmashauri imepokea viuatilifu kutoka Bodi ya Korosho aina ya *Pacha* lita 989, *Subachlo* lita 507, *Indazole* lita 1143, *Bravia* lita 911 na *Tegeta* lita251 kwa ajili ya kuhudumia zao la korosho.

### 5.15.6 Changamoto zinazokabili uendelezaji wa zao la korosho na mapendekezo ya utatuzi wake.

i. Milipuko magonjwa ya ukungu na wadudu waharibifu wa zao
ii. Uvamizi wa mifugo kwenye vitalu na mashamba ya korosho
iii. Upungufu wa zana bora za kilimo kama mabomba ya upuliziaji
iv. Ukosefu wa masoko.

### 5.15.7 Mikakati ya kuendeleza zao la korosho ifikapo 2029/2030

Katika kuendeleza uzalishaji wenye tija katika zao la korosho Halmashauri kwa kushirikiana na Mkoa kupitia Idara ya kilimo imeweka mikakati ifuatayo:

i. Kuendelea kuongeza maeneo ya uzalishaji kwa kuendelea kugawia wakulima miche ya korosho/ mbegu za korosho.

ii. Kujenga maghala ya kuhifadhia pindi wakulima wanaposubiria soko la kuuzia zao la korosho.

iii. Kununua pampu za kupulizia mikorosho ili kukabiliana na visumbufu vinavyopunguza uzalishaji.

iv. Kuendelea kutoa elimu kwa wakulima juu ya kilimo chenye tija cha zao hili na kuendelea kuwajengea uwezo Maafisa Ugani ili waweze kuendelea kutoa huduma bora za ugani kwa wakulima wa korosho.

v. Kuhamasisha wakulima na wajasiriamali wadogo kuongeza thamani katika zao la korosho kwa kuhamsisha matumizi ya mashine za ubanguaji ili kuweza kuuza korosho zilizobanguliwa na kuhifadhiwa katika vifungashio.

### 5.15.8 Hitimisho

Mkoa na Halmashauri wanatoa shukrani kwa Bodi ya Korosho (T) kwa kuendelea kuwa nasi bega kwa bega katika kuendeleza uzalishaji wa zao la korosho kwa kuleta viuatilifu na mbegu kwa wakulima. Aidha tunaendelea kuiomba Bodi ya Korosho (T) kuendelea kusaidia katika suala la kutafuta soko la uhakika ili wakulima wetu waweze kuona tija ya uzalishaji wa zao hilo.

## 5.16 TAARIFA YA MKOA WA SONGWE

### 5.16.1 Utangulizi.

Mkoa wa Songwe ni miongoni mwa Mikoa mipya inayozalisha Korosho Nchini. Zao la korosho lilianza kuzalishwa Mkoa wa Songwe mwaka 2018/2019. Mkoa wa Songwe una eneo linalofaa kwa kilimo Hekta 1, 918,776.94 kati ya hizo Hekta 200,000 zinafaa kwa kilimo cha zao la Korosho ambapo Hekta 2,593 zimelimwa na zina mikorosho 181,510 (Songwe Hekta 2,315 zenye mikorosho 162,050 na Momba Hekta 278 zenye mikorosho 19,460

### 5.16.2 Uzalishaji msimu wa 2024/2025 na mpango wa uzalishaji ifikapo msimu wa 2029/2030.

Msimu wa kilimo 2024/2025 Mkoa ulizalisha tani 4.638 za Korosho ghafi kati ya hizo Songwe tani 3.638 na Wilaya ya Momba tani 0.876 (0.8 kutoka kwenye mikorosho mikuu.na 0.076 kutoka kwenye miti iliyopandwa mwaka 2021/2022, mpango wa uzalishaji ifikapo msimu wa 2029/2030 ni kuzalisha tani 22.11( Songwe tani 19.71 na Momba tani 2.4)

**Uzalishaji msimu wa 2024/2025.**

Msimu wa kilimo 2024/2025 Mkoa ulizalisha tani 4.638 za Korosho ghafi kati ya hizo Songwe tani 3.638 na Wilaya ya Momba tani 0.876 (0.8 kutoka kwenye mikorosho mikuu.na 0.076 kutoka kwenye miti iliyopandwa mwaka 2021/2022.

**Mpango/makadirio ya uzalishaji kiwilaya misimu ya 2025/2026, 2026/2027, 2027/2028, 2028/2029 na 2029/2030.**

| Halmashauri | 2025/2026 TANI | 2026/2027 TANI | 2027/2028 TANI | 2028/2029 TANI | 2029/2030 TANI |
|---|---|---|---|---|---|
| Songwe | 4.77 | 7.73 | 10.75 | 16.79 | 19.71 |
| Momba | 0.88 | 1 | 1.4 | 1.9 | 2.4 |
| **JUMLA TANI** | **5.65** | **8.73** | **12.15** | **18.69** | **22.11** |

### 5.16.3 Mpango wa upatikanaji mbegu na miche bora ya korosho.

Halmashauri za wilaya za Songwe na Momba msimu 2025/2026 zitanunua tani 1.98 za mbegu bora za Korosho ( Songwe tani 0.48 na Momba tani 1.5) kutoka TARI Naliendele Mtwara ili kuzalisha miche 137,200 (Songwe miche 67,200 na Momba miche 70,000 na kuigawa kwa wakulima bure.

### 5.16.4 Ubanguaji msimu wa 2025/2026 na mpango wa ubanguaji ifikapo msimu wa 2029/2030.

Msimu 2025/2026 kilo 5,650 za Korosho ghafi zitabanguliwa (Songwe 4,770 na Momba kilo 880) na kotoa jumla ya kilo 1,412.5 za karanga (Songwe kilo 1,192.5 na Momba kilo 220) na ifikapo msimu 2029/2030 katika Mkoa wa Songe jumla ya tani 22.11 za korosho ghafi zitabanguliwa ili kuzalisha tani 5.5 za karanga.

**Ubanguaji msimu wa 2025/2026.**

Msimu 2025/2026 kilo 5,650 za Korosho ghafi zitabanguliwa (Songwe 4,770 na Momba kilo 880) na kotoa jumla ya kilo 1,412.5 za karanga (Songwe kilo 1,192.5 na Momba kilo 220).

**Mpango/makadirio ya ubanguaji kiwilaya misimu ya 2026/2027, 2027/2028, 2028/2029 na 2029/2030.**

| Halmashauri | 2026/2027 (TANI) | 2027/2028 (TANI) | 2028/2029 (TANI) | 2029/2030 (TANI) |
|---|---|---|---|---|
| Songwe | 1.9 | 2.7 | 4.2 | 4.9 |
| Momba | 0.3 | 0.4 | 0.5 | 0.6 |
| **JUMLA** | **2.2** | **3.1** | **4.7** | **5.5** |

#### 5.16.5 Huduma za ugani, mafunzo na mpango wa msimu 2026/2027.

Huduma za Ugani zilizotolewa kwa wakulima;

i. Elimu ya ubanguaji wa korosho ili kuongeza thamani ya zao;
ii. Matumizi sahihi ya viuatilifu; na
iii. Mbinu bora za kilimo cha korosho.

#### 5.16.6 Changamoto zinazokabili shughuli za uendelezaji zao la korosho na mapendekezo ya utatuzi wake.

i. Ukosefu wa mfumo mzuri wa Soko la Korosho.
ii. Mifugo kuharibu miti ya mikorosho.
iii. Wadudu waharibifu na magonjwa ya korosho.
iv. Uhaba wa upatikanaji wa miche iliyothibitishwa ubora.
v. Ukame unaosababishwa na mabadiliko ya tabia ya nchi.

#### 5.16.7 Mapendekezo ya utatuzi wa changamoto.

i. Sheria ya kutochungia mifugo kwenye ardhi ya Kilimo isimamiwe ipasavyo na mifugo itengewe maeneo maalumu ya malisho.
ii. Bodi ya Korosho ipeleke ruzuku ya viuatilifu na Mbegu Mikoani kwa wakati ili viweze kuwafikia wakulima kwa wakati.

iii. Halmashauri zizalishe miche na kuigawa kwa wakulima bure badala ya kuwagawia mbegu wakulima.

iv. Kuendelea kuhamasisha wakulima kupanda mikorosho kila mwaka.

### 5.16.8 Mikakati ya kuendeleza zao la korosho ifikapo 2029/2030

i. Kuongeza uzalishaji wa Korosho kwa mti mmoja kutoka kilo 6-10 hadi kilo 35-40.

ii. Kuongeza uzalishaji wa miche ya Korosho iliyothibitishwa ubora kutoka miche 23,127 hadi miche 100,527.

iii. Kuhamasisha wakulima kulima zao la korosho.

iv. Kusimamia na kuhakikisha maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kilimo cha korosho yanapandwa mikorosho.

v. Kuwaelimisha wakulima kubangua korosho ili kuongeza thamani

vi. Kuunda vyama vya msingi vya zao la korosho ili kusimamia na masoko ya korosho.

### 5.16.9 Hitimisho

Korosho katika Mkoa wa Songwe ni zao la kimkakati na biashara hivyo Mkoa Umejipanga kuwaunganisha wakulima na wasambazaji wa mashine rahisi za kubangua korosho, ili wakulima walio anza kuvuna waweze kunufaika na zao hilo kwa kulibangua na kuwauzia wajasiliamali wadogo kwa lengo la kuimarisha soko.

## 5.17. TAARIFA YA MKOA WA KATAVI

### 5.17.1. Utangulizi

Mkoa wa Katavi ni miongoni mwa Mikoa Mipya iliyoanza kilimo cha zao la korosho. Mkoa ulianza rasmi kilimo cha korosho msimu wa kilimo 2017/2018 ambapo hadi sasa jumla ya wakulima 17,837 wamelima ekari 65,032 za mikorosho. Zao hili ni miongoni mwa mazao ya kimkakati ambalo Mkoa umeona unalojukumu la kuendelea kuhamasisha wadau mbalimbali kuweza kuwekeza ipasavyo katika kilimo cha zao hili.

Katika msimu wa 2021/2022 Mkoa ulipokea jumla ya kilo 4,233 za mbegu toka Bodi ya Korosho Tanzania na kuzigawa kwa Halmashauri zake zote ambazo ziliweza

kugawiwa kwa wakulima wapatao 1,000 kwa ajili ya kujazia miche iliyokufa na kuanzisha mashamba mapya ya korosho. Mbegu ziliweza kupandwa kwenye jumla ya ekari 7,597 hivyo kuongeza idadi ya hekta zilizopandwa zao la korosho hadi sasa kutoka ekari 65,032 hadi kufikia ekari 72,629. Msimu wa 2024/2025 Mkoa uligawa kwa wakulima miche 25,000 ya korosho. Msimu wa kilimo wa 2025/2026 Mkoa unatarajia kuzalisha na kugawa kwa wakulima miche 65,000. Aidha, katika msimu wa ununuzi wa 2024/2025 jumla ya kilo 41,100 za korosho ghafi zimakusanywa na kilo 5,000 kati ya hizo zimechakatwa na kuuzwa ndani na nje ya Mkoa.

### 5.17.2. Uzalishaji msimu wa 2024/2025 na mpango wa uzalishaji ifikapo msimu wa 2029/2030

**Uzalishaji msimu wa 2024/2025**

Katika msimu wa Uzalishaiji wa 2023/2024 Jumla ya kilo 3,600 za korosho ghafi zilizalishwa msimu. Uzalishaji mdogo ni kutokana na wakulima kushindwa kudhibiti ipasavyo wadudu na magonjwa ya zao la korosho.

**Mpango/Makadirio ya uzalishaji kwa Halmashauri msimu wa kilimo 2024/2025 hadi 2029/2030**

| **Makadirio ya Uzalishaji (Kilo) wa zao la Korosho kwa msimu wa 2024 hadi 2029** | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Halmashauri** | **2024/2025** | **2025/2026** | **2026/2027** | **2027/2028** | **2028/2029** | **2029/2030** | **Jumla (Kilo)** |
| Mlele DC | 7,520 | 9,400 | 11,750 | 14,688 | 18,359 | 22,949 | 84,666 |
| Mpanda MC | 8,940 | 11,175 | 13,969 | 17,461 | 21,826 | 27,283 | 100,654 |
| Mpimbwe DC | 6,880 | 8,600 | 10,750 | 13,438 | 16,797 | 20,996 | 77,460 |
| Nsimbo DC | 7,860 | 9,825 | 12,281 | 15,352 | 19,189 | 23,987 | 88,494 |
| Tanganyika DC | 9,900 | 12,375 | 15,469 | 19,336 | 24,170 | 30,212 | 111,462 |
| Jumla Kuu | 41,100 | 51,375 | 64,219 | 80,273 | 100,342 | 125,427 | 462,736 |

### 5.17.3. Mpango wa upatikanaji wa mbegu na miche bora ya Korosho

Katika msimu wa Kilimo wa 2025/2026 Mkoa unatarajia kununua kilo 450 za mbegu bora za Korosho na kuazalisha miche. Ambapo baada ya kuazalishwa wakulima watagaiwa bure kwa ajili ya uanzishaji wa mashamba mapya na kurudishia mashamba ya zamani.

### 5.17.4. Ubanguaji msimu wa 2024/2025 na mpango wa ubanguaji ifikapo msimu wa 2029/2030

#### 5.17.4.1. Ubanguaji msimu wa 2024/2025

Katika msimu wa Kilimo wa 2024/2025 kiasi cha kilo 6,165 kilichozalishwa na kubanguliwa katika kiwanda cha wakulima hakikuweza kubanguliwa kutokana na wakulima kusubiri ahadi ya bodi ya korosho kuja kununua kiasi walichozalisha. Hivyo inaelezwa kuwa bado korosho zalishwa bado zipo majumbani kwa wakulima.

#### 5.17.4.2. Mpango/makadirio ya ubanguaji kwa Halmashauri msimu wa 2024/2029 hadi 2029/2030

Katika kipindi cha misimu minne ijayo Mkoa unatarajia kuendelea kuhamasisha ubanguaji ili kuongeza thamani kiasi cha korosho zitakazo zalishwa kwa asilimia ishirini (20) sawa kilo 462,736 za korosho ghafi zinatarajiwa kubanguliwa. Kupitia mafunzo ya ubanguaji yatakayotolewa kwa wazalishaji wa zao la korosho kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania pamoja na Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Naliendele -TARI - Naliendele. Makadirio ya ubanguaji ni ufuatao:-

| Halmashauri | 2024/2025 | 2025/2026 | 2026/2027 | 2027/2028 | 2028/2029 | 2029/2030 | Jumla (Kilo) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mlele DC | 1,128 | 1,880 | 2,350 | 2,938 | 3,672 | 4,590 | 16,557 |
| Mpanda MC | 1,341 | 2,235 | 2,794 | 3,492 | 4,365 | 5,457 | 19,684 |
| Mpimbwe DC | 1,032 | 1,720 | 2,150 | 2,688 | 3,359 | 4,199 | 15,148 |
| Nsimbo DC | 1,179 | 1,965 | 2,456 | 3,070 | 3,838 | 4,797 | 17,306 |
| Tanganyika DC | 1,485 | 2,475 | 3,094 | 3,867 | 4,834 | 6,042 | 21,797 |
| **Jumla Kuu** | **6,165** | **10,275** | **12,844** | **16,055** | **20,068** | **25,085** | **90,492** |

### 5.17.5. Huduma za ugani na mafunzo

Mkoa katika uboresha wa huduma za ugani kwa zao la korosho wataalam wapatao 60 na wakulima 250 katika nyakati tofauti wamepatiwa mafunzo ya kanuni bora zao la korosho. Aidha, mwaka 2023 Madiwa wapatao 20 na wataalam 10 toka Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda walifanya ziara ya mafunzo Mkoani Mtwara kujifunza uzalishaji na uongezaji wa thamani wa zao la korosho.

Katika Misimu ijayo Mkoa utaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ndani na nje ya Mkoa ikiwemo Bodi ya Korosho Tanzania pamoja na Kituo cha Utafiti wa Kilimo - TARI -Naliendele katika kuendeleza utoaji wa huduma bora za ugani kwa wakulima wa zao la korosho ikiwemo

### 5.17.6. Uanzishaji wa mashamba darasa/mfano ya zao la korosho

i. Kutoa mafunzo rejea kwa maafisa ugani katika ngazi mbalimbali

ii. Kutoa mafunzo ya kanuni bora za zao la korosho kwa wakulima viongozi wa zao la korosho

iii. Kuanzisha vikundi vya uzalishaji/ubanguaji wa zao la korosho katika maeneo mbalimbali Mkoani.

iv. Kuhamasisha usafishaji na udhibiti wa wadudu na magonjwa katika mashamba ya mikorosho

v. Kuzisimamia Halmashauri katika kuanzisha sheria ndogo za udhibiti uingizaji wa mifugo na uchomaji moto katika mashamba ya mikorosho.

vi. Kusimami Halmashauri kuwezesha mafuta maafisa ugani ili kuweza kuwatembelea wakulima kwa wakati.

vii. Kuboresha madaftari ya wakulima wa zao la korosho katika maeneo mbalimbali Mkoani.

viii. Kuratibu upokeaji na usambazaji wa pembejeo za zao la korosho zanazoletwa toka Serikalini.

### 5.17.7. Changamoto zinazokabili shughuli za uendelezaji zao la korosho na mapendekezo ya utatuzi wake

Katika uendelezaji wa zao la korosho zipo changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikijitokeza kama ifuatavyo:-

i. Uelewa mdogo kwa viongozi, wataalam na wakulima juu ya kilimo cha zao la korosho

ii. Uelewa mdogo juu ya utambuzi na uthibiti wa wadudu na magojwa ya zao la korosho

iii. Uwezo mdogo wa wakulima kumudu gharama za pembejeo" Viuatilifu"

iv. Kuto kuwepo kwa sheria ndogo zinazodhibiti mifugo na uchomaji moto katika maeneo ya mashamba ya mikorosho.

v. Uwepo wa mashambulizi ya wadudu na magonjwa katika mashamba ya mikorosho

vi. Uelewa mdogo wa vyama vya ushirika juu ya usimamizi wa zao la korosho

vii. Uelewa duni juu ya mfumo wa masoko ya zao la korosho

viii. Kutokuwepo kwa viwanda vya kuchakata zao la korosho

ix. Kutokuwepo kwa mashamba darasa/mashamba ya mfano wa zao la korosho.

x. Kutokuwepo kwa vituo/maghala maalum ya kukusanyia korosho.

**5.17.8. Pamoja na kuwepo kwa changamoto hizi, bado zipo fursa mbalimbali za kuendeleza kilimo cha zao hili**:

i. Mkoa unashirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo wa Bodi ya Korosho Tanzania, TARI-Naliendele, Sekta binafsi na mashirika yanayotekeleza programu mbalimbali Mkoani ikiwepo programu za uhifadhi wa mazingira ya Tuungane pamoja na Vyama vya ushirika katika uzalishaji wa miche ya mikorosho, usambazaji kwa wakulima na uanzishaji wa mashamba ya pamoja ya vyama vya ushirika.

ii. Elimu ya uhudumiaji wa zao la korosho imeendelea kutolewa kwa wakulima/wadau mbalimbali waliowekeza katika mashamba ya mikorosho pamoja na wakulima hasa walopanda awali kuhudumia mikorosho yao ikiwemo usafishaji wa mashamba pamoja na udhibiti wa magonjwa na wadudu ili kuanza uzalishaji wa zao hili.

iii. Kushirikiana na wadau ikiwemo Bodi ya Korosho Tanzania, Kituo cha Utafiti wa Kilimo -TARI -Naliendele kutoa elimu ya ubanguaji/uongezaji thamani zao la korosho

iv. Kuendelea kusimamia mpango wa Serikali wa Usambazaji wa Viuatilufu bure kwa wakulima wa Korosho ili kuongeza tija na uzalishaji wa zao la korosho Mkoani.

v. Kuendeleza mpango wa mafunzo rejea kwa viongozi, wataalam na wakulima juu ya kilimo bora cha zao la korosho

vi. Kushirikiana na Bodi ya Korosho pamoja na Kituo cha Utafiti TARI- Naliendele kuanzisha mashamba darasa/mfano ya zao la korosho Mkoani

vii. Kujengea uwezo wa wanavikundi vya wakulima wa zao la korosho kupatiwa mashine za ubanguaji wa zao la korosho kupitia bodi ya korosho Tanzania.

#### 5.17.9. Hitimisho

Mkoa wa Katavi utaendelea kuhamasisha uzalishaji na uongezaji thamani zao la korosho na kuhakikisha zao hili linakuwa miongoni mwa mazao yanalotegemewa na wakulima wetu kiuchumi. Aidha, tunapenda kuishukuru Serikali kwa kutuunga mkono katika mpango wa ugawaji bure wa pembejeo" viuatilifu na mbegu za korosho kwa wakulima kwani imekuwa ni sehemu ya kuongeza chachu na hamasa kwa wakulima wetu kuendelea kulima zao hili. Vilevile tunaomba Bodi ya Korosho Tanzania itusaidie katika kuwajengea uwezo wataalam na wakulima viongozi katika udhibiti wa magonjwa na wadudu katika zao la korosho pamoja na matumizi ya zana za uongezaji thamani zao la koshoro Mkoa wa Katavi.

## 5.18. TAARIFA YA MKOA WA RUKWA

### 5.18.1. Utangulizi

Zao la Korosho ni miongoni mwa mazao ya biashara yaliyoanzishwa katika Mkoa. Zao hili limeanza kulimwa na wakulima wachache kuanzia mwaka 2018 katika vijiji vya Muze na Zimba katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga na Samazi katika Wilaya ya Kalambo. Zao la Korosho kulingana na hali ya hewa inayostahili linastawi zaidi katika ukanda wa ziwa Tanganyika na Ukanda wa Bonde la ziwa Rukwa kama ifuatavyo:-

i. Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi; Kata ya Kipili, Mkinga, Itete, Ninde, Kizumbi, Kala, Kabwe, Wampembe, Kirando na Korongwe.
ii. Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo; Kata ya Kisumba, Kasanga, Samazi, Mpombwe, Mkowe na Mambwenkoswe.

iii. Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga; Kata ya Muze, Mfinga, Kalumbaleza, Mwadui, Mtowisa, Zimba, Milepa, Ilemba, Nankanga, Kipeta, Kapenta, Kaoze, na Kilangawana.

### 5.18.2. Uzalishaji wa korosho msimu wa 2024/2025

Katika msimu wa 2024/2025 halmashauri za mkoa wa Rukwa zilizalisha jumla ya Tani 11.928 za korosho.

**Mpango wa uzalishaji wa korosho (tani) katika mkoa kwa kila Halmashauri kuanzia msimu wa 2025/26 hadi 2029/30.**

| Na | Halmashauri | 2025/26 | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SUMBAWANGA DC | 9.1 | 16.9 | 20.02 | 22.3 | 25.7 |
| 2 | NKASI DC | 12 | 15 | 19 | 24 | 30 |
| 3 | KALAMBO DC | 0.045 | 0.1 | 0.65 | 0.85 | 1.45 |
| JUMLA | | 21.145 | 32 | 39.67 | 47.15 | 57.15 |

### 5.18.3. Mpango wa upatikanaji wa mbegu na miche bora ya korosho.

Mkoa kupitia Halmashauri za Wilaya za Nkasi, Kalambp na Sumbawanga ilipokea mbegu na miche bora ya korosho kutoka Bodi ya korosho na kituo cha utafiti Naliendele msimu wa 2022/2023. kwa msimu wa 2025/2026 pia tunatarajia kuomba Mbegu na Miche bora kutoka kwenye Taasisi hizo na pia kutenga bajeti kwa mapato ya ndani.

### 5.18.4. Ubanguaji wa korosho kwa msimu wa 2025/26.

Kwa sasa wakulima walio wengi wanatumia njia ya asili kama mbinu ya kubangua korosho na mkoa unatarajia kuwaunganisha na SIDO ili kupata elimu na vifaa vya ubanguaji wa Korosho.

Mpango/makadirio ya ubanguaji wa korosho unatarajiwa kuwa kama ifuatavyo katika msimu wa2025/2026 tani 21.145, 2026/2027 tani 30, 2027/2028 tani 39.67,2028/2029 tani 47.15, na 2029/2030 tani 57.15.

#### 5.18.5. Hali ya huduma za ugani

Wakulima wa korosho katika mkoa wameendelea kupewa elimu ya kilimo cha korosho kutoka kwa maafisa ugani wa Halmashauri na wale wa Bodi ya Korosho. Mpango ni kutoa elimu kwa wakulima wapatao 300 juu ya utunzaji wa miti ya korosho, uoteshaji wa mbegu katika vitalu na ubanguajia wa korosho kwa kutumia mashine rahisi.

#### 5.18.6. Changamoto

i. Zao la korosho kutopewa kipaumbele katika mipango ya Halmashauri,

ii. Ufinyu wa bajeti inayotokana na mapato ya Halmashauri katika kuendeleza mazao ya kimkakati ikiwemo korosho.

iii. Mwitikio mdogo wa wakulima juu ya zao hili kwa sababu ya dhana iliyojengeka kwa wakulima ya zao hili kuchukua muda mrefu kuanza kutoa mavuno.

iv. Teknolojia duni inayotumika wakati wa kubangua korosho

v. Mikakati ya kukabiliana na changamoto.

vi. Kuendelea kuhimiza utengaji wa fedha unaotokana na mapato ya ndani

vii. Kuendelea kutoa hamasa na elimu kwa wakulima juu ya uzalishaji wa zao la korosho.

viii. Kuendelea kutoa elimu kwa wakulima juu ya mbinu bora na kanuni za kufuata ili kuweza kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

ix. Kuendelea kuhamasisha wadau katika kuwekeza kwenye viwanda vidogo sana vya kubangua korosho

x. Kutoa hamasa kwa wakulima kuongeza maeneo kwa ajili ya kilimo cha korosho na kuratibu mahitaji ya mbegu na kununua kutoka Bodi ya Korosho ya Tanzania.

xi. Kuhamasisha wakulima wa korosho kujiunga katika vyama vya ushirika ili kuweza kupata fursa za mikopo kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha korosho.

xii. Kufanya ziara ya mafunzo kwa viongozi, wataalam na wakulima kwenye maeneo yanayofanya vizuri katika kilimo cha korosho mfano Manyoni Singida.

xiii. Mikakati ya kuendeleza zao la korosho ifikapo 2029/2030.

xiv. Kwa kushirikiana na Halmashauri mkoa umejipanga kuvutia mashirika na wat binafsi kuleta teknolojia za ubanguaji wa korosho katika mkoa.

xv. Kutoa Mafunzo kwa wakulima 300 kuhusu zao la korosho katika halmashauri zote tatu zinazozalisha Korosho

xvi. Kuanzisha mashamba darasa katika kata ambazo zinauzalishaji mkubwa.

xvii. Kuanzisha Vyama vya ushirika maalum kwa ajili ya zao la korosho ili kurahisisha ununuzi na uuzaji wa zao hilo kupitia mifumo ya stakabadhi ghalani.

xviii. Kuendelea kushirikiana na wadau wa korosho ikiwemo Bodi ya Korosho Tanzania na vituo vya utafiti katika kuongeza uzalishaji na tija.

#### 5.18.7. Hitimisho:

Mkoa utaendelea kuratibu, kusimamia na kutoa elimu kwa wakulima juu ya Kilimo cha zao la korosho ili wakulima waweze kuongeza uzalishaji na kunufaika na uzalishaji wa korosho.

### 5.19. TAARIFA YA MKOA WA IRINGA

#### 5.19.1. Utangulizi

Mkoa wa Iringa ni miongoni mwa Mikoa yenye maeneo yanayofaa kwa uzalishaji wa zao la korosho kimkakati kwa lengo la kuendeleza zao hili. Halmashauri 2 ambazo ni Kilolo DC na Iringa DC zina maeneo yenye hali ya hewa inayoruhusu ustawi wa zao la korosho. Mikakati mbalimbali inatumika kuongeza tija katika uzalishaji wa zao la korosho ikiwa ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora za korosho, kutoa elimu ya uzalishaji bora wa korosho kwa wakulima na wapuliziaji wa viwatilifu, Kuhamasisha wakulima kuunda vikundi vya wazalishaji wa Korosho, wakulima kupata viuatilifu vya ruzuku vinavyotolewa na Bodi ya Korosho bila malipo na kuanzisha ubanguaji wa korosho.

#### 5.19.2. Hali ya Uzalishaji Msimu wa 2024/2025 na Mpango wa Uzalishaji Ifikapo Msimu wa 2029/2030

**Uzalishaji msimu wa 2024/2025**

Msimu wa kilimo 2024/2025 Mkoa ulifanikiwa kuzalisha tani 16.49 kwa mchanganuo ufuatao:

**Uzalishaji msimu 2024/2025**

| Na. | Halmashauri | Tani |
|---|---|---|
| 1 | Iringa DC | 13.99 |
| 3 | Kilolo DC | 2.5 |
| Jumla | | 16.49 |

**Mpango/makadirio ya uzalishaji msimu wa 2024/2025, 2025/2026 na 2026/2027, 2027/2028, 2028/2029 na 2029/2030.**

Makadirio ya Uzalishaji msimu 2024/2025 hadi 2029/2030

| Na. | Halmashauri | 2025/2026 | 2026/2027 | 2027/2028 | 2028/2029 | 2029/2030 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Tani | Tani | Tani | Tani | Tani |
| 1 | Iringa DC | 27.87 | 50.78 | 69.7 | 82.3 | 94.4 |
| 2 | Kilolo DC | 8.5 | 16.0 | 25 | 35 | 58 |
| Jumla | | 36.37 | 66.78 | 94.7164.78 | 117.3 | 152.4 |

**5.19.3. Mpango wa upatikanaji wa mbegu bora na miche bora ya korosho**

i. Kuandaa mahitaji ya mbegu bora za korosho kulingana na mahitaji ya wakulima kutoka katika Halmashauri zenye maeneo yanayofaa kwa kilimo cha Korosho.

ii. Kuwasilisha Bodi ya Korosho orodha ya mahitaji ya pembejeo na mbegu bora za korosho kwa msimu husika ili wakulima wapate Mbegu kwa wakati kulingana na mahitaji.

iii. Kutoa elimu ya upandaji bora wa miche na upandaji wa moja kwa moja wa mbegu za korosho kwa wakulima.

iv. Kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kujiridhisha na maendeleo ya zao kwa wakulima waliopata mbegu na viuatilifu kutoka Bodi ya Korosho

### 5.19.4. Hali ya Ubanguaji Mwaka 2025 na Mpango wa Ubanguaji Ifikapo 2029/2030

#### 5.19.4.1. Ubanguaji mwaka wa 2025/2026

Msimu wa kilimo 2024/2025 Halmashauri ya Iringa DC pekee ilifanikiwa kubangua kilo 850 kupitia mashine ndogo mbili zinazomilikiwa na wakulima katika kata ya Nzihi na Kiwere. Kiasi kinachosalia kilibanguliwa kwa njia za asili katika maeneo ya wazalishaji.

#### 5.19.4.2. Mpango/makadirio ya ubanguaji msimu 2025/2026, 2026/2027,2027/2028, 2028/2029 na 2029/2030.

Katika misimu 2025/26 hadi 2029/2030 Mkoa unatarajia kuendelea kufanya uhamasishaji wa vikundi na Wadau mbalimbali kuwekeza katika tasnia ya ubanguaji wa korosho kwa kutumia mashine rahisi zinazotengenezwa na Taasisi ya SIDO. Makadirio ya ubanguaji ni kama inavyoonyeshwa kwenye.

**Makadirio ya ubanguaji**

| **Na.** | **Halmashauri** | **2025/2026** | **2026/2027** | **2027/2028** | **2028/2029** | **2029/2030** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Tani** | **Tani** | **Tani** | **Tani** | |
| 1 | Iringa DC | 1 | 3.4 | 3.8 | 4.2 | 7.8 |
| 2 | Kilolo DC | 0.8 | 1.2 | 2.8 | 3.5 | 5.7 |
| **Jumla** | | **1.8** | **4.6** | **6.6** | **7.7** | **13.5** |

### 5.19.5. Huduma za ugani na mafunzo:

Katika kuhakikisha kuwa tija ya uzalishaji wa zao la korosho inaongezeka shughuli zifuatazo zitaendelea kutekelezwa;-

i. Kutoa elimu ya kilimo bora cha korosho kwa wakulima kupitia mikutano ya hadhara inayofanyika katika Vijiji husika kwa kupitia wataalamu wa kilimo wa Kata na vijiji.

ii. Kutoa elimu ya upuliziaji wa viwatilifu kwenye mikorosho kwa maafisa ugani na watoa huduma ya upuliziaji wa viuatilifu ili kusogeza huduma hiyo kwa wakulima.

iii. Kuhamasisha vyama vya ushirika vya mazao (AMCOS) kushiriki katika uzalishaji wa zao la korosho ili kuongeza uzalishaji.

iv. Kutoa elimu ya uzalishaji wa miche bora ya Korosho kwa wazalishaji ili kuhakikisha upatikanaji wa miche bora ya Korosho

v. Kuendelea kutoa mafunzo rejea kwa Maafisa Ugani wa maeneo yanayozalisha zao la korosho kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti ya Naliendele.

**5.19.6. Changamoto zinazokabili shughuli za uendelezaji zao la korosho na mapendekezo ya utatuzi wake**

i. Mwitikio mdogo kwa wakulima kuwekeza katika zao la korosho kutokana na Mabadiliko ya tabianchi yanayoathiri maendeleo ya korosho shambani kwani wakulima wengi hutegemea mvua kuendesha shughuli zao za kilimo.

ii. Kutokuwa na vyama vya ushirika vinavyojishughulisha na uzalishaji wa zao la Korosho.

iii. Kutokuwa na wanunuzi wanaoshirikiana na wataalamu katika uhamasishaji na ununuzi wa kiasi kidogo kinachozalishwa na wakulima.

iv. Mifugo na wanyama pori kutoka Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kushambulia na kuleta uharibifu wa mikorosho.

**5.19.7. Mapendekezo ya utatuzi wa changamoto**

i. Kuwezesha wakulima na wataalamu kutoka katika mikoa mipya kufanya ziara za mafunzo kwenye mikoa mikongwe ili kujifunza zaidi na kuona mafanikio yatokanayo na zao la korosho.

ii. Bodi ya korosho kusambazwa mbegu kwa wakulima badala ya miche maana baadhi ya wakulima wamekiri kuwa wakipanda mbegu zinafanya vizuri kuliko miche.

iii. Kuendelea kutoa elimu ya matumizi ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho badala ya kuingiza mifugo kwenye maeneo ya mashamba ya wakulima.

iv. Kuendelea kuwashauri wakulima wa korosho kuzungushia uzio kwenye mashamba yao ili kuepuka athari zinazotokana na wanyama pori na mifugo.

v. Bodi ya korosho iwezeshe upatikanaji wa mashine rahisi za kubangua korosho katika mikoa mipya kipindi hiki ambacho uzalishaji ni mdogo.

vi. Kuhamasisha uanzishaji wa vikundi vitakavyowekeza katika uzalishaji na ubanguaji wa korosho.

### 5.19.8. Hitimisho.

Tunaishukuru Bodi ya Korosho kwa kuendelea kutoa pembejeo hususan viuatilifu kwa wakulima bila malipo, hii inaleta hamasa kwa wakulima wanaolima zao la Korosho pamoja na kuvuta wakulima wengine kuwekeza katika kilimo cha zao la Korosho. Aidha, uhamasishaji wa wakulima zaidi kuingia kwenye kilimo cha Korosho unaendelea ili kuongeza wigo wa mazao ya kibiashara kwa ajili ya kuboresha kipato cha wakazi na Mkoa kwa ujumla.

**AGENDA NA. 6: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA UENDELEZAJI ZAO LA KOROSHO MSIMU WA 2024/2025 NA MIPANGO KUELEKEA MSIMU WA 2025/2026 KUTOKA BODI YA KOROSHO TANZANIA**

**KUPOKEA NA KUPITIA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA UENDELEZAJI WA ZAO LA KOROSHO MSIMU WA 2024/2025 NA MIPANGO KUELEKEA MSIMU 2025/2026 KUTOKA BODI YA KOROSHO TANZANIA**

## 6.1. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA UENDELEZAJI ZAO LA KOROSHO MSIMU WA 2024/2025

### 6.1.1. Utangulizi

Katika msimu wa 2024/2025 shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:

i. Uhuishaji wa kanzidata ya wakulima wa korosho.
ii. Usambazaji wa viuatilifu na mabomba kwa wakulima.
iii. Mafunzo ya kilimo bora cha zao la korosho pamoja na matumizi sahihi na salama ya viuatilifu.
iv. Uimarishaji wa upatikanaji wa huduma za ugani kwa wakulima (BBT Korosho).
v. Usambazaji wa mbegu na miche bora ya zao la korosho.
vi. Uhamasishaji na usimamizi wa mashamba makubwa ya pamoja ya zao la korosho.
vii. Mafunzo ya ubanguaji wa korosho na usindikaji wa bidhaa zitokanazo na korosho.
viii. Ujenzi wa kongani la viwanda vya kubangua korosho katika eneo la Maranje mkoani Mtwara.

### 6.1.2. Uhuishaji wa kanzidata ya wakulima wa korosho

Katika msimu wa mwaka 2024/2025 zoezi la uhuishaji wa kanzidata ya wakulima wa korosho nchini liliendelea kwa kuchukua taarifa za mkulima, picha ya mkulima, idadi ya ekari, idadi ya miti ya mikorosho, namba ya simu na taarifa nyingine zinazomhusu mkulima. Zoezi la uhuishaji wa kanzidata lilianza tarehe 25 Februari, 2025 hadi Mei, 2025 kwa mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma na Pwani; na Mei hadi Juni, 2025 kwa mkoa wa Tanga. Lengo lilikuwa kuhuisha wakulima 600,000 ambapo kati ya hao waliohuishwa ni wakulima 549,936 sawa na 91.66% ya lengo. Jedwali hapa chini linaonesha takwimu za uhuishaji wa kanzidata ya wakulima wa korosho nchini kwa mwaka 2025.

**Takwimu za uhuishaji wa kanzidata ya wakulima wa korosho kutoka mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani na Tanga kwa mwaka 2025.**

| Na. | Mkoa | Idadi ya Wakulima | Ekari | Idadi ya Mikorosho |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mtwara | 335,543 | 2,336,830.73 | 70,104,922 |
| 2. | Lindi | 127,260 | 1,221,922.07 | 36,657,662 |
| 3. | Ruvuma | 57,041 | 736,200.13 | 22,086,004 |
| 4. | Pwani | 26,800 | 258,219.37 | 7,746,581 |
| 5. | Tanga | 3,292 | 14,038.00 | 421,164 |
| **Jumla** | | **549,936** | **4,567,210.30** | **137,016,333** |

### 6.1.3. Usambazaji wa Viuatilifu na Mabomba kwa Wakulima

Kwa mara ya tano mfululizo kuanzia msimu wa mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026; Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kutoa pembejeo bure kwa wakulima wa korosho nchini ili kuwapunguzia gharama za kulima zao la korosho hususani katika udhibiti wa magonjwa na wadudu waharibifu wa zao hilo. Pembejeo hizo hununuliwa na Mradi wa Pamoja wa Vyama Vikuu vya Ushirika (KCJE) vinavyohusika na zao la korosho kutoka mikoa ya Mtwara (MAMCU Ltd na TANECU Ltd), Lindi (RUNALI Ltd na LMCU Ltd), Ruvuma (TAMCU Ltd) na Pwani (CORECU Ltd). Hadi kufikia tarehe 03 Agosti, 2025 *sulphur* ya unga tani 151,083.20, viuatilifu vya maji lita 10,705,882.18 na mabomba ya kupulizia/kunyunyiza *(Motorized blowers)* 6,337 vimesambazwa kwa wakulima vikiwa na thamani ya jumla ya Shilingi 753,707,352,403.98. Jedwali hapo chini linaonesha takwimu za viuatilifu na mabomba yaliyosambazwa kwa wakulima kuanzia msimu wa 2021/2022 hadi 2025/2026 kuishia tarehe 03 Agosti, 2025.

**Takwimu za viuatilifu na mabomba yaliyosambazwa kwa wakulima kuanzia msimu wa 2021/2022 hadi 2025/2026 kuishia tarehe 03 Agosti, 2025.**

| MSIMU | SULPHUR | VIUATILIFU VYA MAJI | MABOMBA YA KUPULIZIA | JUMLA YA THAMANI (TSHS) |
|---|---|---|---|---|
| 2021/2022 | 13,561.68 | 1,497,354.00 | 121.00 | 59,489,171,000.00 |
| 2022/2023 | 15,015.02 | 2,684,470.50 | 1,216.00 | 96,836,379,300.00 |
| 2023/2024 | 39,244.00 | 1,952,282.00 | 5,000.00 | 191,490,745,288.00 |
| 2024/2025 | 41,263.00 | 2,689,581.00 | - | 208,902,762,215.98 |
| 2025/2026 | 41,999.50 | 1,882,194.68 | - | 196,988,294,600.00 |
| **JUMLA KUU** | **151,083.20** | **10,705,882.18** | **6,337.00** | **753,707,352,403.98** |

Aidha, katika msimu wa 2025/2026; mpango uliokuwepo ni kusambaza tani 40,000 za *sulphur* ya unga na lita 3,000,000 za viuatilifu vya maji (lita 1,200,000 za kudhibiti wadudu na lita 1,800,000 za kudhibiti magonjwa). Hadi kufikia tarehe 03 Agosti, 2025; utekelezaji ni kama ifuatavyo; sulphur tani 41,999.50 sawa na 105%, viuatilifu vya kudhibiti wadudu lita 718,726.68 sawa na 60% na viuatilifu vya maji vya magonjwa lita 1,163,468 sawa na 65%. Kwa mujibu wa kalenda ya upuliziaji shughuli ya usambazaji wa viuatilifu linatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 30 Agosti, 2025 isipokuwa Mkoa wa Tanga ambao zoezi litaendelea hadi tarehe 30 Septemba, 2025.

#### 6.1.4. Usambazaji wa Mbegu na Miche Bora ya Zao la Korosho

Katika msimu wa 2024/2025 Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na TARI Naliendele imesambaza miche bora ya korosho 766,986 katika Halmashauri 26 za Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Ruvuma. Aidha, mbegu bora za korosho Kg 11,710 zenye uwezo wa kuzalisha miche 1,639,400 zimesambazwa katika Mikoa ya Singida, Dodoma na Tanga. Jedwali hapa chini linaonesha takwimu za usambazaji wa mbegu na miche bora ya mikorosho kuanzia msimu wa 2021/2022 hadi 2024/2025.

**Takwimu za usambazaji wa mbegu na miche bora ya mikorosho kuanzia msimu wa 2021/2022 hadi 2024/2025.**

| Msimu | Mbegu (Kg) | Miche (Idadi) | Thamani ya Mbegu (Tshs) | Thamani ya Miche (Tshs) | Jumla ya Thamani ya Mbegu na Miche |
|---|---|---|---|---|---|
| 2021/2022 | 91,764 | - | 458,820,000.00 | - | 458,820,000.00 |
| 2022/2023 | 23,490 | 3,288,600 | 117,450,000.00 | 1,644,300,000.00 | 1,761,750,000.00 |
| 2023/2024 | 30,380 | 103,858 | 151,900,000.00 | 51,929,000.00 | 203,829,000.00 |
| 2024/2025 | 11,710 | 766,986 | 58,550,000.00 | 383,493,000.00 | 442,043,000.00 |
| **Jumla** | **157,344** | **4,159,444** | **786,720,000.00** | **2,079,722,000.00** | **2,866,442,000.00** |

#### 6.1.5. Mafunzo ya kilimo bora cha zao la korosho pamoja na matumizi sahihi na salama ya viuatilifu

Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na TARI Naliendele na Mamlaka za Serikali ngazi ya Mikoa na Wilaya zinazolima zao korosho nchini zimeendesha mafunzo ya kilimo bora cha korosho ikiwa ni pamoja na matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa wataalam wa kilimo waliopo ngazi ya Kata na Vijiji ikijumuisha maafisa kilimo waliopo kwenye kwa programu ya Jenga Kesho Iliyobora katika zao la korosho (BBT Korosho). Jumla ya wataalam wa kilimo 408 kutoka mikoa ya

Mtwara, Lindi na Singida wamepatiwa mafunzo hayo. Utekelezaji unatarajia kuendelea kwa mikoa mingine iliyobaki ikiwemo Ruvuma, Pwani, Tanga, Morogoro, Shinyanga, Mbeya, Katavi, Rukwa, Dodoma, Kagera (Biharamulo), Njombe, Iringa, Kigoma na Tabora.

#### 6.1.6. Uimarishaji wa upatikanaji wa huduma za ugani kwa wakulima (BBT Korosho)

Ili kusogeza huduma za ugani kwa wakulima wa zao la korosho kwa mwaka 2024/2025, wataalam wa kilimo 500 kupitia programu ya Jenga Kesho Iliyobora wamepangwa katika Kata zenye fursa kubwa ya kuongeza uzalishaji korosho kutoka mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani na Tanga. Ili waweze kutekeleza majukumu ya kuwahudumia wakulima kwa ufasaha Bodi ya Korosho Tanzania imewawezesha vitendea kazi ikiwemo pikipiki na vishikwambi kwa ajili ya usafiri na ukusanyaji wa taarifa za wakulima. Uwepo wa wataalam wa kilimo wa BBT umesaidia kutatua changamoto za zoezi la uhuishaji wa kanzidata na usambazaji wa pembejeo kwa wakulima sanjari na kuwapatia elimu ya matumizi sahihi na salama viuatilifu. Jedwali hapo chini linaonesha mchanganuo wa idadi ya wataalam wa kilimo wa BBT korosho waliopo kazini katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani na Tanga.

**Mchanganuo wa idadi ya wataalam wa kilimo wa BBT korosho waliopo kazini katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani na Tanga.**

| Na. | Mkoa | Idadi ya Wataalam wa Kilimo wa BBT | Idadi ya Pikipiki | Idadi ya Vishikwambi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mtwara | 245 | 245 | 245 |
| 2. | Lindi | 153 | 153 | 153 |
| 3. | Ruvuma | 50 | 50 | 50 |
| 4. | Pwani | 29 | 29 | 29 |
| 5. | Tanga | 23 | 23 | 23 |
| **Jumla** | | **500** | **500** | **500** |

### 6.1.7. Uhamasishaji na Usimamizi wa Mashamba Makubwa ya pamoja ya zao la korosho *(Block farms)*

Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na TARI Naliendele na Mamlaka za Serikali ngazi ya Mikoa na Wilaya imeendelea kusimamia na kufuatilia kwa kukaribu mashamba makubwa ya pamoja yaliyopo Manyoni Mkoani Singida na Manispaa ya Lindi Mkoani Lindi. Wilaya ya Manyoni ina jumla ya ekari 23,000 za mashamba ya pamoja na Manispaa ya Lindi ekari 52,000. Pia, Bodi ya Korosho Tanzania imeanza kuendeleza shamba la pamoja la zao la korosho lililopo Kijiji cha Nyawanje-Ngwembele Kata ya Chemchem katika Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji Mkoa wa Pwani lenye ukubwa wa ekari 6,500.

### 6.1.8. Mafunzo ya Ubanguaji wa Korosho na Usindikaji wa Bidhaa zitokanazo na Korosho

Mafunzo ya ubanguaji yametolewa kwa wabanguaji na wakulima 1,504 wa mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani, Mbeya, Tanga, Songwe na Katavi. Pamoja na mafunzo haya pia zilitolewa jumla ya mashine 66 kwa vikundi vya ubanguaji na usindikaji wa korosho na bidhaa zake.

### 6.1.9. Ujenzi wa Kongani la Viwanda vya Kubangua Korosho Eneo la Maranje Mkoani Mtwara

Ujenzi wa Kongani la Viwanda Maranje umeendelea kutekelezwa ambapo miradi iliyofanyika kwa mwaka 2024/2025 ni ujenzi wa ghala 2 zenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 20,000 za mazao, utafiti na chimbaji wa maji, kufunga mfumo wa umeme kwenye eneo la mradi, kujenga barabara ya urefu wa km 7.5 kwa kiwango cha changarawe na kufanya tathmini ya mazingira.

## 6.2. MIPANGO YA MSIMU WA MWAKA 2025/2026 KUTOKA BODI YA KOROSHO

Katika msimu wa mwaka 2025/2026 Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na wadau imepanga kutekeleza mipango ya kuendeleza zao la korosho nchini kama ifuatavyo:-

i. Uboreshaji wa kanzidata ya wakulima wa zao la korosho.
ii. Usambazaji wa viuatilifu vya ruzuku vya zao la korosho.
iii. Mafunzo ya kilimo bora cha zao la korosho.

iv. Uimarishaji wa upatikanaji wa huduma za ugani kwa wakulima (BBT Korosho).
v. Uzalishaji na usambazaji wa miche bora ya zao la korosho.
vi. Usimamizi wa mashamba makubwa ya pamoja ya zao la korosho.
vii. Mafunzo ya ubanguaji wa korosho na usindikaji wa bidhaa zitokanazo na korosho.
viii. Ujenzi wa Kongani ya Viwanda vya Kubangua Korosho katika Eneo la Maranje Mkoani Mtwara.

### 6.2.1. Mpango wa Uboreshaji wa Kanzidata ya Wakulima wa Zao la Korosho Nchini

Katika msimu wa mwaka 2025/2026 Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na wadau wakiwemo Wizara ya Ardhi ***(National Land Use Planning Commission)***, Wizara ya Kilimo, Sekretarieti za Mikoa, Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Halmashauri, Vyama vya Ushirika vya Msingi na Vikuu itatekeleza mpango wa uboreshaji wa kanzidata ya wakulima wa korosho kwa kupima ardhi ya shamba, kupiga picha ya mkulima na kuhesabu idadi ya mikorosho ambapo mwishowe kila mkulima aliyefikiwa atapatiwa hati ya shamba. Mpango huu pamoja na mambo mengine unakuja kuondoa changamoto ya mashamba kujirudia kwenye kanzidata iliyopo na hatimaye kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa mipango mingine kama vile usambazaji na ugawaji wa pembejeo za ruzuku. Jedwali lifuatalo linaonesha makadirio ya bajeti ya mpango wa uboreshaji wa kanzidata ya wakulima wa zao la korosho nchini.

**Makadirio ya bajeti ya mpango wa uboreshaji wa kanzidata ya wakulima wa zao la korosho nchini kwa mwaka 2025/2026.**

| Na. | Shughuli | Makadirio ya Gharama (Tshs.) |
|---|---|---|
| 1. | Shajala | 64,000,000.00 |
| 2. | Mavazi kinga | 20,000,000.00 |
| 4. | Diesel | 281,998,500.00 |
| 5. | Vifaa | 4,422,500.00 |
| 6. | Upimaji wa ardhi ya mashamba | 12,260,000,000.00 |
| 7. | Usajili | 648,000,000.00 |
| 8. | Posho ya kujikimu (Per Diem) | 3,960,000,000.00 |
| 9. | Posho kazi za ziada (Extra Duty) | 108,000,000.00 |
| | **Jumla (Tshs.)** | **17,346,421,000.00** |

### 6.2.2. Mpango wa Usambazaji wa Viuatilifu vya Ruzuku vya Zao la Korosho

Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushikiriana na wadau inaendelea kuratibu upatikanaji wa viuatilifu vinavyotolewa bure kwa wakulima. Mpango huu kama ilivyoada unatekelezwa na Mradi wa Pamoja wa Vyama Vikuu vya Ushirika (KCJE). Aidha, kwa mujibu wa mikataba iliyofungwa baina ya KCJE na wazabuni; *sulphur* ya unga ni tani 69,000, viuatilifu vya maji lita 9,000,000 na magunia 9,000,000. Viuatilifu na magunia hayo ni kwa ajili ya kutosheleza misimu miwili ambayo ni 2025/2026 na 2026/2027. Jedwali hapo chini linaonesha makadirio ya bajeti ya mpango wa usambazaji wa viuatilifu vya zao la korosho.

**Makadirio ya bajeti ya mpango wa usambazaji wa viuatilifu vya ruzuku vya zao la korosho**

| Na. | Shughuli | Makadirio ya Gharama (Tshs.) |
|---|---|---|
| 1. | Ununuzi wa Viuatilifu | 74,466,000,000.00 |
| 2. | Usimamizi wa usambazaji wa pembejeo | 1,134,000,000.00 |
| | **Jumla** | **75,600,000,000.00** |

### 6.2.3. Mpango wa Mafunzo ya Kilimo Bora cha Zao la Korosho

Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana TARI Naliendele, MATI Mtwara na wadau wengine imepanga kutoa mafunzo kwa maafisa ugani, wakulima na wapuliziaji kwa kuzingatia kalenda ya kilimo cha zao la korosho nchini. Mafunzo hayo yataambatana na kampeni za kuhamasisha uzingatiwaji wa kanuni za kilimo bora cha zao la korosho. Aidha, kampeni hiyo itahusisha mikutano na wakulima katika ngazi ya vijiji kwa lengo la kubadilishana uzoefu. Jedwali lifuatalo linaonesha makadirio ya bajeti ya mpango wa mafunzo ya kilimo bora cha zao la korosho kwa mwaka 2025/2026.

**Makadirio ya bajeti ya mpango wa Mafunzo ya Kilimo Bora cha Zao la Korosho kwa Mwaka 2025/2026.**

| Na. | Shughuli | Makadirio ya Gharama (Tshs.) |
|---|---|---|
| 1. | Posho ya Mafunzo *(Facilitation allowance)* | 95,200,000.00 |
| 2. | Chakula na viburudisho | 38,250,000.00 |
| 3. | Shajala | 8,000,000.00 |
| 4. | Posho ya kujikimu *(Per Diems)* | 200,000,000.00 |
| | **Jumla** | **341,450,000.00** |

#### 6.2.4. Mpango wa Upatikanaji wa Huduma za Ugani kwa Wakulima

Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa imepanga kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma bora za ugani kwa wakulima. Lengo la mpango huu ni kuhakikisha kuwa kila mkulima anafikiwa na huduma za ugani kwa kuanzisha mashamba ya mfano kila kijiji na kuwa na mkulima mmoja kiongozi *(Lead farmer)* kwa kila kijiji kinacholima zao la korosho. Aidha, utekelezaji wa mpango huu utaenda sambamba na programu ya BBT ugani kwa kipindi cha miezi sita ya kwanza ya mwaka wa fedha wa 2025/2026.

**Makadirio ya Bajeti ya Mpango wa Upatikanaji wa Huduma za Ugani kwa Wakulima.**

| Na. | Shughuli | Makadirio ya Gharama (Tshs.) |
|---|---|---|
| 1. | Chakula na Viburudisho | 21,250,000.00 |
| 2. | Shajala | 30,000,000.00 |
| 3. | Posho | 277,500,000.00 |
| | **Jumla** | **328,750,000.00** |

#### 6.2.5. Mpango wa Uzalishaji na Usambazaji wa Miche Bora ya Korosho

Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na TARI Naliendele na Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya imepanga kuzalisha miche bora ya mikorosho 3,000,000 kwa kutumia vikundi vya vijana na wanawake, Vyama vya Ushirika na taasisi zisizo za Serikali. Lengo kuu la mpango huu ni kuongeza uzalishaji wa korosho ghafi kufikia tani 1,000,000 ifikapo mwaka 2029/20230.

**Makadirio ya bajeti ya mpango wa kuzalisha na kusambaza miche bora ya korosho**

| Na. | Shughuli | Makadirio ya Gharama (Tshs.) |
|---|---|---|
| 1. | Mafunzo ya kuzalisha miche ya korosho kwa wazalishaji | 178,835,500.00 |
| 2. | Kuwasilisha rasimu ya mwongozo wa uzalishaji wa miche msimu 2025/2026 | 147,175,500.00 |
| 3. | Mafunzo ya kutumia mfumo wa kidijitali maafisa ugani kata na BBT | 15,860,000.00 |
| 4. | Kutambua vikundi vitakavyohusika kuzalisha miche ya korosho | 166,130,000.00 |
| 5. | Kununua vifaa vya kuzalishia miche bora ya korosho. | 80,000,000.00 |
| 6. | Kusafirisha, kupakia na kushusha vifaa vya kuoteshea miche ya korosho | 34,000,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| 7. | Kununua mbegu bora za korosho. | 105,000,000.00 |
| 8. | Kusafirisha, kupakia na kushusha mbegu za korosho. | 46,000,000.00 |
| 9. | Gharama za kuzalisha miche bora ya korosho | 1,200,000,000.00 |
| 10. | Ufuatiliaji na Tathmini ya utekelezaji wa mpango | 121,000,000.00 |
| 11. | Dharura (5% ya gharama za mpango) | 104,700,050.00 |
| **Jumla (Tshs.)** | | **2,198,701,050.00** |

#### 6.2.6. Mpango wa Usimamizi wa Mashamba Makubwa ya Pamoja ya Zao la Korosho *(Block farms)*

Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na TARI Naliendele na Mamlaka za Serikali ngazi ya Mikoa na Wilaya itaendelea kusimamia mashamba makubwa ya pamoja yaliyoanzishwa katika Halmashauri za Wilaya ya Manyoni, Manispaa ya Lindi na Wilaya ya Rufiji. Jedwali hapo chini linaonesha makadirio ya bajeti ya mpango wa mashamba makubwa ya pamoja ya zao la korosho (*Block farms*).

**Makadirio ya Bajeti ya Mpango wa Mashamba Makubwa ya Pamoja ya zao la Korosho.**

| Na | Shughuli | Makadirio ya Gharama (Tshs.) |
|---|---|---|
| 1. | Vibarua | 336,000,000.00 |
| 2. | Mbegu | 282,240,000.00 |
| 3. | *Outsource maintenance contract* | 3,494,400,000.00 |
| | **Jumla (Tshs.)** | **4,112,640,000.00** |

#### 6.2.7. Mpango wa Mafunzo ya Ubanguaji wa Korosho na Usindikaji wa Bidhaa Zitokanazo na Korosho

Katika mwaka 2025/2026 mafunzo yatatolewa kwa wabanguaji wa mikoa yote inayolima korosho vikiwemo vikundi na mtu mmoja mmoja. Lengo la mafunzo haya ni kuwaweza kuzalisha bidhaa zinazokidhi mahitaji ya soko. Lengo ni kutoa mafunzo kwa washiriki 2,500.

#### 6.2.8. Mpango wa Kongani la Viwanda vya Kubangua Korosho Maranje Mkoani Mtwara

Katika mwaka 2025/2026 miradi itakayotekelezwa ni ujenzi wa kiwanda cha kubangua korosho tani 30,000 kwa mwaka, kujenga ukuta wa waya kuzunguka eneo la mradi ukiwa na urefu wa km 11, kujenga kituo cha afya, kujenga barabara

kuzunguka eneo la ekari 1,208 ikiwa na urefu wa km 12 na kukamilisha majadiliano na wawekezaji ili kuwapatia maeneo kwa ajili ya ujenzi wa viwanda.

**Makadirio ya bajeti ya mpango wa ujenzi wa kongani la viwanda vya kubangua korosho Maranje Mkoani Mtwara**

| Na. | Shughuli | Makadirio ya Gharama (Tshs.) |
|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa kiwanda | 5,000,000,000.00 |
| 2. | Ujenzi wa ukuta wa waya | 1,200,000,000.00 |
| 3. | Ujenzi wa kituo cha afya | 620,000,000.00 |
| 4 | Ujenzi wa barabara ya urefu wa km 12 | 700,000,000.00 |
| | **Jumla (Tshs.)** | **7,520,000,000.00** |

### 6.2.9. Changamoto na Mapendekezo ya Utatuzi

Pamoja na taarifa ya utekelezaji ya msimu wa 2024/2025 kama ilivyoelezwa hapo juu changamoto zifuatazo zilikabiliwa:-

**Changamoto na Mapendekezo ya Utatuzi**

| Na. | Changamoto | Mapendekezo ya Utatuzi | Mhusika |
|---|---|---|---|
| 1. | Baadhi ya wakulima kutohuisha taarifa zao za mashamba ya mikorosho kwa wakati, na baadae kutoa malalamiko ya kukosa mgao wa pembejeo | Kuhamasisha wakulima kuhuisha taarifa zao za mashamba kwa wakati | CBT, LGAs, Wakulima |
| 2. | Baadhi ya wakulima kutoa taarifa za uongo wakati wa uhuishaji wa taarifa zao. | Kushirikiana na Wizara ya Ardhi kupima ardhi na kutoa hati kwa kila mkulima. | CBT |
| 3. | Kuchelewa kusambazwa kwa viuatilifu vya maji vya kudhibiti magonjwa na wadudu waharibifu. | Kuagiza viuatilifu vya maji vya kutosheleza misimu miwili kama inavyofanyika kwa upande wa kiuatilifu cha sulphur ya unga. | KCJE na Wazabuni |
| 4. | Kutozingatiwa kwa matumizi sahihi ya viuatilifu hususani kuchanganya mipulizo kwa kuhusisha viuatilifu vya maji vya kudhibiti wadudu na magonjwa. | Elimu ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa kuzingatia kalenda ya zao iendelee kutolewa kwa wakulima | CBT, TARI, LGAs. |
| 5. | Mashamba pori. | Sheria ndogo *(By-laws)* za kuondoa mashamba pori zilizopo katika Halmashauri zisimamiwe ipasavyo. | RS, LGAs, CBT, TARI, Union, Wakulima |
| 6. | Mikorosho iliyozeeka. | Mpango wa kuboresha mikorosho hiyo kwa kubebesha *(Top-working)* ufanyike. | CBT, TARI, RS na LGAs |

### 6.2.10. Hitimisho

Bodi ya Korosho Tanzania inazishukuru Taasisi wadau pamoja na wadau wengine wote wa Tasnia ya korosho kwa ushirikiano wao uliowezesha kwa namna moja ama nyingine kufanikisha utekelezaji wa shughuli zilizokuwa zimepangwa ili kufikia malengo mama yaliyowekwa na Serikali ya kuongeza uzalishaji kufikia Tani 700,000 Mwaka 2025/2026 na tani 1,000,000 mwaka 2029/2030 ili kufikia agenda 10/30.

**AGENDA NA 7.0: KUPITIA NA KUJADILI JUU YA MWENENDO WA MASOKO YA KOROSHO KWA MSIMU WA MWAKA 2024/2025 NA MAANDALIZI YA MWAKA 2025/2026**

## 7. KUPITIA NA KUJADILI JUU YA MWENENDO WA MASOKO YA KOROSHO KWA MSIMU WA MWAKA 2024/2025 NA MAANDALIZI YA MWAKA 2025/2026

### 7.1.1. Mwenendo wa masoko kwa msimu wa 2024/2025

Msimu wa masoko na mauzo ya Korosho ghafi nchini kwa mwaka 2024/2025 ulizinduliwa rasmi tarehe 23 Agosti, 2024 kupitia Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wadau wa Tasnia ya Korosho nchini uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa PSSSF – Mkoa wa Dodoma na ulifunguliwa rasmi tarehe 1 Septemba, 2024 na minada ya mauzo ya korosho ghafi iliyoanza tarehe 11 Oktoba, 2024. Jumla ya leseni 82 za ununuzi wa Korosho ghafi zilitolewa kwa wanunuzi kwa ajili ya kusafirisha korosho nje ya nchi, idadi hii ikiwa ni ongezeko la kampuni 6 ukilinganisha na wanunuzi 76 waliopata leseni katika msimu 2023/2024. Jumla ya leseni 44 zilitolewa kwa wabanguaji wa ndani kupitia utaratibu wa soko la awali wenye lengo la kuwawezesha kupata malighafi ya viwanda vyao kwa urahisi kupitia vyama vya ushirika vya msingi (AMCOS). Huku leseni 81 zikiwa zimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa korosho zilizobanguliwa (korosho karanga).

### 7.1.2. Makusanyo na mauzo ya korosho ghafi msimu wa 2024/2025

Hadi kufikia tarehe 1 Agosti, 2025 jumla ya minada 75 imefanyika na korosho ghafi kiasi cha tani 409,075.062 zimekusanywa na kuuzwa katika ghala za minada zikiwa na thamani ya shilingi 1,469,036,244,102 ambapo daraja la kwanza ni tani 390,359.534 zenye thamani ya Shilingi 1,421,684,143,553.60 na daraja la pili tani 18,715.534 zenye thamani ya Shilingi 47,460,530,408.60. Aidha, kupitia Soko la Awali mauzo ni tani 10,029.281 zenye thamani ya shilingi 25,073,202,500 na zilizobanguliwa na wanguaji wadogo ni tani 33,134.361 zenye thamani ya wastani wa shilingi 82,835,902,500. Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na TARI Naliendele na Mamlaka za Serikali ya Mitaa na Vyama Vikuu vya Ushirika ilifanya utafiti na kubaini kiasi cha korosho ghafi zilizobaki majumbani kwa ajili ya kujumuishwa kwenye takwimu za mwisho za uzalishaji wa korosho ghafi Kitaifa kwa msimu wa 2024/2025. Kwa mujibu wa utafiti huo korosho ghafi zilizouzwa kupitia mifumo rasmi (TMX, Soko la Awali na Wabanguaji wadogo) ni tani 452,238.704 na zilizobaki majumbani kwa ajili ya matumizi mbalimbali ni tani 76,025.116. Hivyo, takwimu za mwisho za uzalishaji wa korosho ghafi Kitaifa kwa msimu wa 2024/2025 ni tani 528,263.820 zenye thamani ya shilingi 1,493,995,760,028 sawa na ongezeko

la asilimia 70% ikilinganishwa na uzalishaji wa korosho ghafi msimu wa 2023/2024 ambapo iliishia tani 310,787.17

**Mwenendo wa ukusanyaji na mauzo ya korosho ghafi**

| NA. | MKOA | VYAMA VIKUU | KIASI KILICHOKUSANYWA (TANI) | KIASI KILICHOUZWA KUPITIA MINADA (TANI) | KIASI KILICHOUZWA KUPITIA SOKO LA AWALI NA UBANGUAJI KUPITIA VIKUNDI NA KILICHOBAKI KWA WAKULIMA (TANI) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MTWARA | TANECU | 150,060.610 | 124,047.884 | 26,012.726 |
| | | MAMCU | 180,444.440 | 116,770.945 | 63,673.495 |
| | | **Jumla ndogo** | **330,505.050** | **240,818.829** | **89,686.221** |
| 2 | LINDI | RUNALI | 85,661.860 | 73,826.620 | 11,835.240 |
| | | LINDI MWAMBAO | 47,314.810 | 41,853.885 | 5,460.925 |
| | | **Jumla ndogo** | **132,976.670** | **115,680.505** | **17,296.165** |
| 3 | RUVUMA | TAMCU | 36,028.950 | 31,608.038 | 4,420.912 |
| 4 | PWANI | CORECU | 25,676.410 | 19,950.228 | 5,726.182 |
| 5 | TANGA | TACACU | 2,004.060 | 474.788 | 1,529.272 |
| 6 | SINGIDA | CEAMCU | 550.000 | 172.073 | 377.927 |
| 7 | MOROGORO | UKICU | 431.140 | 370.601 | 60.539 |
| 8 | MBEYA | | 59.250 | | 59.250 |
| 9 | SONGWE | | 0.840 | | 0.840 |
| 10 | KATAVI | | 3.700 | | 3.700 |
| 11 | RUKWA | | 3.600 | | 3.600 |
| 12 | KIGOMA | | 24.160 | | 24.160 |
| | **JUMLA KUU** | | **528,263.830** | **409,075.062** | **119,188.768** |

***Chanzo:*** **Bodi ya Korosho Tanzania, 2025**

### 7.1.3. Mwenendo wa bei kwa msimu wa 2024/2025

Katika msimu wa masoko na mauzo wa mwaka 2024/2025 bei ya juu kwa daraja la kwanza ni shilingi 4,195 na bei ya chini ni Shilingi 1,810 na daraja la pili bei ya juu ni shilingi 2,870 na bei ya chini Shilingi 1,410. Bei ya wastani kwa daraja la kwanza ilikuwa shilingi 3,592 na daraja la pili shilingi 2,140 kwa kilo. Kwa upande wa Soko la Awali mauzo ya korosho ghafi katika Soko la Awali kwa ajili ya kubangua ndani ya nchi yalikuwa kati ya shilingi 3,000 hadi 2,000 kwa kilo ambapo wabanguaji walinunua korosho kupitia AMCOS na wengine waliingia mnadani na kununua korosho kwa njia ya ushindani. Wakulima walilipwa fedha zao kupitia akaunti zao, makato mengine ambayo ni ushuru wa Halmashauri, ushuru wa chama kikuu, magunia na tozo nyingine zililipwa na mnunuzi.

**Bei ya korosho ghafi msimu 2024/25 kwa kila chama kikuu**

| MWENENDO WA BEI KWA KILA CHAMA MSIMU 2024/2025 | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| MNADA NA | TANECU | MAMCU | RUNALI | LINDI MWAMBAO | TAMCU | CORECU | UKICU | CEAMCU | TACACU |
| 1 | 4,120-4,035 | 4,195-3,440 | 4,150-3,760 | 3,865-3,400 | | | | | |
| 2 | 3,760-3,540 | 3,520-2,990 | 3,480-3,290 | 3,430-3,060 | | 3,710-2,730* | | | |
| 3 | 3,430-3,200 | 3,390-3,000 | 3,390-3,290 | 3,140-2,810 | 3,510-3,210 | 3,430-2,610* | | | |
| 4 | 3,570-3,220 | 3,430-3,010 | 3,600-3,330 | 3,320-3,040 | 3,230-3,150 | 3,440-2,590* | | | |
| 5 | 3,410-3,210 | 3,310-2,950 | 3,410-3,230 | 3,190-2,510* | 3,250-3,180 | 3,180-2,410* | 2,710-2,610* | | |
| 6 | 3,240-2,960 | 2,930-2,410 | 3,070-2,910 | 2,900-2,510* | 3,290-3,200 | 2,940-2,410* | | | |
| 7 | 2,915-2,410* | 2,900-2,110* | 3,060-2,610 | 2,460-2,060* | 2,790-2,570 | 2,714-2,220* | 2,410-2,210* | | |
| 8 | 2,920-2,410* | 2,710-1,910 | 3,000-2,650 | 2,600-1,990* | 2,910-2,830 | 2,520-2,000* | | | |
| 9 | 2,830-2,420* | 2,620-1,810* | 2,350-1,510* | | 2,090-2,010 | 2,250*-1,900* | | | |
| 10 | 2,750-1,910* | 1,910-1,510* | 1,960-1,310* | | 2,380-1,510* | 1,010*-1,010* | | | |
| 11 | 2,540-1,510* | 2,140-1,530* | | | 2,020-1,210* | 1,110* | | | |
| 12 | 2,310-1,670* | 1,970-1,410* | | | | | | | |
| 13 | 2,110-1,950* | | | | | | | 3,167 | 2,860*-2,610 |
| 14 | 2,310-1,510* | | | | | | | 2,110 | 2,100*-1510* |
| 15 | | | | | | | | | 1,810* |

### 7.1.4. Mwenendo wa Usafirishaji wa korosho msimu 2024/2025

Hadi kufikia tarehe 01 Agosti, 2025 kiasi cha tani 391,669.448 zilikuwa zimesafirishwa kwenda nje ya nchi katika nchi za Vietnam (209,724.44) India (181,883.008), China (40.000), Zambia (15.000) Kenya (7.000) huku korosho ghafi zilizosafirishwa kwenda nje ya nchi kupitia bandari ya Mtwara ni tani 370,232.148 na korosho zilizosafirishwa kupitia bandari ya Dar es salaam ni tani 21,437. Hadi kufikia tarehe 1 Agosti 2025 kiasi cha tani 4,500.678 za korosho karanga zimesafirishwa Kwenda nchi mbalimbali duniani ikiwemo China (tani 1,050.320), Uholanzi ( tani 960.899), Umoja wa falme za kiarabu (tani 444.107), Uturuki (tani 438.245), Kuwait (tani 153.520), Afrika Kusini (tani 100.613) n.k.

### 7.1.5. Hali ya Ubora wa Korosho na Udhibiti wa Ghafi kwa Msimu 2024/2025

Hali ya ubora wa korosho ghafi zilizouzwa kupitia Mfumo wa Stakabdhi za Ghala (WRRB) Msimu wa Mauzo ya Korosho Ghafi 2024/2025 umeendelea kuimarika kwa asilimia 95.4%. Hii ilitokana na hatua zilizochukuliwa na Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) ambazo ni pamoja na:- kuweka wasimamizi katika ghala zote 45 za mnada kwa kwa ajili ya kuhakikisha korosho zinazopokelewa ghalani zinakidhi viwango vya ubora kama ilivyoainishwa katika Sheria Na.18 ya Tasnia ya Korosho ya Mwaka 2009 kifungu cha. 19 na Kanuni zake kanuni za Mwaka 2010 Kanuni Na.26(I), pamoja na kufanya ukaguzi maalumu na kushitukiza katika ghala kuu za mnada na ghala za Vyama vya Msingi (AMCOS), kuunda Kikosi kazi kilichokuwa kinadhibiti biashara ya magendo katika tasnia ya korosho.

Hata hivyo Pamoja na mafanikio makubwa katika kulinda ubora tofauti na Msimu wa Mwaka 2023/2024 ubora umeshuka kwa 3.1% kutoka asilimia 98.5% ya korosho daraja la kwanza msimu 2023/2024 hadi asilimia 95.4% ya korosho daraja la kwanza msimu wa mwaka 2024/2025 katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani, Mbeya, Njombe, Morogoro na Dodoma. Kushuka kwa ubora kumechangiwa na ongezeko kubwa la uzalisha kutoka tani 310,000 mwaka 2023/2024 hadi tani 528,000 mwaka 2024/2025 ikiwa ni ongezeko la asilimia 70% la uzalishaji ambalo lilipelekea miundombinu kuzidiwa hivyo korosho kuhifadhiwa katika miundombinu isiyosahihi kwa ubora wa korosho kwa mfano baadhi ya korosho zilihifadhiwa kwenye viroba majumbani kwa wakulima kwa muda mrefu, pia korosho nyingi zilikaa nje kwenye ghala za Vyama vya Msingi (AMCOS) kwa muda mrefu zikisubiria kupatikana kwa nafasi katika ghala kuu za mnada.

## 7.2. MAANDALIZI YA MSIMU NA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KATIKA MSIMU WA MAUZO YA KOROSHO GHAFI MWAKA 2025/2026

Bodi ya Korosho Tanzania inaendelea na maandalizi ya usimamizi wa masoko na mauzo ya korosho ghafi ili kuhakikisha msimu wa mwaka 2025/2026 unakuwa na mafanikio kwa wadau wa Tasnia ya Korosho nchini. Jumla ya tani 700,000 zinatarajiwa kuzalishwa katika msimu wa 2025/2026 sawa na ongezeko la asilimia 32.51 (%) ya uzalishaji wa msimu 2024/2025 ambapo zilizalishwa jumla ya tani 528,263.82. Katika msimu wa mauzo ya Korosho ghafi kwa mwaka 2025/2026, Bodi ya Korosho Tanzania ikishirikiana na Bodi ya Usimamizi wa stakabadhi za ghala, Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Soko la Bidhaa Tanzania, tayari imekamilisha maandalizi ya Mwongozo wa Usimamizi wa Masoko na Mauzo ya korosho ghafi, Mwongozo wa Usimamizi na Udhibiti Ubora wa korosho ghafi na Mwongozo wa Soko la Awali kwa wabanguaji wa ndani kwa msimu wa 2025/2026 ambao utasambazwa kwa wadau kabla ya msimu wa mauzo kuanza.

### 7.2.1. Upatikanaji wa leseni za ununuzi wa korosho kwa wanunuzi walioko ndani na Nje ya Nchi

Mnunuzi atakayeruhusiwa kununua korosho ghafi katika msimu wa mauzo wa mwaka 2025/2026 atatakiwa awe amesajiliwa na kupata Leseni ya ununuzi inayotolewa na Bodi ya Korosho Tanzania. Wanunuzi wote wa korosho watasajiliwa

na Bodi ya Korosho Tanzania kupitia Mfumo wa Wizara ya Kilimo wa Kusimamia Biashara za Kilimo (*'Kilimo Portal' (https://portal.kilimo.go.tz)*). Wanunuzi wataingia kwenye mfumo huu na kuambatisha nyaraka zote zinazohitajika kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo. Kila mnunuzi atatakiwa kuweka kinga ya zabuni (*Bid Security*) fedha taslimu kabla ya kupata leseni ya ununuzi katika Akaunti ya Malipo ya Bodi ya Korosho kwa kuzingatia viwango vifuatavyo:

***Viwango vya kinga ya dhamana kwa kampuni zilizo ndani ya nchi***

| TANI KWA MNADA | KIASI (Shilingi za Tanzania) |
|---|---:|
| 50 - 100 | 20,000,000.00 |
| 101 - 250 | 50,000,000.00 |
| 251 - 500 | 100,000,000.00 |
| 501 - 1000 | 300,000,000.00 |
| 1001 - 3000 | 500,000,000.00 |
| 3001- Nakuendelea | 1,000,000,000.00 |

Wanunuzi watakaokamilisha hatua ya usajili na kulipa kinga/dhamana ya zabuni 'bid security' wataingizwa kwenye mfumo wa Mauzo wa Kielektroniki wa TMX.

**NB**: Wanunuzi wa ndani watakaohitaji kununua korosho mnadani kwa ajili ya kubangua korosho hapa nchini wataweza kununua korosho ghafi chini ya Tani 50. Aidha, hawatalazimika kuweka kinga ya dhamana na badala yake watatakiwa kuleta ushahidi wa benki kuweza kulipia kiasi cha korosho ghafi wanachohitaji kununua. Pia wabanguaji wa ndani wanaweza kununua korosho kwa ajili ya malighafi ya viwanda vyao kupitia utaratibu wa soko la awali ambapo wanaweza kununua korosho mojakwa moja kwa mkulima kupitia AMCOS.

### 7.2.2. Utaratibu wa mauzo

#### 7.2.2.1. Ununuzi kwa ajili ya kusafirisha nje ya Nchi

Mauzo ya korosho ghafi kwa msimu wa 2025/2026 yatafanyika kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani na minada itafanyika kwa mfumo wa Kielektroniki wa Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) chini ya Usimamizi wa Bodi ya Korosho Tanzania na Vyama Vikuu vya Ushirika. Hati ya mauzo (Sales Catalogue) itatolewa na chama kikuu cha ushirika na soko la bidhaa (baada ya uhakiki kufanyika na timu itakayoundwa) saa

10:00 jioni siku moja kabla ya mnada. Nyongeza ya hati ya mauzo (Sales Catologue) itatolewa saa moja kabla ya kuanza mnada.

#### 7.2.2.2. Utaratibu wa malipo kwa wakulima

Malipo kwa wakulima yatafanyika kupitia akaunti za benki baada ya Korosho kuuzwa katika mnada na mnunuzi kulipia korosho hizo. Aidha mnunuzi atawajibika kulipa tozo zilizoainishwa kisheria katika mkutano Mkuu wa Wadau wa tasnia ya korosho. Chama cha Ushirika cha Msingi kinatakiwa kuandaa na kuwasilisha orodha ya majina ya Wakulima na Wanachama wanaouza Korosho kupitia Chama husika yakionesha nambari ya akaunti ya Benki ya kila Mkulima na kuwasilisha Benki husika kwa ajili ya uhakiki kabla ya kupelekwa Vyama Vikuu. Mnunuzi anatakiwa kuweka fedha za mauzo ya Korosho pamoja na tozo ya ushirika, tozo ya uendelezaji zao, tozo ya magunia na tozo ya Halmashauri katika akaunti ya pamoja ("*Settlement Account*") ya Chama Kikuu cha Ushirika. Aidha, tozo ya CBT na tozo ya TARI Naliendele zitalipwa Bodi ya korosho kama itakavyo ainishwa na CBT kupitia Akaunti Namba. Malipo ya fedha za mauzo ya korosho kutoka kwa mnunuzi kwenda akaunti ya pamoja (Settlement Acount) ya Chama Kikuu husika na akaunti ya Bodi ya Korosho yatafanyika ndani ya **siku tano (5)** za kazi tangu tarehe ya mnada husika. Chama Kikuu cha Ushirika kitahakikisha malipo kwa mkulima yanafanyika ndani ya siku saba (7) za kazi baada ya mnada kufanyika na korosho kununuliwa. Orodha ya wakulima iliyotumika kupeleka korosho ghala kuu, itatumika kuwalipa wakulima hao na sio vinginevyo.

#### 7.2.2.3. Usafirishaji wa korosho na Utoaji wa vibali

Bodi ya Korosho itasajili magari yote yatakayotumika kusafirisha korosho toka ghala kuu kwenda bandarini au katika ghala la mnunuzi. Mnunuzi atakayeingia mkataba na kampuni ya usafirishaji isiyosajiliwa na Bodi ya Korosho atawajibika kwa uhalibifu au upotevu wowote wa Korosho utakaotokea. Mnunuzi atawajibika kulinda ubora wa Korosho zake wakati wote wa usafirishaji wa korosho ndani na nje ya nchi. Korosho itasafirishwa ndani ya nchi kwa kutumia kibali cha kusafirisha Korosho ndani ya nchi (*PDN*) kinachotolewa kwa njia ya kielektroniki na Bodi ya Korosho Tanzania. Waendesha maghala watawajibika kujaza taarifa za wanunuzi katika mfumo wa Bodi ya korosho ili kuomba kibali hiki kwa niaba ya mnunuzi. Korosho itasafirishwa nje ya nchi ikiwa na kibali cha kusafirisha korosho nje ya nchi (*Export Permit*), kinachotolewa na Bodi ya Korosho Tanzania kwa njia

ya kielektroniki. Maombi ya kibali hiki yataambatishwa na barua ya Ankara ya Biashara (*Commercial Invoice*) na agizo la kusafirisha mzigo kwa meli (*Shipping Order*).

#### 7.2.2.4. Usafirishaji wa korosho nje ya nchi

Korosho kwa ajili ya kusafirishwa nje ya nchi inatakiwa kulipiwa ushuru wa kusafirisha Korosho nje ya nchi (*Dola za Marekani 160 kwa tani au 15/% ya bei ya malipwani kiwango chochote kitakachokuwa juu kati ya hivi*) kama itakavyokuwa imekokotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Bodi ya Korosho itawasilisha TRA viwango vya bei vitakavyotumika kukokotoa Export Levy. Usafirishaji wa korosho kutoka Mtwara, Lindi na Ruvuma kwenda nje ya nchi utafanyika kupitia bandari ya Mtwara na korosho za Mkoa wa Pwani na Mikoa mingine zitasafirishwa kupitia Bandai za Dar es Salaam na Tanga kwa kuzingatia Mwongozo wa Masoko na Mauzo ya Korosho ghafi.

### 7.2.3. Hali ya soko la korosho

#### 7.2.3.1. Mwenendo wa Bei ya Korosho Karanga Katika Soko la Dunia.

Bei ya Korosho ghafi katika soko la dunia hutegemea mwenendo wa bei ya korosho Karanga. Bei ya korosho karanga imekuwa ikipanda na kushuka kutokana na kupungua ama kuongezeka kwa mahitaji/ulaji katika masoko makuu ya India, Vietnam pamoja na masoko ya China, Ulaya, Marekani na Mashariki ya kati. Bei ya Korosho Karanga nchini India na Vietnam kwa madaraja mbalimbali imepanda kidogo katika mwezi Julai hadi mwanzoni mwa Agosti, 2024 ukilinganisha na mwezi Julai hadi Agosti, 2024 licha ya vita vya ushuru vilivyoanzishwa na Marekani vinavyoleta athari katika uchumi wa dunia na kuathiri matumizi ya korosho.

Bei ya Korosho karanga (FOB) katika nchi za India na Vietnam hadi mwanzoni mwa mwezi Agosti, 2025 ni kati ya shilingi 19,787 – 20,979 (7.64USD – 8.10USD) huku katika nchi za Afrika ikiwa ni kati ya shilingi 18,829 – 19,968 (7.27 USD – 7.71 USD) kwa kilo kwa korosho daraja la WW320. Bei hii imepanda kwa wastani wa asilimia 5.07 (5.07%) ukilinganisha na mwenendo wa bei wa mwezi Julai kwa mwaka 2024 kwa upande wa India na Vietnam na kwa upande wa Afrika imepanda kwa wastani asilimia 1.49 (1.49%). India na Vietnam kwa kipindi cha Julai, 2024 bei ilikuwa ni Tzs 18,974 – 20,723 (7.16USD – 7.82USD) na kwa Afrika bei ilikuwa kati ya shilingi 19,265 – 19,848 (7.27 USD – 7.49 USD) kwa kilo kwa daraja la WW320. Daraja la WW320 ndio lina mahitaji makubwa katika soko ukilinganisha na madaraja mengine. Msimu wa mavuno na mauzo katika nchi za India, Vietnam na Afrika

Magharibi ambayo huanza mwezi Februari hadi Julai, tayari umefika ukingoni, hivyo kupunguza ushindani katika soko pindi mauzo yatakapoanza hapa nchini. Msimu wa mavuno hapa nchini unaenda sambamba na nchi chache ambazo ni Brazil, Kenya, Msumbiji pamoja na Indonesia. Kuimarika kwa bei ya korosho karanga huwa kuna mahusiano ya moja kwa moja na bei ya Korosho ghafi. Viwango vya bei ya korosho ghafi duniani vinatofautiana kati ya nchi moja na nyingine kutokana na nguvu ya soko. Kwa kuwa bei ya korosho ghafi na korosho karanga hupanda na kushuka kutokana na nguvu ya soko, Bodi ya Korosho itaendelea kutoa taarifa ya mwenendo wa bei mara kwa mara kwa wadau wa Tasnia.

**7.2.3.2. Shughuli zitakazotekelezwa katika kuimarisha Ubora Msimu 2025/2026**

Katika msimu wa mauzo ya korosho ghafi wa mwaka 2025/2026, Bodi itaendelea kuhakikisha ubora wa korosho unaimarika kwa mujibu wa kifungu cha 5(I)(2)(b) cha Sheria Na.18 ya Tasnia ya Korosho Mwaka 2009 kwa kufanya shughuli zifuatazo:-

i. kufanya zoezi la ukaguzi wa ghala za mnada na ghala za Vyama vya Msingi (AMCOS) kwa kutumia kikosi kazi (Task force) kitakachohusisha wataalam kutoka Bodi ya Korosho, Vyama Vikuu vya Ushirika na Halmashauri ("DSMs Cashew"/Afisa Ushirika);
ii. Kutoa mafunzo ya udhibiti ubora wa korosho ghafi kwa wakulima, viongozi wa AMCOS na wataalam ghala za mnada kabla ya kuanza msimu;
iii. Kutoa mafunzo ya udhibiti ubora wa korosho ghafi kwa wakulima wa maeneo yote yanayolima korosho kwa njia ya Redio za kijamii na mitandao ya kijami;
iv. Kutoa mafunzo kwa maafisa ugani kwa wilaya zinazolima korosho pamoja, Mameneja wa ghala kuu za mnada, na Kampuni za usafirishaji zilizosajiliwa;
v. Kuimarisha mifumo ya udhibiti ikiwemo kusajili kampuni za usafirishaji zitakazokuwa zinasafirisha korosho, hii itasaidia kufanya ufuatiliaji endapo changamoto ya ubora ikijitokeza;
vi. Kusimamia mapokezi ya korosho katika ghala za Vyama vya Msingi AMCOS kwa kutumia Maafisa Kilimo walioko katika Program ya Jenga Kesho iliyobora BBT;
vii. Kuhakikisha korosho zote zitakazobainika kuwa na ubora chini ya kiwango i,e chini ya SOT =35lbs/80Kg zinakusanywa na kuondolewa kwenye mfumo

wa mauzo na thamani kwa wakati ili kuepushwa kuchanganywa na korosho nzuri.

**7.2.3.3. Mafanikio katika msimu 2024/2025**

i. Kuongezeka kwa uzalishaji kutoka tani 310,787.168 msimu 2023/2024 hadi tani 528,263.82 msimu 2024/2025;

ii. Kuuzwa kwa korosho ghafi asilimia 99 ya zilizoingizwa mnadani pamoja na changamoto ya uhaba wa ghala za mnada kutokana na uzalishaji kuwa mkubwa;

iii. Kusafirishwa kwa korosho tani **370,232.148** sawa na asilimia **94.53 (94.53%)** ya korosho zote zilizosafirishwa kwenda nchi za nje kupitia bandari ya Mtwara baada ya agizo la Mheshimiwa Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan;

iv. Kuongezeka kwa bei ya korosho ghafi kutoka bei ya juu kwa Daraja la kwanza sh 2,200 msimu 2023/2024 hadi sh 4,195 msimu 2024/2025; na

v. Kuongezeka kwa wanunuzi wa korosho ghafi nchini kutoka kampuni 76 Msimu 2023/2024 hadi kampuni 82 msimu 2024/2025.

***7.2.3.4.*** **Changamoto za usimamizi wa mauzo na Mapendekezo ya Utatuzi**.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana bado kuna changamoto mbalimbali ambazo zinahitaji ufumbuzi kwa ajili ya kusimamia msimu wa 2025/2026 ili kuhakikisha soko la korosho ghafi linaendelea kuwa endelevu. Changamoto hizi ni kama ifuatavyo: -

**Changamoto na Mapendekezo**

| S/N | CHANGAMOTO | MAPENDEKEZO | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|
| 1 | Uwepo wa Ghala chache za kuhifadhia korosho ghafi wakati wa msimu 2024/2025. Hii ilitokana na ongezeko la uzalishaji kuliko uwezo wa ghala zilizokuwepo na hivyo kusababisha korosho kukaa nje kwa muda mrefu katika ghala za Vyama vya Msingi (AMCOS) zikisubiri nafasi kupatikana katika ghala za mnada. Aidha na katika baadhi ya ghala kuu za mnada zilikuwa zinasitisha mapokezi ya korosho mara kwa mara kutokana na ukosefu wa nafasi ya kupokea korosho. | Kuhamasisha ujenzi wa ghala za kutosha kupitia uwekezaji wa miundombinu ya kuhifadhia korosho ili kulinda ubora wa korosho pamoja na kupunguza gharama za wakulima kukaa katika ghala za Vyama vya Msingi kwa muda mrefu wakisubiri korosho zao kupokelewa na kupelekwa ghala kuu la mnada. | CBT Msimamizi wa Sheria.<br><br>Wengine ni WRRB & TCDC |
| 2 | Kuibuka kwa vikundi vya kihalifu vilivyokuwa vikishusha ubora wa korosho kwa kubadilisha korosho safi na bora chafu wakati wa usafirishaji kutoka ghala Kuu za mnada kwenda ghala za wanunuzi. | • Kusajili kampuni zote za usafirishaji na kuzipatia leseni ya kusafirisha korosho ghafi wakati wa msimu. Hii itadhibiti waharifu kwa kutambua chombo husika cha usafirishaji na kampuni itakayobainika itahusika kulipa gharama za mnunuzi na kuwajibika mbele ya vyombo vya sheria. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 15 (4) cha Sheria na. 18 ya mwaka 2009 inayosimamiwa na CBT.<br>• Kuundwa kwa kikosi maalum kutoka taasisi mbalimbali kwa ajili ya kudhibiti vitendo hivi katika kipindi chote cha Msimu wa Mauzo ya Korosho Ghafi. | CBT Msimamizi wa Sheria.<br><br>Wengine ni<br><br>TCDC, Vyombo vya Dola na Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3 | Kuchelewa kuchukuwa hatua stahiki za kinidhamu kwa waendesha ghala wanaobainika kukiuka Sheria Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Tasnia ya Korosho kama vile:- kushusha ubora wa korosho zikiwa ghalani, na kupokea korosho ambazo hazijakidhi viwango vya kuuzwa mnadani na kutoa taarifa za uongo mfano kuna tani 500 ghalani kumbe kuna tani 200 tu. Hii imesababisha hasara ya kuikosesa serikali mapato pamoja na wadau wengine kama vile Vyama vikuu na hasara ya kifedha kwa wanunuzi. | Hatua stahiki zichukuliwe kwa wakati dhidi ya waendesha ghala wanaokiuka Sheria Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Tasnia ya Korosho hii itasaidia kulinda ubora wa korosho zinazozalishwa nchini. Kifungu cha 15 cha Sheria na.18 ya mwaka 2009 cha Bodi ya Korosho Tanzania kitahusika. | CBT Msimamizi wa Sheria.<br><br>Wengine ni TCDC na Serikali za Mitaa |
| 4 | Wanunuzi kupokea korosho pungufu kwenye ghala za mnada baada ya kushinda mnada na kulipia kinyume na kifungu Na.3.3.2 cha Mwongozo Na.1 wa Usimamizi wa Masoko na Mauzo ya Korosho Ghafi kupitia Stakabadhi za Ghalani Msimu wa Mauzo 2024/2025 Toleo Na.4 | Kifungu Na. 15 cha Sheria na.18 ya tasnia ya korosho ya mwaka 2009 cha Bodi ya Korosho Tanzania kitahusika. Waendesha Ghala wasimamiwe ipasavyo ili kuhakikisha wanatoa korosho zenye ubora na kiasi kama walivyoshinda mnadani na kuainishwa katika hati ya mchanganuo wa mauzo (sales invoice).Aidha rasimu ya muongozo namba 1 wa usimamizi wa masoko na mauzo ya korosho ghafi kupitia stakabadhi ghalani wa mwaka 2025/2026 ni kifungu namba 4(xv) kinaeleza Chama Kikuu cha ushirika kwa kushirikiana na Soko la Bidhaa (TMX) wataanda hati ya mchanganuo wa mauzo baada ya ukaguzi kufanyika na timu itakayoundwa ili kujiridhisha kiasi na ubora wa korosho zilizopo ghalani. | CBT Msimamizi wa Sheria.<br><br>Wengine ni<br>TCDC, Sekretarieti za Miko ana Serikali za Mitaa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 5 | Upungufu wa vifungashio katika baadhi ya maeneo, hali iliyopelekea Vyama vya Msingi (AMCOS) kukaa na korosho za wakulima kwa muda mrefu bila kuzipeleka katika ghala kuu za mnada na Vyama vingine kutumia vifungashio vyenye nembo za mazao mengine kama vile nembo za mazao ya sukari, na kahawa hali inayoweza kupelekea kushusha ubora wa korosho. | Taasisi zinazohusika na ununuzi na usambazaji wa vifungashio, zihakikishe kunakuwa na utoshelezi wa vifungashio wakati wote wa msimu. | CBT Msimamizi wa Sheria<br><br>Wengine ni<br>TCDC na KCJE |
| 6 | Huduma mbovu kwa wateja, katikaTasnia ya Korosho wadau wamekuwa wakiwasilisha malalamiko Bodi ya Korosho Tanzania baada ya kukosa huduma stahiki kutoka katika taasisi zinazohusika katika mnyonyoro wa thamani katika Tasnia ya Korosho. | Taasisi zote zinahusika katika mnyonyoro wa mauzo ya korosho ghafi kutoa huduma stahiki na kwa wakati kwa wateja ili kuepusha usumbufu kwa wateja. | CBT Msimamizi wa Sheria<br><br>Wengine ni Taasisi zingine zote zinazohusika |
| 7 | Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS) vina kipima unyevu kimoja licha ya kuwa na zaidi ya eneo moja la kukusanyia korosho hali inayopelekea kupokea korosho bila kuhakiki kiwango cha unyevu hivyo kupeleka ghalani korosho zenye kiwango cha unyevu zaidi ya 10%. | Vyama Vikuu vya Ushirika kuhakikisha matawi yote ya Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS) yanakuwa na vipima unyevu ili kuhakikisha korosho zinazopokelewa zinakuwa na kiwango cha unyevu chini ya 10%. Hata hivyo Vyama Vikuu vya Ushirika vinaendelea kuviwezesha Vyama vya Msingi vya Ushirika kwa kuwakopesha vipima unyevu. Sambamba na hilo hakuna tawi jipya la kukusanyia korosho litakaloanzishwa na Chama cha Msingi bila kuwa na kipima unyevu. | CBT Msimamizi wa Sheria<br><br>Wengine ni TCDC na Serikali za Vijiji na Mitaa |
| 8 | Baadhi ya viongozi wa Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS) kutokuwa waaminifu kwa | Vyama ambavyo vimekuwa na changamoto sugu za ubora viongozi wa vyama | CBT Msimamizi wa Sheria |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | kupokea korosho zenye ubora hafifu kutoka kwa wafanya biashara na kuzichanganya na Korosho za wakulima hivyo kupelekea kushusha ubora wa korosho za wakulima. | waondolewe kwenye uongozi maana ndiyo wanakuwa chanzo kushusha ubora wa korosho za wakulima kwa mfano UMOJA MIKOMA AMCOS, Pande AMCOS, Mshikamano AMCOS, Ulina AMCOS, Mtungi AMCOS, Ujirani Mwema AMCOS. | Wengine TCDC na Serikali za Mitaa. |

**AGENDA NA 8.0 MAPENDEKEZO YA TOZO MBALI MBALI KATIKA MAUZO YA KOROSHO MSIMU WA 2025/2026**

**AGENDA NA 9.0 KUPOKEA TAARIFA YA MAANDALIZI YA MSIMU KUTOKA KATIKA TAASISI MBALIMBALI**

**AGENDA NA. 9.1 TAARIFA KUTOKA UMOJA WA WABANGUAJI WAKUBWA WA KOROSHO (TACP)**

## 9.1. TAARIFA KUTOKA UMOJA WA WABANGUAJI WAKUBWA WA KOROSHO (TACP)

### 9.1.1. Utangulizi

Chama cha wabanguaji wa korosho Tanzania (Tanzania Association of CashewNuts Processors - TACP) kilianzishwa na kusajiliwa nchini mwaka 2020 kwa lengo la kutengeneza jukwaa moja la wabanguaji na kushirikiana na serikikali kuhamisha ubanguaji wa korosho nchini. Tangu kuanzishwa kwake kumekuwa na mwitikio mzuri wa wawekezaji katika viwanda vya korosho kutoka wanachama tisa mwaka 2020 hadi Zaidi ya wanachama 26 mwaka 2024.

### 9.1.2. Mafanikio msimu wa 2024/2025:

i. Ubanguaji umeongezeka kutoka wastani wa 2% mwaka 2019/2020 hadi 23% mwaka 2024/25 na kuajiri zaidi ya watanzania 14000.

ii. TACP imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika tasnia ya ubanguaji wa korosho. Ipo miradi mikubwa zaidi ya minne (4) katika hatua mbalimbali za Ujenzi.

iii. TACP imeendelea kushiriki semina na makongamamo ya kimataifa ya kibiashara. Hatua hii imeendelea kutanua wigo wa kibiashara na kukutana na wadu mbalimbali ulimwenguni kote. February 2025 tulishiriki World Cashew Conference, Dubai na Julai 2025 tulishiriki Mafunzo ya mchakato wa utungaji sera, Sogakope Ghana.

iv. Masoko ya korosho karanga ya Tanzania yameendelea kuimarika katika masoko ya ndani ya nchi, Ulaya, Mashariki ya kati, Uchina na Afrika. Hali hii imechagizwa na ukuaji wa ubanguaji wa ndani unaotumia teknolojia za kisasa.

v. Mwitikio wa wakulima wanao ongeza thamani korosho ghafi kupitia viwanda vikubwa na vidogo umeendelea kuongezeka na hivyo kupelekea unafuu wa upatikanaji wa korosho karanga kwa soko la ndani ya nchi.

vi. Jumla ya wanuafaika 450 walipatiwa mafunzo ya kanuni bora za utunzaji wa mavuno na njia bora za ubanguaji (Post Harvest Managemnet and good processing practice). Mafunzo haya yalitolewa kwa kushirikiana na kampuni ya Akros Limited, Sabayi Investments, Workpoint Ltd na Korosho Group katika maeneo ya Mkuranga, Rufiji, Tandahimba na Masasi. Mafunzo hayo yalienda sambamba na ugawaji wa machine 30 za ubanguaji kwa vikundi vya

wanawake na vijana pamoja na uanzishwaji wa vituo vya uuzaji wa korosho karanga.

#### 9.1.3. Matarajio/Mikakati ya Msimu 2025/2026

i. Kuendelea kuimarisha ufanisi wa soko la awali ili liwe na tija kwa wadau wote katika tasnia. Hii ni pamoja na upatikanaji wa mwongozo wa soko la wali wa muda mrefu, hatua hii itachochea uwekezaji zaidi katika tasnia ya ubanguaji wa korosho nchini.

ii. TACP imejipanga kuendelea kushrikiana na Serikali kupitia Bodi ya korosho kuongeza kiwango cha ubanguaji wa korosho kufika 35% kwa msimu huu wa mwaka 2025/26. Hatua hii itahusisha:

   a. Kushirikiana na Bodi ya korosho kusajili na kurasimisha wabanguaji wadogo ili waweze kuchangia pato la taifa kama ilivyoanishwa katika Dira ya maendeleo 2025-2050.
   b. Kuogeza ubora wa korosho karanga zilizobanguliwa na wabanguaji wadogo kwa kuendelea kutoa mafunzo na zana sahihi za ubanguaji zinazoendana na mazingira.
   c. Kuhakikisha uwepo wa masoko ya uhakika kwa wote.
   d. Kuendelea kushawishi uwekezaji wa viwanda vikubwa vya ubanguaji kutoka kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi
   e. Kuanzisha kiwanda cha kutengeneza mashine za kisasa za ubanguaji wa korosho kwa kuingia ubia na kampuni za nje. Hatua hii itapunguza gharama za uagizaji mashine na vipuri na kuongeza tija kwa wabanguaji.
   f. Kuendelea kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vya uongezaji thamani kwa mabaki yatokanayo na ubanguaji wa korosho (Vaue addition on cashew By-Products)

iii. Kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa, Wilaya, Bodi ya korosho, vyama vikuu na vyama vya msingi, taasisi za fedha na wadau wengine katika Kuhamashisha ujengwaji wa maghala madogo madogo ya kuhifadhia korosho vijijini ili kupunguza upotevu wa ubaora wa korosho ghafi. Hatua hii itaongeza tija kwa mbanguaji na mkulima. Kipaumbele kitakuwa kwenye vijiji vyenye changamoto zaidi ya maghala.

iv. Kuendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali za kitaifa na kimataifa kupata masoko ya uhakika ya kikanda na kimataifa.

v. Kuendelea kuwajengea imani wawekezaji wa dani na nje kuhusu kuwekeza kwenye tasnia ya korosho nchini. Hii ni pamoja na taasisi za fedha.

### 9.1.4. Changamoto

i. Mahitaji makubwa ya korosho za Tanzania katika soko la China huku wabanguaji **Wazawa wakiendelea kutoruhusiwa kuingiza korosho katika soko la china.** Hali hii ni tofauti na mazao mengine kama Soya, Ufuta ..n.k
ii. Uwepo wa wanunuzi holela katika soko la awali la korosho ghafi na korosho karanga.
iii. Ushindani mkubwa wa **Bei** toka katika nchi nyingine ambazo zinauza korosho karanga kama vile Vietnam, Ghana, Ivory Coast, Nigeria…n.k
iv. Kuzuiwa kuingiza korosho karanga katika soko la **India** ambalo ndilo siko leye bei nzuri kuliko yote Duniani. Hatua hii inasababisha ushindani usio na usawa katika ununuzi wa korosho ghafi.
v. Kutokua na mwongozo wa soko la awali wa muda mrefu, hali hii imeathiri kwa kiasi kikubwa mipango ya ununuzi na uwekezaji kwa wabanguaji.
vi. Masharti na riba kubwa zinazotozwa na mabenki ya kibiashara (>12%) na hivyo kuwafanya wabanguaji wa Tanzania kutoshindana kimataifa ambapo washindani wetu katika masoko ya kimataifa hutozwa riba ya <5%
vii. Kubadilika mara kwa mara kwa mwongozo wa soko la awali na hivyo kuathiri mipango na mfumo wa ununuzi kwa wabanguaji wa ndani
viii. Tozo nyingi zinatozwa na taasisi mbalimbali kwa wabanguaji wa ndani.

### 9.1.5. Mapendekezo

Ili kuimarisha ubanguaji wa ndani na kufikia malengeo ya serikali kubangua 60% ifikapo 2026/2027, tunapendekeza yafuatayo:

i. Serikali iendelee kuimarisha mfumo wa soko la awali ili kuvilinda viwanda vya ndani na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Uwepo wa soko hili umeendelea kuwa kivutio kikubwa kwa wawekezaji kutoka Ulaya na Korea ya kusini kwani unaendana na uhitaji wa soko (Traceability).

ii. Serikali itenge sehemu ya ‘export levy’ kusaidia ubanguaji wa ndani kwa kutoa fungu maalumu kuhamsisha ubanguaji kama zinavyofanya nchi za Ivory coast na Benin. Fungu hili liwe rejeshi (Revolving fund)

iii. Kuanzishwe mfuko mahususiwa kukopesha wabanguaji kwa riba shindani kimataifa

iv. Serikali iendele kutumia diplomasia ya uchumi kufungua masoko katika nchi marafiki kama India na China.

v. Serikali kuendelea kushirikiana na TACP kuimarisha ubanguaji na kutoa ajira kwa watanzania

vi. Ujenzi wa Kongani ya Malanje iende sambamba na kuimarisha uwezo wa viwanda vya ndani ambavyo vinahitaji tu mtaji wenye riba nafuu ili kuongeza uzalishaji mara dufu.

**AGENDA NA. 9.2 TAARIFA KUTOKA TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA (TCDC)**

## 9.2. TAARIFA KUTOKA TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA (TCDC)

### 9.2.1. Utangulizi.

Msimu 2024/2025 wa mauzo na biashara ya korosho ulizinduliwa rasmi kitaifa Mkoani Mtwara katika Chama Kikuu cha Ushirika TANECU mnamo tarehe **11 Oktoba,2024** na kumalizika Mwezi Januari 2025. Bei elekezi iliyotangazwa na Serikali kupitia Bodi ya Korosho Tanzania ilikuwa **Shilingi 4,000** kwa kilo moja ya Korosho ambapo kwenye baadhi ya maeneo ilifika **Shilingi 4,193** kwa kilo moja ya Korosho.

### 9.2.2. Mauzo na biashara ya korosho msimu wa 2024/2025.

Hadi kufikia tarehe 31/01/2025 jumla ya kilo **409,727,752** za Korosho zenye thamani ya **Shilingi 1,286,672,683,638** zimekusanywa na kuuzwa kupitia Vyama vya Ushirika katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani, Morogoro na Singida. Aidha katika msimu wa mwaka 2024/2025 jumla ya thamani ya kiasi cha Shilingi **1,275,857,098,784** zimelipwa kwa wakulima wa korosho **1,435,676** kama inavyoonesha katika**.**

Mchanganuo wa mauzo ya Korosho kwa kila Mkoa ni kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini.

**Ununuzi wa Korosho kwa msimu wa soko 2024/2025**

| MKOA | Mauzo | |
|---|---|---|
| | Kilo | Thamani (Tshs) |
| MTWARA | 240,803,909 | 763,484,540,785 |
| LINDI | 115,680,505 | 364,383,881,765 |
| RUVUMA | 31,372,359 | 92,562,665,869 |
| PWANI | 21,328,577 | 63,200,975,119 |
| SINGIDA | 172,458 | 499,922,280 |
| MOROGORO | 369,944 | 982,542,040 |
| TANGA | 586,876 | 1,558,155,780 |
| **Jumla kuu** | **410,314,628** | **1,286,672,683,638** |

**Taarifa ya malipo kwa wakulima**

| Na. | MKOA | JINA LA CHAMA | IDADI YA WAKULIMA | THAMANI YA MALIPO KWA WAKULIMA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | MTWARA | TANECU LTD | 339,287 | 388,225,005,317 |
| | | MAMCU LTD | 834,765 | 370,847,782,645 |
| 2. | LINDI | LINDI MWAMBAO LTD | 74,030 | 131,091,932,070 |
| | | RUNALI LTD | 56,567 | 233,120,684,045 |
| 3. | RUVUMA | TAMCU LTD | 103,380 | 91,035,994,467 |
| 4. | PWANI | CORECU LTD | 26,540 | 58,682,051,990 |
| 5. | SINGIDA | CEAMCU LTD | 348 | 499,109,930 |
| 6. | TANGA | TACACU LTD | 461 | 1,369,908,510 |
| 7. | MOROGORO | UKICU LTD | 298 | 984,629,810 |
| | | **Jumla** | **1,435,676** | **1,275,857,098,784** |

### 9.2.3. Mpango wa malipo ya pamoja

Kwa mara ya kwanza utaratibu wa vituo vya malipo (Payment Centre) umeanza kutumika msimu wa 2024/2025 ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa maelekezo ya Serikali. Utaratibu huu, umewezesha Vyama Vikuu vya Ushirika kufanya malipo moja kwa moja kwa wakulima badala ya kupitishia malipo hayo kwenye Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS) kama ilivyokuwa awali.

### 9.2.4. Mafanikio yaliyopatikana katika msimu wa mauzo ya korosho 2024/2025 kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani

Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika msimu wa mauzo ya korosho ghafi wa mwaka 2024/2025 ni kama ifuatavyo; -

i. Wakulima kupata malipo ya fedha zao kwa wakati kwa kuzingatia maelekezo ya Serikali ya kulipa wakulima moja kwa moja kupitia Vyama Vikuu vya Ushirika;
ii. Kuendelea kurahisisha upatikanaji wa takwimu za mazao yanayozalishwa na wakulima. Hii inasaidia Serikali na wadau katika kupanga mipango ya Maendeleo;
iii. Urahisi wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali na wadau wengine waliopo katika mnyororo wa thamani wa zao la korosho;
iv. Matokeo chanya ya matumizi sahihi ya mizani za kidigitali kwa Vyama vya Ushirika ambavyo vilipata mizani hizo;

**9.2.5. Changamoto zilizojitokeza katika msimu wa mauzo ya korosho 2024/2025**

i. Baadhi ya makampuni kutolipa fedha za korosho walizonunua mnadani mfano Kisasika Company Ltd ilinunua Tani 800 kutoka Chama Kikuu Lindi Mwambao na hawakulipia mzigo huo kwa wakati;
ii. Baadhi ya Vyama vya Ushirika vya msingi kutotumia mizani ya kidigitali kwa ufanisi;
iii. Baadhi ya wakulima kutofufua akaunti zao za kibenki na hivyo kupelekea malipo yao kutolipwa kwa wakati;
iv. Baadhi ya wakulima kutosafisha na kukausha kwa ufasaha korosho zao vizuri;
ghala yanazingatia viwango vya ubora na usalama;

iv. Kusimamia matumizi ya kanzidata ya mfumo inayohusisha na ukusanyaji wa takwimu na za bidhaa zinazopokelewa na kutolewa ghalani;

v. Kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali wa mfumo wakiwemo waendesha ghala, wanunuzi, vyama vya wakulima na wadau wengine wenye maslahi katika Mfumo;

vi. Kusimamia utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya ubora kutoka kwa taasisi nyingine za udhibiti kama vile Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

## AGENDA NA. 9.4 TAARIFA KUTOKA SOKO LA BIDHAA TANZANIA (TMX)

## 9.4. TAARIFA KUTOKA SOKO LA BIDHAA TANZANIA (TMX)

### 9.4.1. Utangulizi

Kufuatia maelekezo ya Serikali kupitia Wizara ya Kilimo ya Kuuza zao la Korosho kupitia Mfumo wa Soko la Bidhaa Tanzania, Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na Soko la Bidhaa Tanzania, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala, Tume ya Maendeleo ya Ushirika pamoja na Wadau wengine katika msimu wa 2024/25 ilisimamia na kuendesha shughuli za minada kupitia mfumo wa mauzo wa kielektroniki wa Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) kwa lengo la kuweka mazingira ya uwazi na ushindani katika biashara ya zao la Korosho ili kuongeza tija kwa wakulima kwa kuongeza kipato kutokana na zao hili kama ilivyo adhima ya Serikali.

Katika Msimu wa 2024/25, jumla ya Mikoa Saba (7) inayozalisha zao la Korosho imeuza kupitia Mfumo wa Stakabadhi Ghala na Soko la Bidhaa Tanzania, mikoa hiyo ni pamoja na Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani, Morogoro Singida pamoja na Tanga ambapo jumla ya **kilo 409,039,713** zenye thamani ya shilingi za kitanzania **1,468,905,696,522.72** ziliuzwa.

### 9.4.2. MAANDALIZI KUHUSU MAUZO YA KOROSHO

Maandalizi ya kuuza Korosho kupitai mfumo wa Soko la Bidhaa yalifanyika vizuri kwa kushirikiana na wadau wote ikiwa ni pamoja na elimu kutolewa kwa Wanunuzi jinsi ya kununua kupitia mfumo wa kilekitroniki, Vyama Vikuu vya Ushirika pamoja na wadau wengine. Pia kuwa na vifaa vya kuwezesha wakulima kufuatilia minada (TV & Projector) kwa kushirikiana na Vyama Vikuu vya Ushirika, uwepo wa Ofisi ya Soko la Bidhaa katika ofisi za Bodi ya Korosho ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kutoka Soko la Bidhaa.

### 9.4.3. UENDESHWAJI WA MINADA

Utaratibu na uendeshwaji wa Minada ulifanyika kwa ushirikiano mkubwa baina ya wadau husika wakiwemo Soko la Bidhaa Tanzania, Bodi ya Korosho pamoja na Vyama Vikuu vya Ushirika. Ushirikiano huu uliwezesha pamoja na mambo mengine:-

- Uandaaji wa kabrasha la Mauzo kwa wakati na kwa ufanisi;
- Kukubaliana juu ya bei ya kuanzia (Kinga bei);
- Utatuzi wa changamoto zilizokuwa zinajitokeza wakati na baada ya mnada kufanyika
- Uwasilishwaji wa taarifa za ridhio la kuuza/ kutokuuza kwa wakati;

### 9.4.4. MAUZO YA KOROSHO

Katika Msimu wa mauzo ya Korosho 2024/25, jumla ya kilo 409,039,713 ziliuzwa kupitia mfumo wa Soko la Bidhaa Tanzania. Mchnganuo wa mauzo haya ni kama ifuatavyo:

***Mchanganuo wa Mauzo kwa Mkoa***

| Na | Mkoa | Kilo | Thamani (Tzs) |
|---|---|---:|---:|
| 1 | Mtwara | 240,843,386 | 873,548,505,950.84 |
| 2 | Lindi | 115,680,505 | 417,013,825,817.20 |
| 3 | Ruvuma | 31,608,038 | 107,582,102,395.72 |
| 4 | Pwani | 19,950,228 | 67,788,134,058.32 |
| 5 | Morogoro | 370,601 | 1,153,786,930.44 |
| 6 | Singida | 172,073 | 577,650,930.12 |
| 7 | Tanga | 414,882 | 1,241,690,440 |
| | **JUMLA** | **409,039,713** | **1,468,905,696,522.72** |

*1.3*

***Mchanganuo wa Mauzo kwa kila Chama Kikuu cha Ushirika***

| Na. | Chama Kikuu cha Ushirika | Mkoa | Kilo | Thamani (TZS) |
|---|---|---|---:|---:|
| 1 | TANECU LTD | Mtwara | 124,072,441 | 454,854,956,260.04 |
| 2 | MAMCU LTD | Mtwara | 116,770,945 | 418,693,549,690.80 |
| 3 | RUNALI LTD | Lindi | 73,826,620 | 266,818,106,477.80 |
| 4 | Lindi Mwambao Ltd | Lindi | 41,853,885 | 150,195,719,339.40 |
| 5 | TAMCU LTD | Ruvuma | 31,608,038 | 107,582,102,395.72 |
| 6 | CORECU LTD | Pwani | 19,950,228 | 67,788,134,058.32 |
| 7 | UKICU LTD | Morogoro | 370,601 | 1,153,786,930.44 |
| | CEAMCU | Singida | 172,073 | 577,650,930.12 |
| | TACACU | Tanga | 414,882 | 1,241,690,440.08 |
| | **JUMLA** | | **409,039,713** | **1,468,905,696,522.72** |

***Mchanganuo Kwa Wanunuzi***

| Na | Jina la Mnunuzi | Kilo | Thamani (TZS) |
|---|---|---|---|
| 1 | A and V Group Ltd | 99,609 | 348,276,891.96 |
| 2 | Acorp Export Limited | 454,969 | 1,798,660,300.36 |
| 3 | Afagri Global Limited | 728,940 | 2,743,536,663.60 |
| 4 | Afri (EA) Ltd | 795,428 | 2,845,018,636.32 |
| 5 | Africa Harmony Industries & Trade Ltd | 2,007,288 | 6,920,167,724.72 |
| 6 | Afrisian Ginning Ltd | 2,165,689 | 7,519,477,267.16 |
| 7 | Afritech Greencrops Group Company Limited | 2,325,284 | 6,072,092,778.96 |
| 8 | Agro Pulses Export Tanzania Ltd | 1,572,768 | 5,537,916,705.92 |
| 9 | Agro Valley Tanzania Ltd | 2,756,167 | 10,465,846,545.48 |
| 10 | Agrolink Exports Tanzania Limited | 1,548,100 | 5,150,474,387.00 |
| 11 | Ags East Africa Ltd | 3,287,664 | 12,070,910,516.16 |
| 12 | Alpha Namata Company Ltd | 21,034,037 | 80,917,058,645.28 |
| 13 | Alphavillah Company Limited | 7,700,553 | 26,936,453,286.32 |
| 14 | Ananuts Agro Commodity (Tz) Ltd | 1,791,617 | 6,320,723,003.48 |
| 15 | Atmtot Company Limited | 2,954,913 | 10,614,226,619.72 |
| 16 | Cdjkl Nuts Ltd | 859,144 | 2,812,633,757.36 |
| 17 | Cedar Exim Limited | 644,755 | 2,488,649,922.20 |
| 18 | Cnb Brother Technology Limited | 1,026,856 | 3,377,543,662.64 |
| 19 | Coastal Nuts (T) Limited | 2,159,753 | 6,138,322,529.32 |
| 20 | Comafrique Trading Limited | 3,385,647 | 12,561,037,851.68 |
| 21 | Dorman (Tanzania) Ltd | 19,796,669 | 77,928,847,663.36 |
| 22 | Dunamis Agric Limited | 16,858,658 | 61,906,667,037.52 |
| 23 | Emmpire Commodities Limited | 2,747,972 | 9,266,592,975.68 |
| 24 | Equator Ventures Company Ltd | 185,960 | 736,510,522.40 |
| 25 | Exodus Agro Export | 1,664,575 | 5,932,211,733.00 |
| 26 | Export Connect Tanzania | 4,180,908 | 14,259,538,937.52 |
| 27 | Export Trading Company | 52,998,427 | 198,071,704,499.88 |
| 28 | Farheem Co Limited | 319,925 | 962,793,717.00 |
| 29 | Fi Commodities Tanzania Ltd | 1,747,921 | 5,709,224,271.24 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 30 | Glc Holding Limited | 58,108 | 115,428,055.52 |
| 31 | Global Golden Grains Ltd | 170,584 | 519,673,920.96 |
| 32 | Golden Cashews Limited | 6,956,556 | 25,089,196,940.64 |
| 33 | Golden Nuts Cashew Company Limited | 172,094 | 455,371,875.36 |
| 34 | Harmony Agro Ltd | 1,984,924 | 6,957,681,720.56 |
| 35 | Hs Impex Limited | 11,367,678 | 41,470,937,696.32 |
| 36 | Indotech Tanzania Limited | 2,613,102 | 9,253,465,426.88 |
| 37 | Iscon Commodities (T) Ltd | 37,057,350 | 137,778,322,639.00 |
| 38 | Karibu Kilimo Limited | 94,746 | 362,539,884.24 |
| 39 | Kasuga General Traders Ltd | 1,475,399 | 5,934,663,809.56 |
| 40 | Kisasika and Company Limited | 61,659 | 239,634,003.96 |
| 41 | Kopac Co Ltd | 20,880,199 | 77,786,108,841.56 |
| 42 | Leyan Commodities Tanzania Ltd | 2,241,394 | 6,751,245,507.36 |
| 43 | Lion Agro Global Limited | 2,760,762 | 10,291,268,027.28 |
| 44 | Listram Commodities Company Limited | 95,780 | 223,229,723.20 |
| 45 | Makanjiro Ompany Limited | 4,802,880 | 16,390,232,177.20 |
| 46 | Makonde Nuts Expoters Ltd | 4,924,911 | 15,378,660,086.84 |
| 47 | Mateak Holdings Limited | 4,770,737 | 13,677,730,606.28 |
| 48 | Matrics Overseas Limited | 3,837,061 | 12,953,274,842.84 |
| 49 | Mayani Enterprises Ltd | 239,993 | 923,118,674.92 |
| 50 | Megnacio Company Limited | 3,380,302 | 9,353,955,444.88 |
| 51 | Mohamed Entreprises | 3,436,037 | 12,343,149,938.28 |
| 52 | Nine Five Group Ltd | 3,743,538 | 11,356,443,674.72 |
| 53 | Ospher International Limited | 5,769,975 | 20,926,618,629.00 |
| 54 | Paramount Commodities Limited | 8,374,409 | 31,122,894,623.96 |
| 55 | Paramount Exim Ltd | 538,085 | 1,602,479,247.40 |
| 56 | Ph Agro Commodities Limited | 8,205,890 | 29,580,070,981.60 |
| 57 | Proscom Tanzania Company Limited | 11,306,821 | 40,260,693,687.24 |
| 58 | Psc Agro Impex Company Limited | 624,264 | 2,150,462,310.16 |
| 59 | R. V. Exports Ltd | 7,136,818 | 24,373,335,117.92 |
| 60 | Raa Trading Tanzania Limited | 369,683 | 1,289,757,178.52 |
| 61 | Rajan Agro Exports Ltd | 1,107,223 | 2,870,019,046.12 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 62 | Renatus Tanzania Ltd | 4,632,140 | 16,765,450,676.60 |
| 63 | Riya Star Commodities Limited | 1,690,698 | 5,836,820,735.12 |
| 64 | Robust Agro Commodities Trade International Limited | 2,682,551 | 10,790,214,968.44 |
| 65 | S R Impex Tanzania Limited | 1,136,598 | 4,774,499,861.12 |
| 66 | Sedaco Agro Tanzania Ltd | 9,364,237 | 35,811,015,826.28 |
| 67 | Sg Trade Tanzania Limited | 12,244,059 | 41,468,045,759.96 |
| 68 | Shri Salasar Export Tz Limited | 3,793,694 | 10,159,475,309.36 |
| 69 | Simba Korosho Limited | 1,764,552 | 7,282,975,764.88 |
| 70 | Sm Holdings | 3,982,058 | 15,002,413,903.52 |
| 71 | Speed Commodities Company Ltd | 4,786,232 | 17,828,869,384.08 |
| 72 | Star Arise Tanzania Limited | 1,835,669 | 6,234,769,048.36 |
| 73 | T.C Agriculture Company Limited | 244,494 | 886,642,821.36 |
| 74 | Tambuli Group Of Co Ltd | 736,421 | 2,768,870,471.24 |
| 75 | Tandahimba Newala Cooperative Union Limited | 1,058,792 | 3,159,473,820.48 |
| 76 | Tanzind International Limited | 49,504 | 127,192,865.76 |
| 77 | The Blue Moon Agro Limited | 481,977 | 1,869,165,971.88 |
| 78 | Three Leaves Commodity Tz Limited | 15,417,817 | 56,514,043,881.48 |
| 79 | VNBP Trading Ompany Limited | 22,779,062 | 73,430,972,059.28 |
| | **Jumla** | **409,039,713** | **1,468,905,696,522.72** |

### 9.4.5. MAFANIKIO

Msimu wa mauzo ya Korosho simu wa 2024/25 umekuwa na mafaniko makubwa uliochangiwa kwa kiasi kikubwa na ushirikiano wa wadau wote katika biashara ya Korosho. Mafanikio hayo ni pamoja na:

### 9.4.6. Ushindani Katika Minada

Kutokana na usimamizi Madhubuti katika biashara ya Korosho na kufuatia uhitaji wa Soko na matumizi ya Mfumo wa mauzo wa kielektroniki uliongeza uwazi na ushindani kwa Wanunuzi uliopelekea Wakulima kupata bei yenye tija.

### 9.4.7. Uwazi Katika Mauzo

Mauzo ya Korosho katika kupitia mfumo wa Kielektroniki yameongeza uwazi kwa wadau wote kuanzia kwa Wauzaji, Wanunuzi na wadau wengine ambapo kila mmoja aliweza kufuatilia mubashara mwenendo wa mnada pindi ulipokuwa unafanyisha. Uwazi huu ulisaidia katika suala la maaumuzi ya kuongeza bei kwa wanunuzi na maamuzi ya kuuza kwa wakulima mara tu walipotakiwa kufanya hivo.

### 9.4.8. Upatikanaji Wa Taarifa

Taarifa za bei, mauzo na mwenendo wa mauzo ya korosho ulipatikana kwa urahisi kwa kila mdau na kuwezesha kufanya maamuzi yaliyohitaji taarifa hizi.

### 9.4.9. Ongezeko La Wanunuzi Katika Minada

Katika msimu wa mauzo 2024/25, utaratibu wa kuuza Korosho kwa njia ya kielektroniki uliwezesha ongezeko la wanunuzi wengi walioshiriki na kununua Korosho nchini Tanzania kwa kuwa mnunuzi alikuwa na uwezo wa kushiriki kununua kutokea popote hata nchi za nje.

### 9.4.10. Ongezeko la Korosho zilizouzwa kupitia mfumo rasmi

Kutokana na Usimamizi madhubuti wa Serikali kupitia taasisi zake na wadau wengine wa zao Korosho, tumeshuhudia kiasi cha Korosho zilizouzwa na kurekodiwa katika mfumo rasmi kimeongezeka maradufu na kupekelekea pia ongezeko la pato la Serikali na Wadau wengine kupitia tozo na shuru zilizoainishwa na Bodi ya Korosho Tanzania.

### 9.4.11. CHANGAMOTO

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika mauzo ya Korosho msimu wa 2024/25, zipo changamoto zilizobainika ambao ni pamoja na:

#### *9.4.11.1. Mtandao Hafifu Katika Baadhi Ya Maeneo Ya Minada*

Baadhi ya vijiji vilivyoteuliwa kwa ajili ya wakulima kufuatilia minada na kufanya maamuzi ya kuuza au kutouzwa yalikuwa na changamoto ya upatikanaji wa mtandao (internet) wenye nguvu;

#### *9.4.11.2. Matumizi ya Ghala Moja kwa Vyama vikuu tofauti*

Chama kikuu cha TANECU na MAMCU kutumia ghala moja Micronix System lililoko Masasi kuhifadhi korosho kulileta changamoto hasa wakati wa uandaaji wa Kabrasha la Mauzo lakini pia kutambua makusanyo ya TANECU na MAMCU katika

ghala husika kwa kuwa taarifa za Mapokezi ya Korosho Ghalani kwenye kanzidata ya WRRB haiwezi kutofautisha korosho za TANECU na za MAMCU;

#### *9.4.11.3. Utofauti wa taarifa za Ubora wa Korosho*

Minada iliyofanyika mwishoni mwa msimu, kulikuwepo na baadhi ya ghala ambazo ubora wa korosho ulioripotiwa katika kanzidata na kuingizwa kwenye kabrasha la Mauzo ulikuwa tofauti na hali halisi ya korosho baada ya Mnunuzi kununua na kwenda kuhakiki ubora wa korosho hizo hata kupelekea baadhi ya wanunuzi kukataa kulipia/kudai fidia;

#### *9.4.11.4. Upungufu Wa Kiasi Cha Korosho Kwa Wanunuzi*

Baadhi ya Wanunuzi walipata kiasi cha korosho pungufu na kiasi walichonunua;

### 9.4.12. MAPENDEKEZO

Yafuatayo ni mapendekezo katika kuboresha mauzo ya Korosho kwa msimu ujao wa 2025/26:

#### *9.4.12.1. Suala la Ubora wa Korosho kabla Mnada*

Uwepo mkakati maalumu wa kusimamia na kuhakikisha suala la ubora wa korosho unaowasilishwa na watunza ghala unaendana ubora halisi wa korosho hususani katika minada ya mwishoni. Ikiwezekana katika minada ya mwisho Bodi ya Korosho ifanye uhakiki wa ubora wa Korosho kabla ya kuzipeleka sokoni ili kujiridhisha;

#### *9.4.12.2. Uhakiki wa uwepo wa Korosho Kabla ya Mnada*

Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho na Vyama, ifanye uhakiki wa uwepo wa Korosho ghalani hasa kwa minada ya mwishoni mwa msimu ili kuepuka kuuza mzigo hewa.

#### *9.4.12.3. Fidia kwa Wanunuzi wanaokosa Korosho baada ya Kulipia*

Wanunuzi wanaokosa Korosho ghalani walipwe fidia kwa wakati kama mwongozo unavyotaka hasa baada ya kuhakiki madai yako ili kulinda na kujenga Imani kwa Wanunuzi kulingana na taarifa tunazowapatia kupitia kabrasha la mauzo;

#### *9.4.12.4. Maeneo ya yatakayo chaguliwa kuonyesha minada*

Ili wadau na wakulima waweze kushuhudia minada mubashara inashauriwa maeneo hayo yazingatie upatikanaji mzuri wa mtandao wa *internet.*

### 9.4.13. MAANDALIZI YA MAUZO YA KOROSHO MSIMU WA 2025/2026

Katika kuhakikisha Soko la Bidhaa linashiriki kikamilifu katika kuwezesha mauzo ya Zao la Korosho kwa Msimu wa 2025/26 kwa kushirikiana na wadau wengine, yafuatayo yamefanyika: -

i). Soko la Bidhaa linaendelea kutoa mafunzo kwa wanunuzi na wadau wengine kipindi cha msimu wa Ufuta na Mbaazi 2025/2026 kwa mikoa inayozalisha zao la Korosho ili waweze kuelewa mfumo wa mauzo wa kidijitali pamoja na majukumu yao;

ii). Soko la Bidhaa Tanzania limeshiriki katika maandalizi ya Mwongozo wa Mauzo wa Korosho Msimu wa 2025/2026;

iii). Soko la Bidhaa limeendelea kuboresha mfumo wa mauzo kulingana na maoni ya wadau;

iv). Soko la Bidhaa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao, limeendelea kuboresha usalama wa mfumo wa mauzo;

v). Kuongeza idadi ya watumishi katika Soko la Bidhaa kwa ajili kuendana na ongezeko la majukumu ili kuweza kusimamia uendeshaji wa minada katika mikoa yote wakati wa msimu wa mauzo;

vi). Katika kipindi cha msimu wa Mauzo ya Korosho, Soko la Bidhaa kuendelea kutumia Ofisi zake zilizopo katika ofisi za Bodi ya Korosho mkoa wa Mtwara kutoa huduma kwa wadau mbali mbali katika tasinia ya Korosho;

vii). Kuboresha mawasiliano na uratibu pamoja na wadau wakuu ikiwemo WRRB, TCDC, Bodi ya Korosho, Vyama vya Ushirika, Halmashauri, Mamlaka za Serikali za Mikoa na Wilaya ili kuongeza ufanisi.

viii). Kuandaa Program ya mafunzo kwa wadau yatakayo tolewa mapema kabla ya kufunguliwa kwa msimu wa 2025/26.

### 9.4.14. HITIMISHO

Soko la Bidhaa Tanzania lipo tayari kushirikiana na wadau wote kwa msimu wa mauzo wa 2025/26 na linaendelea kupokea maoni mbalilmbali kwa ajili ya kuboresha mauzo kwa njia ya kielekitroniki.

**AGENDA NA.9.5: TAARIFA YA MAANDALIZI YA USAFIRISHAJI WA KOROSHO KUPITIA BANDARI YA MTWARA (TPA – MTWARA) KWA MSIMU WA MWAKA 2025/2026**

## 9.5. TAARIFA YA MAANDALIZI YA USAFIRISHAJI WA KOROSHO KUPITIA BANDARI YA MTWARA (TPA – MTWARA) KWA MSIMU WA MWAKA 2025/2026

### 9.5.1. Utangulizi

Bandari ya Mtwara imeendelea kutekeleza maelekezo yaliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa tarehe 15 Septemba, 2023 katika ziara yake Mkoani Mtwara ambapo alielekeza kuwa, Korosho zote ghafi zinazozalishwa katika Mikoa ya Kusini mwa Tanzania zisafirishwe kupitia Bandari ya Mtwara.

Mbali na maelekezo hayo, Mheshimiwa Rais alizitaka Mamlaka zinazohudumia zao la Korosho kushirikiana na wadau katika kujadili changamoto mbalimbali zinazolikabili zao hilo**.**

### 9.5.2. Utekelezaji wa usafirishaji wa shehena ya korosho kwa mwaka 2024/2025

Upatikanaji wa Meli, Makasha na Shehena iliyosafirishwa:

i. Katika msimu wa 2024/2025, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2025 jumla ya tani 370,896 za korosho zimehudumiwa kwa kusafirishwa kwenda Nchi za nje ikilinganishwa na tani 253,616.94 zilizohudumiwa katika msimu wa korosho wa mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 46.2 ikiwa ni kiwango cha juu zaidi ya malengo ya TPA ya kuhudumia tani 200,000 na zaidi ya makisio ya uzalishaji wa korosho tani 300,000 yaliyotolewa na Bodi ya Korosho Tanzania kwa kiwango cha asilimia 85 na 23.6 mtawalia. Shehena hiyo ya korosho kwa msimu wa mwaka 2024/2025 imesafirishwa kwenda Nchi za India tani 271,781 na Vietnam tani 99,115 ambapo mwaka 2023/2024 jumla ya tani za mapato 161,364 zilisafirishwa kwenda nchi za India na tani 92,253 Vietnam sawa na ongezeko la asilimia 68% na 7% mtawalia kwa kulinganisha na mwaka 2024/2025.

ii. Katika msimu wa Korosho wa mwaka 2024/2025, jumla ya Meli 36 zimehudumiwa ikilinganishwa na jumla ya Meli 28 zilizohudumiwa katika msimu wa mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 28.6.

### 9.5.3. Changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji

Katika kutekeleza zoezi la usafirishaji wa korosho kupitia Bandari ya Mtwara, changamoto zifuatazo zilijitokeza:

i. Upungufu wa mitambo ikiwemo Reach Stackers, Empty Handlers, Gottwalds, Terminal Tractors na Mobile Cranes.
ii. Ufinyu wa eneo la kufungashia Korosho (Stuffing) wakati wa zoezi la usafirishaji kutokana na wingi wa makasha.
iii. Msongamano wa Meli Miezi ya November, 2024 – Februari, 2025.

### 9.5.4. Hatua zilizochukuliwa kutatua changamoto

i. Bandari ya Mtwara imeongeza idadi ya mitambo miwili ya kushusha na kupakia shehena kwenye meli (Mobile Harbor Cranes za Tani 63 na 100). Aidha, mitambo miwili (2) ya *Reachsteaker* imefanyiwa ukarabati mkubwa hivyo kufanya jumla ya *Reachstaker* tatu (3) zinazomilikiwa na Mamlaka kutumika kipindi cha msimu.
ii. TPA inaendelea kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya ununuzi wa mitambo zaidi ili kwenda sambamba na ukuaji wa Bandari ya Mtwara katika kuhudumia shehena. Kwa sasa zoezi la kusimika mtambo mpya wa kisasa wa kuhudumia Makasha (SSG) wenye thamani ya takriban Shilingi Bilioni 52.5 linaendelea na linatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2025.
iii. Bandari ya Mtwara ilifanikiwa kukodisha TTs na Reachstacker kwa kushirikiana na Sekta Binafsi ili kuongeza ufanisi kwenye uhudumiaji wa Shehena.
iv. Maeneo yenye jumla ya ukubwa wa mita za mraba takriban 60,000 yalitengwa na kuboreshwa kwa ajili ya kuhifadhia shehena ya makasha.
v. Bandari ya Mtwara kwa kushirikiana na sekta binafsi ilihamasisha uwekezaji kwenye huduma za CFSs iliyosababisha uwepo wa CFSs mbili (2) zilizoshiriki kuhudumia makasha kwenye msimu wa 2024/2025 ambapo jumla ya Makasha 2,774 yenye jumla ya Tani 85,484 za Korosho yamehudumiwa kwenye *CFSs* hizo.
vi. Bandari ilichukua hatua ya kuhudumia kwanza meli ambazo zilikuwa na utayari kwa maana zilizokamilisha malipo yote husika pamoja na meli ambazo mzigo wake ulikuwa tayari kupakiwa. Hatua hii iliwezesha kukabiliana na

changamoto ya msongamano ambayo ilisababishwa na wateja wenyewe kutofanya mapema maandalizi ya kimsingi kabla meli hazijawasili Bandarini.

### 9.5.5. Mipango ya kuhudumia korosho katika msimu wa mwaka 2025/2026

Katika msimu wa mwaka 2025/2026 Bandari ya Mtwara imejipanga kusafirisha shehena ya korosho kama ifuatavyo:

i. Bandari kuendelea kushirikiana na wadau wengine ikiwemo sekta binafsi wakati wote wa zoezi la usafirishaji wa shehena ya korosho ili kuondoa changamoto zinazoweza kujitokeza.

ii. Kuendelea kusisitiza ufanyikaji wa shughuli za ufungashaji wa korosho (stuffing) zifanyike nje ya eneo la Bandari (Kutumia CFS za wamiliki waliopo katika sekta binafsi) ili kupunguza changamoto ya ufinyu wa maeneo.

iii. Bandari imeongeza mtambo mwingine wa SSG ambao unafanya idadi ya mitambo hiyo kuwa miwili (2) kwa lengo la kuongeza ufanisi wakati wa zoezi la usafirishaji wa korosho.

iv. Bandari imeandaa mpango mahsusi wa kukodi mitambo mingine zaidi wakati wa zoezi la kuhudumia shehena ya korosho ili kuondoa changamoto zinazoweza kujitokeza ya kuharibika kwa baadhi ya mitambo hali inayoweza kuzorotesha shughuli za utekelezaji.

v. Bandari imeongeza idadi ya wafanyakazi kwa ajili ya kusimamia shughuli za utekelezaji kwa kufanyika kwa muda wa siku saba saa ishirini na nne (24/7) ili kuongeza ufanisi wa utendaji.

### 9.5.6. Hitimisho

Bandari ya Mtwara imefanikiwa kutekeleza maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kusafirisha korosho yote iliyowasilishwa Bandarini. Mafanikio hayo yametokana na ushirikiano mkubwa wa Watumishi wa Bandari pamoja na ushirikiano wa karibu kati ya Bandari na Wadau wote wanaohusika katika mnyororo mzima wa thamani wa zao la Korosho. Ni matumaini yetu kuwa, ushirikiano huu utadumishwa na kuimarika zaidi katika msimu ujao wa mwaka 2025/2026.

**AGENDA NA 10.0: TAARIFA YA MAENDELEO YA UTAFITI WA ZAO LA KOROSHO NCHINI**

## 10. TAARIFA YA MAENDELEO YA UTAFITI WA ZAO LA KOROSHO NCHINI

### 10.1 Utangulizi

Nchini Tanzania, Korosho ni zao kuu la kibiashara na miongoni mwa mazao 13 ya kimkakati. Zao hili limeendelea kuwa la muhimu na kulimwa kwa wingi nje na ndani ya nchi yetu. Hii ni kutokana na sababu kuwa uhitaji wa korosho na bidhaa zake katika soko la ndani pamoja na nje ya nchi umeendelea kuwa mkubwa. Na hii imepelekea hapa Tanzania ufanyike utafiti na kuongeza maeneo ya uzalishaji korosho kutoka mikoa mitano ya awali hadi kufikia zaidi ya kumi na saba.

Pamoja na umuhimu wa zao hili la korosho nchini, bado zipo changamoto mbali mbali zinazowakabili wakulima na wadau mbalimbali katika mnyororo mzima wa zao hili kuanzia uzalishaji mpaka uongezaji wa thamani. Hivyo, ili kutatua changamoto hizo Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara ya Kilimo kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kituo cha Naliendele imekuwa ikitekeleza jukumu la kufanya utafiti kwenye zao la Korosho ili kutatua changamoto zinazowakabili wakulima na wadau wa korosho.

TARI kupitia kituo cha Naliendele pamoja na majukumu mengine ina jukumu la kufanya utafiti kwenye zao la korosho kama ifuatavyo:-

i. Kugundua na kuzalisha mbegu bora za korosho
ii. Kubaini na kupendekeza njia bora za uzalishaji miche bora ya korosho
iii. Kuanzisha mashamba ya kuzalishia vikonyo kwaajili ya kubebeshea miche
iv. Kubaini na kupendekeza maeneo yanayofaa kwa kilimo cha korosho
v. Kutafiti teknolojia za kilimo bora cha korosho na kupendekeza kwa wakulima
vi. Kubaini mbinu za kudhibiti magonjwa na wadudu waharibifu wa korosho
vii. Kugundua viuatilifu hai vya kudhibiti magonjwa na wadudu waharibifu wa korosho
viii. Kubaini wadudu rafiki wa zao la korosho na namna ya kuwatumia
ix. Kubaini mbinu za kuboresha na kufufua mashamba ya korosho yaliyotelekezwa
x. Kubaini na kutumia mbinu za bayoteknolojia katika kuzalisha mbegu bora za korosho
xi. Kufanya utafiti wa udongo na matumizi bora ya ardhi kwenye zao la korosho
xii. Kutafiti mbinu za uongezaji thamani korosho na mabibo

xiii. Kutoa elimu kwa maafisa ugani juu ya teknolojia zilizopendekezwa katika kilimo cha zao la Korosho

### 10.2 Uzalishaji wa mbegu na miche bora za korosho

Uzalishaji wa mbegu na miche bora ya korosho inazalishwa na kituo cha TARI Naliendele na vituo vidogo vilivyo chini ya TARI Naliendele. Vituo hivyo vijulikanavyo kama vituo vya uendelezaji zao la korosho yaani ‘Cashewnuts Development Centres, CDCs), ambavyo ni:- Nyangao (Lindi Vijijini), Nanyanga (Tandahimba), Nakayaya (Tunduru), Mkuranga (Mkuranga), Mkumba (Nachingwea), Mtopwa (Newala) na Chambezi (Bagamoyo). Vituo hivi vilianzishwa karibu na wakulima kwenye mikoa inayolima korosho ambayo ni Mtwara, Lindi, Pwani, Tanga na Ruvuma. Pia mashamba ya kuzalishia mbegu za korosho yameongezwa katika maeneo ya Lusewa na Paradiso mkoani Ruvuma, Manyoni Mkoa wa Singida,Tumbi katika mkoa wa Tabora, Pangani na Mkinga katika mkoa wa Tanga. Kupitia vituo hivi tumeendelea kutoa huduma mbalimbali ambapo wadau wanaozunguka maeneo husika huweza kutembelea vituoni na kupata elimu ya kanuni za kilimo bora cha zao la korosho .

Aidha, ili kuhakikisha wakulima wanapata huduma kwa urahisi ikiwemo upatikanaji wa mbegu bora, miche na elimu ya kanuni bora za kilimo cha korosho, TARI Naliendele imeendelea kujengea uwezo wataalam mbalimbali wakiwemo wa vituo vingine kama vile TARI Tumbi, TARI Makutupora na TARI Mikocheni ili waweze kusaidia kutoa huduma ya kilimo bora cha korosho kwenye mashamba/ vituo vya uendelezaji wa zao la korosho kwa kuwa vituo hivi vya TARI viko jirani na mashamba ya korosho ya TARI Naliendele.

 

**Picha:** Mbegu na miche bora ya korosho inayozaliwa na kituo cha TARI Naliendele,

| 2.0. Kazi za program ya korosho zilizofanyika katika mwaka wa Fedha 2023/2024 | | | |
|---|---|---|---|
| **Na** | **KAZI** | **MAFANIKIO** | **KAZI ZINAZOENDELEA** |
| 1 | Uzalishaji wa mbegu bora za korosho | Uzalishaji wa mbegu umeongezeka na kufikia tani 59 katika msimu wa 2024/2025 ukilinganisha na tani 30.38 kwa msimu wa 2023/2024. Ongezeka hili la uzalishaji wa mbegu ni sawa na asilimia 194.2. | Uzalishaji wa mbegu bora za korosho unaendelea kwa msimu wa 2025/2026. |
| 2 | Uzalishaji miche ya zao la korosho | Kwa msimu huu 2024/2025 uzalishaji wa miche umeongezeka hadi kufikia miche 1,350,000 ukilinganisha na miche 318,928 kwa msimu wa mwaka 2023/2024. Ongezeka hili la uzalishaji wa miche ni sawa na asilimia 423.2. Aidha uzalishaji wa miche iliyobebeshwa yenye ukinzani na ugonjwa wa blaiti unaendelea hadi sasa tumeshabebesha miche 500,000 na miche itaanza kupatikana mapema mwanzoni mwa msimu wa 2025/2026 | Uzalishaji wa miche utaendelea kulingana na mahitaji ya wakulima |
| 3 | Uanzishwaji na uendelezaji wa Mashamba ya mbegu bora za korosho | Jumla ya ekari 40 zaidi za Mashamba mapya ya kuzalisha mbegu bora za korosho yameongezwa katika eneo la Nyangao, Lindi na sasa kufikia jumla ya ekari 403 ya mashamba ya mbegu bora za korosho. | Mashamba tayari yanazalisha mbegu na yanaendelea kuhudumiwa |
| 4 | Uanzishaji wa Mashamba ya vikonyo vya mbegu mpya 8 | Jumla ya ekari 16 zenye mikorosho 432 zimebebeshwa kwa ajili ya kuzalisha vikonyo vya kuzalishia miche ya mbegu mpya kama ifuatavyo;- Naliendele ekari 4.5, Mtopwa 2, Nanyanga 2.5, Nachingwea ekari 5 na Tunduru ekari 2 | Kuendelea kuhudumia mashamba haya ili yazalishe vikonyo kwa ajili ya kubebesha miche yenye ukinzani na blaiti. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 5 | Ugunduzi wa mbegu bora za korosho dhidi ya ugonjwa wa blaiti | Taasisi imefanikiwa kugundua aina mpya nane (8) za zao la korosho zenye ukinzani na ugonjwa wa blaiti. Aina hizo za Mbegu ni TARIKO 1, TARIKO 2, TARIKO 3, TARIKO 4, TARIKO 5, TARIKO 6, TARIKO 7 na TARIKO 8. Ugunduzi huu, utasaidia kupunguza matumizi ya Viuatilifu vya magonjwa. | Kuendelea kutunza mikorosho mama ya aina hizi 8 |
| 6 | Utafiti wa aina 18 za mbegu zinazozaa mapema zinaemdelea kufanyiwa utafiti | Huu ni mwaka wa 5 na takwimu zinaonesha kati ya aina 18 aina tano (5) zinazaa mapema. | Kuendelea na uchunguzi wa mbegu hizi katika mashamba ya wakulima kwa mazingira tofauti |
| 7 | Aina 35 za mbegu za korosho kwa ajili ya Uzalishaji wa mabibo | Huu ni mwaka wa tano, utafiti unaendelea na takwimu zinaendelea kuchukuliwa. | Kuendelea na utafiti pamoja na kuchukua takwimu |
| 8 | Kufanya Utafiti wa Mbolea kwenye korosho | Matokeo ya awali yameonesha mbolea za kwenye majani, aina tatu zinafanya vizuri. Aidha taasisi inafanya uidhinishaji wa ufanisi wa mbolea hizo. Na matokeo ya ufanisi huu yatakuwa tayari musimu wa 2025/2026 | Utafiti unaendelea ili kuthibitisha na kuidhinisha ufanisi wa aina tatu za Mbolea zilizopendekezwa awali |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 9 | Mbinu za kudhibiti magonjwa na wadudu waharibifu | ➢ Taasisi imefanikiwa kupanua wigo wa Viambata Amilifu; ambapo viuakuvu aina ya *azoxystrobin, carbendazim na propamorcarb hydrochloride* vimeongezeka kwa ajili ya Magonjwa (Blaiti na Ubwiriunga), na;<br>Viuadudu *aina ya Abamectin, emamectin benzoate, Imidaclopid, Imidaclopin,* vimeongezeka kwa ajili ya wadudu waharibifu wa korosho.<br>➢ Viuakuvu vya asili vya Wadudu aina ya Pyrethrin vinavyotokana na Pareto, vimeonesha ufanisi mzuri wa awali kwenye kudhibiti Wadudu wa mikorosho, matokeo haya yatasaidia kupunguza matumizi ya Viuati kikemikali. | ➢ Kufanya utambuzi wa visumbufu vipya na kufuatilia maendeleo ya visumbufu vya zamani katika misimu ya korosho.<br><br>➢ Kuthibitisha na kuidhinisha mbinu za kibaiolojia ikiwemo viuakuvu vya kibaiolojia *(biopesticide)*. Pia biolojia-mimea *(botanical pesticides) unaendelea* |
| 10 | Utafiti wa ugonjwa wa Mnyauko fusari | Taasisi imefanikiwa kuthibitisha mbinu mbili ambazo zimeweza kudhibiti ugonjwa wa Mnyauko Fusari; nazo ni<br>a. Matumizi ya viuakuvu vya kibaiolojia jamii ya *Bacillus spp.,* na *Trichoderma sp.,* vimefanikiwa kukinga mikorosho kabla ya kushambuliwa.<br>b. Matumizi ya Viuakuvu vya kemikali jamii ya Carbendazim, Azoxystrobin, Thiophanate methyl na Propamorcarb hydrochloride vikiambatana na mbinu ya ubebeshaji wa mikorosho ilioathirika. | ➢ Kuendelea na program ya kudhibiti ugonjwa wa Mnyauko Fusari katika mashamba ya korosho.<br><br>➢ Kutoa elimu kwa wakulima juu ya matumizi ya njia za kudhibiti ugonjwa wa mnyauko fusari. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 11 | Uongezaji thamani wa korosho na mabibo | ➢ Thamani ya bibo imeongezwa na kuzalisha “*Ethanol”* na nyama ya mabibo<br><br>➢ Utafiti wa awali wa aina mbili za “*Mbolea ya mabibo”* ikiwemo; Mbolea ya maji na Mbolea ya unga unaendelea.<br><br>➢ Thamani ya korosho imeongezwa kwa kuzalisha “maziwa”, Siagi, na unga wa korosho | ➢ Kuendelea kuongeza thamani ya bibo ili kupandisha kiwango cha ethanol mpaka angalau asilimia 95. Aidha Ujenzi wa kiwanda chenye uwezo wa kutafiti na kuzalisha ethanol unahitajika.<br><br>➢ Kuendeleza utafiti lengo ni kupata mbolea hai inayotokana na mabibo<br><br>➢ Kuboresha kiwanda cha Utafiti na ubanguaji wa korosho. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 12 | Kutoa elimu ya kilimo bora cha zao la korosho kwa kushirikiana na wadau mbalimbali | ➢ Jumla ya Maafisa ugani 928 kati ya hao 395 ni kupitia BBT wamepewa elimu juu ya kilimo bora cha zao la korosho<br>➢ Maafisa ugani 928 wamefundishwa matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwenye zao la korosho<br>➢ Jumla ya washiriki 312 katika eneo la mashamba ya Pamoja ya Masigati walipata elimu juu ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu<br>➢ Jumla ya mashamba 42 yenye ukubwa wa eka moja kila shamba yalitumika kama mashamba ya mfano na kupewa huduma ya upuliziaji wa viuatilifu<br>➢ Teknolojia ya ufufuaji wa mashamba pori imetolewa kwa kushirikiana na halmashauri za wilaya kwa mikoa ya Mtwara na Pwani; ambapo mashamba 19 yamefufuliwa mkoa wa Mtwara na 6 mkoa wa Pwani.<br><br>Teknolojia ya utunzaji wa mashamba na udhibiti wa visumbufu zimetolewa kwa kuanzisha mashamba 32 ya mfano (Demonstration Plots): ambapo 8 kutoka Lindi, 15 Mtwara, 3 Ruvuma na 6 Pwani | Kuendelea kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali kwa njia ya mafunzo ya ana kwa ana, mashamba ya mfano/darasa, na vyombo vya habari |

**Picha za huduma mbalimbali**





**Picha:** Uanzishaji na uendelezaji wa mashamba mapya ya mbegu na mashmba ya vikonyo





**Picha:** Mafunzo ya Kilimo bora cha zao la korosho juu ya upandaji na upogoleaji





**Picha:** Mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu








**Picha:** Uongezaji thamani wa zao la korosho kupata bidhaa mbalimbali

## 10.3 Changamoto

### 10.3.1 Mabadiliko ya Hali ya Hewa

Kituo kimeendelea kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwenye zao la korosho. Kunyesha mvua kipindi cha uzalishaji wa korosho, baridi kali pamoja na masaa machache ya kuwaka jua kwa siku vimekuwa vikichangia korosho kutokufanya vizuri. Hata hivo kwa takwimu za mwaka huu kwa kipindi cha mwezi wa sit ana was aba, Pamoja na kuwepo mvua na unyevu mwingi angani bado haijaleta athali kwenye mikrosho (Jedwali Na 1).

Hali ya mazingira ya mvua na unyevu kwenye misimu ya Uzalishaji wa korosho.

| **Hali ya hewa** | **Mwezi (Juni-Septemba 2020-2024 na Juni-Julai 2025** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** |
| Mvua za nje ya msimu (mm) | 21.18 | 30.94 | 39.02 | 42.1 | 9 | 24.7 |
| Unyevu angani (%) | 67 | 70 | 73 | 70.3 | 70 | 71 |
| Jumla ya siku za mvua | 4 | 8 | 12 | 11 | 5 | 6 |

### 10.3.2 Milipuko ya Magonjwa

Kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, kumekuwa na milipuko ya magonjwa na wadudu waharibifu ndani ya msimu wa uzalishaji wa korosho katika maeneo mbalimbali. Magonjwa kama vile blaiti, ubwiriunga, vithiripi na ugonjwa wa chule huwa ni changamoto kwenye zao la korosho hasa usipodhibiti.





Picha: Mashamblizi ya ugonjwa wa ubwiriunga na wadudu waharibifu (Mbu wa mikorosho)

### 10.4 Kazi zinazoendelea ni Pamoja na:-

i. Kuthibitisha na kuidhinisha ufanisi wa aina tatu za Mbolea zinazoonesha kufanya vizuri kwa msimu wa 2025/2026
ii. Kuzalisha mbegu bora za korosho tani 100
iii. Kuendelea kutunza mashamba ya mbegu
iv. Kuzalisha miche bora milioni tatu (3,000,000) ya mikorosho ikiwemo kituo cha Masigati Manyoni mkoani Singida
v. Kuendeleza mashamba ya vikonyo ikiwemo mashamba ya vikonyo vya mbegu bora 8 zilizosajiliwa mwaka jana
vi. Kuendeleza Utafiti wa aina 35 kwa ajili ya uzalishaji wa mabibo
vii. Kuendeleza Utafiti wa aina18 za korosho zinazozaa mapema (early yielding)
viii. Kufanya utambuzi wa visumbufu vipya na kufuatilia maendeleo ya visumbufu vya zamani katika misimu ya korosho
*ix.* Kuthibitisha na kuidhinisha mbinu za kibaiolojia ikiwemo viuakuvu vya kibaiolojia *(biopesticide)*. Pia biolojia-mimea *(botanical pesticides) unaendelea*

x. Kuendelea na program ya kudhibiti ugonjwa wa Mnyauko Fusari katika mashamba ya korosho kwa mpango ujulikanao ‘Ondoa mnyauko fusari linda uzalishaji’
xi. Kuendelea kusimamia program ya ‘Ondoa mapori ongeza uzalishaji’ kwa kushirikiana na maafisa ugani wakiwemo wa BBT
xii. Kufanya ugunduzi wa mashine rahisi ya kutenganisha bibo na korosho karanga
xiii. Kubaini mbinu ya kuukinga mkorosho zidi ya mabadiliko ya tabia nchi
xiv. Kutoa elimu kwa maafisa ugani juu ya kilimo bora cha zao la korosho
xv. Kuongeza thamani kwenye zao la korosho ikiwemo kiwango cha pombe kwenye wine

### 10.5 Utekelezaji wa Miradi miwili (2) inayofadhiliwa na European Union (EU) kwa kushirikiana na BMZ ujerumani kupitia GIZ

TARI Kituo cha Naliendele itaanza kutekeleza miradi miwili (2) kwenye zao la korosho kama ifuatavyo:-

**Mradi 1: ‘***Development of Climate Resilient Pests and Diseases Management Strategies for Improving Livelihood Standards of Cashew Growers in Tanzania and Mozambique’*

Mradi huu una malengo mahususi kama ifuatavyo;

i. Kufanya utafiti Zaidi kwenye visumbufu vya wadudu na magonjwa
ii. Kupata kiuatilifu hai kwa ajili ya kudhibiti magonjwa na wadudu waharibifu wa korosho
iii. Kuwa na teknolojia ya kumwezesha mkulima kutambua visumbufu na mbinu za kutatua changamoto hizo kwa kutumia simu ya mkononi
iv. Kutoa elimu kwa maafisa ugani angalau 1000 namna ya kutumia teknolojia ya simu katika kutambua magonjwa na wadudu waharibifu kwenye zao la korosho

**Mradi wa 2 ‘***Enhancing the Utilization of Cashew Apple for Climate Resilient, Increased Income and Food Security of Smallholder Farmers in Tanzania and Mozambique’*

## 10.6 Malengo mahususi ya mradi huu ni:-

i. Kuzalisha mbolea hai kwa kutumia mabibo ya korosho
ii. Kuzalisha vyakula vyenye vitamini C kutoka kwenye mabibo ya korosho
iii. Kushirikiana na taasisi ya Utafiti ya Msumbiji katika kuongeza thamani ya mabibo kukaa kwa muda mrefu kabla ya kuyatumia kwa kazi mbali mbali

## 10.7 Utekelezaji wa Mkakati wa kuboresha Maisha ya mwananchi wa Mtwara na Lindi kwa kufungua fursa za kilimo cha mazao ya chakula hasa Mahindi, Mpunga na Mbogamboga ujulikanao kama 'Beyond Cashew Crops (BCC): A strategy to unlock food and horticultural crops opportunities in Lindi and Mtwara regions, Tanzania'

Wananchi wengi wa vijijini katika Mikoa ya Lindi na Mtwra, pamoja na kuimarika kwa soko la Korosho, Ufuta na Mbaaazi ambalo huwafanya waongeze kipato, bado maendeleo yao hayatakua kwa kasi inayostahili kwani hutumia pesa nyingi kwa ajili ya kununulia chakula hasa Mahindi na Mchele. Ili kufanikisha mkakati huu, malengo mahususi Matano yatatekelezwa kama ifuatavyo;

i. Kuainisha aina ya mbegu za Mahindi na Mpunga zinazofaa kwa Mazingira ya Lindi na Mtwara
ii. Kuzalisha Mbegu za Mahindi na Mpunga na mboga mboga zinazofaa kwa mazingira ya Lindi na Mtwara na kuzisambaza kwa wakulima
iii. Kuainisha mbolea zinazofaa kwa mazingira ya Mtwara na Lindi katika Kilimo cha Mahindi na Mpunga na kuhamasisha matumizi yake
iv. Kuainisha mbogamboga zinazokubalika na kupendwa kwa wakulima wa Mtwara na Lindi
v. Kutambua aina ya kilimo na aina ya mazao yanayoweza kuchanganywa na Mahindi kwa kilimo chenye tija
vi. Kutoa elimu ya kilimo bora cha Mahindi, Mpunga na Mbogamboga

## 10.8 Mwelekeo wa Msimu wa Korosho 2025/2026

Pamoja na mvua za wastani hadi juu ya wastani zilizotabiriwa na Mamlaka ya hali ya hewa (TMA) na kunyesha hasa maeneo mengi yanayolima zao la korosho kwa kipindi cha Novemba/Disemba 2024 mpaka April/May 2025, bado kutakuwa na uzalishaji mzuri kwani mvua kubwa za msimu 2023/2024 bado zimefanya kiwango cha maji kuwa kizuri kwa mazao jamii ya miti ukiwemo mkorosho.

Kipindi cha kuanzia Mwezi Juni Mpaka Agosti 2025 kumekuwa na baridi zaidi ukilinganisha na mwaka 2024. Pia mvua imenyesha kwa siku 6 ndani ya mwezi Juni 2025 ukilinganisha na siku moja kwa mwezi huo huo wa Juni kwa mwaka 2024. Hali hii imepelekea kuchelewa kwa hatua mbali mbali za mkorosho ikiwemo kuchelewa kuweka maua na tegu hata kwa maeneo yanayowahi. Hata hivyo kwa kipindi hiki cha mwezi wa nane, joto limeanza kuongezeka na kupelekea mikorosho kuendelea kutoa maua na tegu kwa wingi.

Aidha uzalishaji wa tija utategemea matumizi sahihi ya teknolojia zilizopendekezwa kama vile matumizi sahihi na salama ya viuatilifu, matumizi ya mbegu bora na kilimo bora cha korosho kwa ujumla.

## 10.9 Hitimisho

TARI Kituo cha Naliendele, kinaendelea na Shughuli mbalimbali za Utafiti wa zao la korosho ili Kuongeza tija ya Uzalishaji. Pia tunashukuru kwa Serikali na wadau wetu kwa mazingira wezeshi yanayotusaidia kufanikisha utafiti kwa lengo la kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wakulima pamoja na wadau wengine katika mnyororo mzima wa zao.

## AGENDA NA 11.0  UTOAJI WA TUZO KWA WADAU MBALIMBALI

**AGENDA NA 12.0 MENGINEYO**

**AGENDA NA 13.0 KUFUNGA MKUTANO**


BODI YA KOROSHO TANZANIA